SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR



# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

## KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

## AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**
2 Mtaa wa Tume, S.L.P 258, 71125 Kilimani Zanzibar
Simu/Nukushi: +255 24 223 400, Barua Pepe: info@ocagz.go.tz
Tovuti: www.ocagz.go.tz

**MAREJEO NAM: CAC.132/385/01/4** **TAREHE: 26 MACHI, 2024**

**MHE. DKT HUSSEIN ALI MWINYI,**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI,**
**AFISI YA RAIS IKULU,**
**S.L.P. 437,**
**ZANZIBAR, TANZANIA.**

**KUH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

---

Ninayo furaha kuwasilisha kwako Ripoti ya Mwaka inayohusu Ukaguzi wa Hesabu za Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023.

Naomba kuwasilisha.

Ahsante.

.........................................

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU**
**WA HESABU ZA SERIKALI**
**ZANZIBAR.**

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

## Mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka.

## Dira

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi.

## Dhamira

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa.

## MISINGI YA MAADILI YA UKAGUZI

1. **Uaminifu**
Kuhakikisha Afisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia Sheria.

2. **Uadilifu**
Kuwa ni Afisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.

3. **Kuwa Huru**
Kuwa ni Afisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa Sheria.

4. **Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi**
Kuwa ni Afisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.

5. **Kutunza Siri**
Kuwa ni Afisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.

6. **Uwazi na Uwajibikaji**
Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma

# YALIYOMO


YALIYOMO........................V
ORODHA YA MAJADWELI........................X
ORODHA YA PICHA........................XIV
VIFUPISHO........................XV
SHUKURANI........................XVII
DIBAJI........................XIX
MUHTASARI........................XXI
**SURA YA KWANZA**........................1
1.0 TAARIFA ZA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAGULIWA........................1
1.1 UTANGULIZI........................1
1.2 MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023........................1
1.3 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA........................3
1.4 MIRADI ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA UKAGUZI........................4
1.5 MIRADI AMBAYO HAIKUANDALIWA TAARIFA ZA FEDHA ZA MWISHO WA MWAKA (FINANCIAL STATEMENT) KWA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023........................6
1.6 WAJIBU WA MAAFISA MASUULI........................9
1.7 WAJIBU WA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI........................9
1.8 UPEO NA VIWANGO VYA UKAGUZI VINAVYOTUMIKA........................10
1.8.1 UPEO WA UKAGUZI........................10
1.8.2 VIWANGO VYA UKAGUZI VILIVYOTUMIKA........................10
1.9 MBINU ZA UKAGUZI ZILIZOTUMIKA........................11
**SURA YA PILI**........................13
2.0 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MWAKA ULIOPITA NA HATI ZA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023........................13
2.1 HALI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI ULIOPITA........................13
2.2 HATI ZA UKAGUZI........................14
2.2.1 AINA YA HATI ZA UKAGUZI........................14

2.3 MSINGI WA HATI ZA UKAGUZI ....................................................15

2.4 MWENENDO WA HATI ZA UKAGUZI ZILIZOTOLEWA ..................16

**SURA YA TATU** ...........................................................................20

3.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI NA UTENDAJI WA KIFEDHA..................20

3.1 UTANGULIZI ............................................................................20

3.1.1 MRADI WA ISP - DRMNRG ..................................................20

3.1.2 MRADI WA UKUZAJI UCHUMI JUMUISHI ZANZIBAR - (BIG-Z.....................................................................................21

3.1.3 MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA SEKONDARI ZANZIBAR (ZISP).......................................................................21

3.1.4 MRADI WA ELIMU YA JUU KWA MABADILIKO YA KIUCHUMI (HEET)........................................................................................22

3.1.5 MRADI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA WA ELIMU AWAMU YA PILI (GPE II).........................................................................23

3.1.6 MRADI YA UJENZI NA UWEZESHAJI WA SHULE ZA SEKONDARI (BADEA II)...........................................................23

3.2 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ..............................24

3.2.1 MRADI WA USIMAMIZI WA UVUVI NA UKUAJI WA PAMOJA KUSINI MAGHARIBI MWA BAHARI YA HINDI (SWIOFish)...................................................................................24

3.2.2 MRADI WA MAENDELEO YA KILIMO NA UVUVI (AFDP)........25

3.2.3 MRADI WA MABADILIKO NA UPATIKANAJI WA SEKTA YA NISHATI ZANZIBAR (ZESTA)...............................................25

3.2.4 MRADI WA MSAADA WA SEKTA YA NISHATI ZANZIBAR - ZESS......................................................................................25

3.2.5 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TANZANIA (TASAF)........26

3.2.6 MFUKO WA FEDHA WA HUDUMA YA AFYA ZANZIBAR (ZANZIBAR HEALTH BASKET FUND)....................................27

3.2.7 PROGRAMU YA CHANJO – EPI (GAVI)................................28

3.2.8 MRADI WA KUSAIDIA SEKTA YA UCHUKUZI - TSSP ...........29

3.2.9 MRADI WA MPANGO WA CHAKULA KATIKA SKULI ZA MSINGI....29

**SURA YA NNE**....32

4.0 DOSARI ZILIZOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA TAASISI ZA UMMA....32

4.1 WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI....32

4.1.1 MRADI WA MABADILIKO NA UPATIKANAJI WA SEKTA YA NISHATI ZANZIBAR (ZESTA)....32

4.1.2 MRADI WA MSAADA WA SEKTA YA NISHATI ZANZIBAR - ZESS....34

4.2 OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO....37

4.2.1 MRADI WA MSAADA WA TAASISI KWA UHAMASISHAJI WA RASILIMALI ZA NDANI NA UTAWALA WA MALIASILI (ISP - DRMNRG)....37

4.2.2 MRADI WA UKUZAJI UCHUMI JUMUISHI ZANZIBAR - (BIG-Z)....40

4.3 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI....42

4.3.1 MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA SEKONDARI ZANZIBAR (ZISP)....42

4.3.2 MRADI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA WA ELIMU AWAMU YA PILI (GPE II)....46

4.3.3 MRADI WA ELIMU YA JUU KWA MABADILIKO YA KIUCHUMI (HEET)....49

4.3.4 MRADI WA UJENZI NA UWEZESHAJI WA SHULE ZA SEKONDARI (BADEA II)....50

4.4 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI....52

4.4.1 MRADI WA MAENDELEO YA KILIMO NA UVUVI (AFDP)....52

4.5 WIZARA YA AFYA....55

4.5.1 MFUKO WA FEDHA WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR (ZANZIBAR HEALTH BASKET FUND)................................55

4.5.2 PROGRAMU YA CHANJO – EPI (GAVI) .............................59

4.6 WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI ..................67

4.6.1 MRADI WA KUSAIDIA SEKTA YA UCHUKUZI -TSSP ...........67

4.6.2 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TANZANIA (TASAF) .....68

4.7 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI .............................73

4.7.1 MRADI WA USIMAMIZI WA UVUVI NA UKUAJI WA PAMOJA KUSINI MAGHARIBI MWA BAHARI YA HINDI (SWIOFish)..73

4.7.2 MRADI WA MPANGO WA CHAKULA KATIKA SKULI ZA MSINGI..................................................................74

**SURA YA TANO**............................................................................77

5.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA PEMBA..................................77

5.1 UTANGULIZI .................................................................................77

5.1.1 MRADI WA UJENZI WA SOKO LA SAMAKI NA MBOGAMBOGA MTAMBILE..................................................................77

5.1.2 MRADI WA BUSTANI YA MWANAMASHUNGI .....................85

5.1.3 MRADI WA SOKO LA MACHOMANNE ...............................92

5.1.4 MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA MABASI KINOWE ......97

5.1.5 MRADI WA UJENZI WA JENGO JIPYA LA BIASHARA NA MAKAAZI MKUNGU MALOFA CHAKE CHAKE PEMBA.........102

5.1.6 MRADI WA UKARABATI WA NYUMBA ZA MAENDELEO MTEMANI...................................................................109

**SURA YA SITA** ..............................................................................115

6.0 UKAGUZI WA UFANISI KUHUSIANA NA UNUNUZI WA GARI ZA KUBEBEA WAGONJWA NA USAMBAZAJI WA VIFAA TIBA HOSPITALI ..................................................................115

6.1 HISTORIA YA MRADI....115
6.2 MALENGO YA UKAGUZI....116
6.3 UPEO WA UKAGUZI....116
6.4 VIPENGELE VYA UPANGAJI NA USANIFU....117
6.4.1 VIPENGELE VYA MCHAKATO WA UNUNUZI NA UTOAJI WA MIKATABA....117
6.4.2 USIMAMIZI WA MUDA WA MKATABA, UBORA WA VIFAA, GHARAMA NA UPEO WA MRADI....117
6.5 VIGEZO VYA TATHMINI, MBINU NA SAMPULI ZILIZOTUMIKA....117
6.6 MBINU ZA UCHAMBUZI WA TAARIFA....120
6.7 USIMAMIZI WA MIFUMO YA UNUNUZI NA USAMBAZAJI WA VIFAA TIBA....120
6.7.1 SHERIA NA KANUNI ZA UNUNUZI NA UONDOSHAJI WA MALI ZA UMMA....120
6.7.2 KANUNI ZINAZOSIMAMIA UDHIBITI WA GHARAMA....121
6.7.3 MAJUKUMU NA WAJIBU WA WAHUSIKA WA MRADI....122
6.7.4 TARATIBU ZA KUSIMAMIA USAMBAZAJI WA VIFAA TIBA....123
6.7.5 UTENDAJI WA KIFEDHA....123
6.7.6 UTEKELEZAJI WA MRADI....123
6.7.7 MRADI WA UNUNUZI NA USAMBAZAJI WA GARI 12 ZA KUBEBEA WAGONJWA....146
6.7.8 UNUNUZI NA USAMBAZAJI WA GARI 5 ZA KUBEBEA DAWA....147
6.7.9 MRADI WA UNUNUZI NA USAMBAZAJI WA VIFAA VYA KUSAFISHIA DAMU....150
**SURA YA SABA**....156
7.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO....156
**VIAMBATISHO**....158

# ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli Nambari 1: Orodha ya Miradi iliyowasilishwa na kukaguliwa kwa mwaka 2022/2023.................................................. 2
Jadweli Nambari 2: Uwasilishaji wa hesabu za Miradi ya Maendeleo wa mwaka 2022/2023.................................................. 4
Jadweli Nambari 3: Miradi ambayo haikuwasilisha taarifa za ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ........................................................... 7
Jadweli Nambari 4: Utekelezaji wa Mapendekezo katika Taarifa za ukaguzi uliopita ....................................................14
Jadweli Nambari 5: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2022/2023............................................16
Jadweli Nambari 6: Utendaji Kifedha katika Akaunti ya Mradi wa ISP-DRMNRG ......................................................20
Jadweli Nambari 7: Utendaji Kifedha katika Akaunti ya Mradi wa BIG-Z .................................................................21
Jadweli Nambari 8: Mapokezi ya Fedha na Matumizi .............................22
Jadweli Nambari 9: Vyanzo na Matumizi ya Fedha za Mradi wa HEET .....23
Jadweli Nambari 10: Vyanzo vya fedha za mradi wa BADEA II ...............24
Jadweli Nambari 11: Utekelezaji wa Kifedha ........................................25
Jadweli Nambari 12: Utendaji wa Kifedha wa mradi ..............................26
Jadweli Nambari 13: Utendaji wa kifedha wa Mradi wa TASAF kwa Pemba PAA na Unguja PAA............................................27
Jadweli Nambari 14: Utendaji wa kifedha wa Mradi wa Mfuko wa Fedha wa Huduma za Afya Zanzibar ...............................28
Jadweli Nambari 15: Taarifa ya Matumizi ya Mradi ................................28
Jadweli Nambari 16: Utekelezaji wa mradi Kifedha................................29
Jadweli Nambari 17: Utendaji wa kifedha wa Mpango wa Chakula katika Skuli za Msingi ...................................................30
Jadweli Nambari 18: Fedha za mradi ambazo hazikutolewa ...................33

Jadweli Nambari 19: Ucheleweshaji wa mikataba kwa Mwanasheria Mkuu ....................34
Jadweli Nambari 20: Fedha za Mradi ambazo hazijalipwa na Washirika wa Maendeleo ....................35
Jadweli Nambari 21: Fedha ya mradi ambazo hazikutumika ....................39
Jadweli Nambari 22: Malipo yaliyofanyika bila ya stakabadhi za Kielekroniki ....................40
Jadweli Nambari 23: Shughuli ambazo hazikutekelezwa ....................42
Jadweli Nambari 24: Fedha za mradi ambazo hazikutumika ....................50
Jadweli Nambari 25: Matumizi kinyume na Bajeti ....................53
Jadweli Nambari 26: Ucheleweshaji wa shughuli za Manunuzi ....................54
Jadweli Nambari 27: Fedha zilizoingizwa na washirika wa maendeleo ....................56
Jadweli Nambari 28: Fedha iliyoingizwa kwenye akaunti za watekelezaji wa Mradi ....................56
Jadweli Nambari 29: Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye daftari la ghalani ....................58
Jadweli Nambari 30: Shughuli za mradi ambazo zimepangwa na kutengewa fedha lakini hazikutekelezwa ....................59
Jadweli Nambari 31: Chanjo zilizokwisha muda wake ambazo hazijateketezwa ....................61
Jadweli Nambari 32: Kiwango cha VAT kilichotozwa kwa miamala ya Kibenki kwa kila mwezi ....................62
Jadweli Nambari 33: Matumizi yaliyofanywa bila kuzingatia matumizi ya risiti za Kielektroniki ....................63
Jadweli Nambari 34: Ununuzi uliofanywa bila kutumia mfumo wa e-Proz ....................63
Jadweli Nambari 35: Orodha ya Chanjo ya Rotavac ya Wilaya ya Wete-Pemba kutoka Jan, 2023 hadi Juni, 2023 ....................65
Jadweli Nambari 36: Data ya Chanjo ya Rotavac ya Wilaya ya Chake Chake Januari hadi Juni, 2023 ....................66

Jadweli Nambari 37: Kuchelewa Kuwasilishwa kwa Rasimu ya Mkataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ......................68

Jadweli Nambari 38: Fedha zilizohamishwa bila ya kuwafikia walengwa...70

Jadweli Nambari 39: Fedha zisizokusanywa na kaya Unguja PAA............71

Jadweli Nambari 40: Pemba PAA Fedha zisizokusanywa ........................71

Jadweli Nambari 41: Kuchelewa kuhamisha mfuko wa Walengwa kwenda Unguja PAA.....................................................72

Jadweli Nambari 42: Kuchelewa kuhamisha mfuko wa Walengwa kwenda Pemba PAA ....................................................72

Jadweli Nambari 43: Malipo ya mradi yaliyofanywa kwa watu binafsi......75

Jadweli Nambari 44: Kazi ambazo hazijamalizika.................................90

Jadweli Nambari 45: Malipo ya ununuzi wa bidhaa ambazo hazina kibali cha mapokezi ..............................................103

Jadweli Nambari 46: Ununuzi wa bidhaa bila ya kutumia mfumo wa ununuzi wa Kielektroniki...................................104

Jadweli Nambari 47: Malipo ambayo hayakufuata utaratibu wa utoaji wa zabuni ........................................................105

Jadweli Nambari 48: Malipo yenye vielelezo pungufu ..........................106

Jadweli Nambari 49: Kodi ambazo hazikuwasilishwa Serikalini.............107

Jadweli Nambari 50: Malipo ambayo hayakutumia mfumo wa ununuzi wa Kielektroniki ..................................................110

Jadweli Nambari 51: Malipo ambayo hayakufuata utaratibu wa utoaji wa zabuni ........................................................111

Jadweli Nambari 52: Malipo yenye vielelezo pungufu ..........................112

Jadweli Nambari 53: Malipo ya kodi yaliyokosa vielelezo vya uwasilishaji ..................................................113

Jadweli Nambari 54: Mchanganuo wa Gharama, Msambazaji na Hospitali zilizohusika..................................................118

Jadweli Nambari 55: Nyaraka zilizopitiwa na Sababu za Mapitio ...........119

Jadweli Nambari 56: Sheria ya Udhibiti wa Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa Tiba ..................................................121

Jadweli Nambari 57: Kanuni zinazosimamia Ununuzi na Usambazji Vifaa Tiba....121
Jadweli Nambari 58: Utendaji wa Kifedha....123
Jadweli Nambari 59: Hali halisi ya utekelezaji wa Mradi....124
Jadweli Nambari 60: Miradi iliyokaguliwa....125
Jadweli Nambari 61: Asilimia ya Malipo ya Usambazaji wa Vifaa Tiba...128
Jadweli Nambari 62: Malipo ya Awali yaliyofanywa bila Hati ya Malipo ya Awali....130
Jadweli Nambari 63: Ulinganisho wa bei baada ya kujumuisha VAT kwa Bei inayotolewa na msambazaji bila kujumuisha VAT....134
Jadweli Nambari 64: Ulinganishi wa bei kwa Aliyepewa na mzabuni aliyetathminiwa vyema....135
Jadweli Nambari 65: Thamani ya vifaa vya matibabu ambavyo havitumiki kwa sababu ya kasoro....137
Jadweli Nambari 66: Hali ya uwasilishaji wa dhamana ya kazi....140
Jadweli Nambari 67: Hali ya Uwasilishaji wa Hati ya dhamana wa Utendaji....142
Jadweli Nambari 68: Hali ya Malipo ya Wazabuni kuhusiana na Kazi waliyofanya....144
Jadweli Nambari 69: Hali ya Kuongeza Muda....145
Jadweli Nambari 70: Taarifa za Mkataba wa ununuzi wa gari za kubebea wagonjwa....146
Jadweli Nambari 71: Taarifa ya Mkataba kwa gari 5 za kubebea dawa...148
Jadweli Nambari 72: Wazabuni waliowasilisha hati ya zabuni....148
Jadweli Nambari 73: Uwasilishwaji wa Zabuni za Ununuzi wa gari 5......149
Jadweli Nambari 74: Taarifa ya Mkataba wa vifaa vya kusafishia damu.150
Jadweli Nambari 75: Kutofanyika kwa Maandalizi ya kutosha ya vipimo vya vifaa Tiba....152

# ORODHA YA PICHA

Picha Nambari 1: Uwekaji wa Mita za AMR pasipokuwa na Ulinzi ...........36
Picha Nambari 2: Usimamizi usioridhisha wa Mradi ...............................48
Picha Nambari 3: Dosari za usimamizi katika Miradi ya Ujenzi ................51
Picha Nambari 4: Wadau wanaohusika katika Ununuzi na Usambazaji Vifaa Tiba ...........................................................122
Picha Nambari 5: Hali ya uchakavu wa gari za kubebea dawa..............139
Picha Nambari 6: Uchelewaji wa kufanyiwa services kwa mashine hiyo ndani ya kipindi cha uangalizi.................................153

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AfDB | Mfuko wa Benki ya Maendeleo ya Afrika |
| AFDP | Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi |
| AG | Mwanasheria Mkuu |
| APP | Mpango wa Ununuzi wa Mwaka |
| BADEA | Shirika la Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika |
| BIG-Z | Mradi wa Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar |
| BMGF | Mfuko wa Bill na Melinda Gates |
| BoQs | Gharama za Makisio ya Vifaa vya Ujenzi |
| COVID-19 | Ugonjwa wa Virusi vya Corona |
| DFID | Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Uingereza |
| FSDT | Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania |
| GCC | Masharti ya Jumla ya Mkataba |
| GN | Government Notice |
| GPE II | Mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa kwa Elimu |
| HEET | Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi |
| IDA | Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza |
| IMF | Shirika la Fedha la Kimataifa |
| INTOSAI | Jumuiya ya Kimataifa ya Taasisi Kuu za Ukaguzi Kwenye Sekta za Umma |
| IPCs | Cheti cha Malipo ya Muda wa Awali |
| IPSAS | Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu Katika Sekta ya Umma |
| ISP-DRMNRG | Mradi wa Msaada wa Kitaasisi wa Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani na Utawala wa Maliasili |
| ISSAIs | Viwango vya Kimataifa vya Taasisi za Juu za Ukaguzi |
| MoHZ | Wizara ya Afya Zanzibar |
| OCAGZ | Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar |
| OFID | Mfuko wa Maendeleo wa Kimataifa wa Umoja wa Nchi Zinazozalisha Mafuta |

| | |
|---|---|
| PPR | Kanuni za Ununuzi wa Umma |
| PSSN | Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini |
| SCC | Masharti Maalum ya Mkataba |
| SIDA | Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden |
| SWIOFish | Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi na Ukuaji wa Pamoja Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| Tsh/Shs/TZS | Shilingi ya Tanzania |
| TSSP | Mradi wa Kusaidia Sekta ya Uchukuzi |
| UN Agencies | Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa |
| UNICEF | Shirika la Umoja wa Mataifa Linalohudumia Watoto |
| USAID | Shirika la Misaada la Watu wa Marekani |
| USD | Dola ya Kimarekani |
| VAT | Kodi ya Ongezeko la Thamani |
| VO's | Maagizo ya Tofauti |
| WB | Benki ya Dunia |
| WEMA | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali |
| WHO | Shirika la Afya Duniani |
| ZBA | Wakala wa Ujenzi Zanzibar |
| ZECO | Shirika la Umeme Zanzibar |
| ZESS | Mradi wa Msaada wa Sekta ya Nishati Zanzibar |
| ZESTA | Mradi wa Mabadiliko na Upatikanaji wa Sekta ya Nishati Zanzibar |
| ZISP | Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari Zanzibar |
| ZPPDA | Mamlaka ya Ununuzi na Uendeshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| ZRA | Mamlaka ya Mapato Zanzibar |

## SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za mara kwa mara anazoendelea kuzichukuwa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo na kutoa maelekezo katika kufanya maboresho juu ya dosari mbali mbali zinazobainishwa katika Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na hatua anazoendelea kuzichukua kutokana na hoja za ukaguzi zinazoibuliwa kuhusu matumizi ya fedha pamoja na usimamizi wa rasilimali za Umma.

Vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, pamoja na watendaji mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano yao wanayokupatia katika utekelezaji wa majukumu yako ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kuwaletea maendeleo endelevu ya nchi yao.

Shukurani zangu za dhati ziende kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kujitolea kwa dhati kujadili na kutoa mapendekezo pamoja na kufuatilia hatua zinazochukuliwa na Serikali kutokana na dosari zilizojitokeza na kuibuliwa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya watendaji katika sekta mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuniunga mkono na kunipa nguvu katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kikatiba, pamoja na jitihada zake anazozichukuwa katika kusimamia misingi ya utawala bora na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji.

Vile vile nitoe shukurani zangu za dhati kwa Bodi ya Utumishi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kusimamia maadili na nidhamu ya wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya kazi za ukaguzi.

Kwa namna ya kipekee niwashukuru wafanyakazi wote wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Afisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Tanzania Audit Corporation (TAC Associates), Price Waterhouse Coopers (PWC), pamoja na Ernst & Young (EY) kwa kufanya kazi za ukaguzi kwa mashirikiano na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na juhudi zao mbali mbali walizozichukuwa hadi kukamilika kwa ripoti hii.

Mwisho, niwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbali mbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, nitakuwa mchache wa shukurani kama sitatambua jukumu la vyombo mbali mbali vya habari kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuutambulisha Umma juu ya kazi zinazofanywa na Afisi ya Mdhibiti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo matokeo na mapendekezo ya kazi hizo huwasilishwa kwa jamii kupitia vyombo mbali mbali vya habari.

Natumia fursa hii, kuwasihi wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuwa na moyo wa dhati katika kufanya kazi kwa bidii na kuongeza mashirikiano kwa ajili ya siku zijazo ili kuendelea kudumisha nidhamu ya Afisi ya Mdhibiti katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora.

# DIBAJI



Ninafuraha kubwa ya kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa Hesabu za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023. Wasilisho hilo ni kwa mujibu wa Kifungu cha 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria Nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kwa kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa Sheria mbali mbali zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na sheria mbali mbali zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutumiwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ni jukumu langu la kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na usimamizi wa fedha pamoja na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma na hatimae taarifa hizo kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa hatua za utekelezaji.

Ripoti hii inajumuisha mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa taasisi za Serikali kwenye tathmini na ukaguzi wa taarifa za fedha pamoja na nyaraka husika, mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu na mchakato wa manunuzi na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni mbali mbali. Kufuatia kukamilika kwa ukaguzi huo nimetoa hati za ukaguzi kwa kila taasisi kuhusiana na taarifa za fedha zilizoandaliwa kama zinaonesha hali halisi ya shughuli zilizofanywa kulingana na mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha.

Nilifanya ukaguzi huo kwa kuangalia mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu za ununuzi, utayarishaji wa taarifa za fedha na nyaraka zilizoambatishwa, kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizowekwa pamoja na kuzingatia Viwango kubalifu vya Kitaifa na Kimataifa vya Taasisi za Juu za Hesabu za Serikali (ISSAIs) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) ambazo zinahusu ukaguzi wa Sekta za Umma.

Nimetoa Hati za Ukaguzi kwa kuzingatia Taarifa za Fedha nilizozikagua na kuzitolea ripoti ya ukaguzi kwa kila taasisi ambayo ilikaguliwa. Aidha, nilitoa barua za ukaguzi "Management Letters" zinazoonesha dosari zilizobainika kwa kila Mradi uliokaguliwa na mapendekezo ya kutekeleza ili kuboresha na kuondoa dosari zilizobainika kwa lengo la kutokujirejea mara nyengine.

Ni matumaini yangu kwamba Baraza la Wawakilishi litaona taarifa zilizomo katika ripoti hii ni za umuhimu katika kuisimamia Serikali na kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha na usimamizi wa rasilimali za umma ili kuhakikisha kunakuwa na utoaji bora wa huduma kwa umma wa Wazanzibari ambao inawahudumia. Katika suala hili nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi katika siku zijazo.

Kwa mara nyengine tena nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukuwa katika kufuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kusimamia na kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha na usimamizi wa rasilimali za Umma hali inayopelekea kuimarika kwa utawala bora.

…………………………………………..

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**

**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**

# MUHTASARI

Ripoti hii imekusanya jumla ya sura saba (7) zenye kuelezea mambo mbali mbali yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kwenye Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ukaguzi uliofanyika umebaini uwepo wa dosari mbali mbali ambapo dosari hizo zimewasilishwa kwenye uongozi wa Taasisi zilizohusika na utekelezaji huo kwa njia ya hoja za ukaguzi na kutolewa mapendekezo kwa lengo la kuimarisha dosari hizo, baadhi ya dosari ziliweza kufanyiwa kazi na Maafisa Masuuli wakati wa kipindi cha ukaguzi na kutolewa majibu kwa wakaguzi ili kuweza kujiridhisha juu ya uhalali wa dosari hizo. Aidha baadhi ya dosari zilizobainika hazikuweza kupatiwa majibu wakati wa ukaguzi na kupelekea kuingizwa katika Ripoti hii. Mambo yaliyobainika yamefafanuliwa katika sura tofauti zilizomo katika ripoti hii kama ifuatavyo:-

**Sura ya Kwanza:** Sura hii inaelezea kwa kina taarifa za utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa ambapo jumla ya miradi 32 ilikaguliwa, kati ya miradi hiyo miradi 17 iliwasilisha taarifa za hesabu kwa mujibu wa matakwa ya kisheria na miradi 15 ilishindwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za hesabu jambo ambalo lilipelekea kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi.

Jumla ya sekta kumi (10) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilikaguliwa na kupewa Hati za Ukaguzi kutokana na utekelezaji wa miradi iliyotekelezwa na sekta hizo kwa kutumia fedha inayotokana na michango ya washirika wa maendeleo pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kimuhtasari miradi hiyo imetekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha ingawa ipo baadhi ya miradi imebainika kuwa na dosari kubwa za kiutendaji iliyopelekea kutokukamilika kwa wakati na baadhi yake kutumia gharama kubwa ikilinganishwa na mikataba ya awali ya gharama za utekelezaji wa miradi hiyo.

**Sura ya Pili:** Sura hii inaonesha muhtasari wa mapendekezo na hatua zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli katika mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa uongozi katika taarifa za ukaguzi uliyopita. Vile vile inaeleza hati za ukaguzi zilizotolewa katika miradi kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kwa upande wa hali ya utekelezaji wa mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo; Kati ya mapendekezo 62 yaliyotakiwa kutekelezwa kutoka katika taarifa 15 za ukaguzi wa miradi ya Maendeleo iliyowasilishwa na kukaguliwa kwa mwaka

wa fedha 2021/2022 mapendekezo 22 sawa na asilimia 35.5 yalitekelezwa, mapendekezo 8 sawa na asilimia 12.9 yanaendelea kutekelezwa, mapendekezo 22 sawa na asilimia 35.5 hayakutekelezwa, mapendekezo 10 sawa na asilimia 16.1 yamejirudia.

Aidha kwa upande wa hati za ukaguzi wa miradi iliyotekelezwa imebainika jumla ya hati 32 zimetolewa ambapo kati ya hati hizo, hati 17 ni Hati zinazoridhisha sawa na asilimia 53.13 na Hati 15 ni hati za Kushindwa Kutoa maoni sawa na asilimia 46.87. Hati hizo zimetolewa kwa Taasisi 12 zenye miradi iliyokaguliwa.

**Sura ya Tatu:** Sura hii inaelezea utekelezaji wa miradi na utendaji wa kifedha ambapo imefafanua kuhusu hali ya ufadhili wa miradi pamoja na matumizi ya fedha zilizoingizwa kwa kila mradi. Kwa ujumla, sura hii inatoa taarifa muhimu ambazo Serikali inaweza kutumia kufanya maamuzi sahihi kuhusu usimamizi wa kifedha, udhibiti wa ndani ili kuboresha utendaji wa kifedha, kukuza uwajibikaji na kuhakikisha kunakuwepo uwazi katika kuripoti masuala ya kifedha.

**Sura ya Nne:** Sura hii inaeleza dosari zilizobainika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa taasisi za umma ambapo imebainsha mapungufu yaliyojitokeza katika hatua za utekelezaji kwa kila mradi uliokaguliwa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Miongoni mwa dosari zilizobainika ni kutokuwasilishwa kwa rasimu za Mikataba katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu jambo ambalo limepelekea kujitokeza utekelezaji wa miradi chini ya kiwango, kutokukamilika kwa wakati kwa baadhi ya miradi, ongezeko la gharama zisizo za msingi zilizopelekea baadhi ya taasisi kushindwa kuendeleza mradi kama ilivyokusudiwa na hatimae kutokupatikanwa kwa tija iliyokusudiwa. Pamoja na dosari hizo imebainika uwepo wa baadhi ya miradi kutokuendana na gharama halisi ya fedha iliyotumika (value for money) na kusababisha hasara kwa Serikali.

**Sura ya Tano:** Sura hii inatoa maelezo kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa Pemba ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Bustani Mwanamashungi na Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga Machomanne iliyotekelezwa na Baraza la Manispaa Chake Chake pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga Mtambile uliotekelezwa na Baraza la Mji Mkoani.

Aidha, sura hii imetoa ufafanuzi wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi uliotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

**Sura ya Sita:** Sura hii inaelezea kuhusiana na miradi ya ununuzi wa gari za kubebea wagonjwa na usambazaji wa vifaa tiba hospitalini ambapo dosari mbali mbali zilibainishwa katika utekelezaji wa miradi hiyo. Miongoni mwa dosari hizo ni kutokuwepo kwa Meneja wa Mradi aliyeteuliwa kwa ajili ya kupokea Vifaa tiba jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa taarifa muhimu za mapokezi ya vifaa tiba vilivyowasilishwa katika hospitali mbali mbali.

**Sura ya Saba:** Sura hii inatoa hitimisho na mapendekezo juu ya masuala muhimu yaliyojitokeza katika ripoti ya ukaguzi ya mwaka wa fedha 2022/2023. Licha ya matokeo ya kina na mapendekezo ambayo tayari yameshawasilishwa katika ripoti hii, ni muhimu kwa mara nyingine tena kuikumbusha Serikali na Maafisa Masuuli kuhusu masuala muhimu na kupendekeza hatua za jumla za kuchukuliwa.

## Taarifa ya Ujumla ya Utekelezaji wa Miradi

Kwa kuzingatia uchambuzi wa taarifa za ukaguzi nilizozianisha katika ripoti ya mwaka 2022/2023, ninahitimisha kwa ujumla kuwa bado kuna mapungufu katika usimamizi wa miradi ya maendeleo. Changamoto kubwa imekuwa ni ugumu wa kutofanikiwa kwa wakati malengo yaliyopangwa katika miradi husika. Sababu kubwa zinazoleta changamoto kwenye utekelezaji wa miradi hii ni pamoja na mapungufu katika usimamizi wa fedha na bajeti, uzingatiaji wa taratibu za manunuzi, usimamizi wa mikataba, pamoja na masuala ya kiutawala.

Kufanya malipo pasipo viambatisho vya kutosha kunaonesha uwepo wa tatizo kubwa katika utunzaji wa kumbukumbu na taarifa za kihasibu kwenye miradi. Hali hii inaweza kupelekea ubadhirifu katika matumizi ya fedha za miradi au fedha hizo kutumika katika kazi ambazo hazihusiani na miradi. Hivyo, naishauri Serikali na watekelezaji wa miradi wahakikishe kwamba malipo yote yanayohusiana na miradi yanakuwa na viambatisho vya kutosha.

## Usimamizi na Udhibiti wa Fedha

Tatizo la kutoa fedha pungufu kwenye miradi limekuwa kubwa ambalo limepelekea kuchelewa kukamilika kwa miradi mingi iliyotekelezwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023. Kuchelewa kutolewa kwa bajeti kikamilifu kunaathiri miradi ambayo pia hupelekea Serikali kulipa fidia kwa Wakandarasi kutokana na kutolipwa kwa wakati. Hii hupelekea miradi kuwa kwenye hatari ya ongezeko la gharama.

Aidha, kuna maeneo mengine ya miradi ambayo yanahitaji kuangaliwa kwa umakini zaidi ili kuongeza uwajibikaji. Hii ni pamoja na kuhakikisha kwamba Serikali inatimiza wajibu wake wa kibajeti. Maafisa masuuli watekeleze wajibu wao kulingana na makubaliano ili kupunguza ucheleweshaji wa kutekeleza miradi pamoja na kupata ruhusa ya kutumia fedha kutoka kwa wafadhili.

Ni matarajio yangu kuwa maafisa masuuli wataongeza juhudi na kutimiza matakwa ya miradi. Serikali itaokoa fedha ambazo zingelipwa kama fidia kwa Wakandarasi kutokana na ucheleweshaji wa malipo.

## Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba

Ukaguzi umebaini uwepo wa mapungufu katika manunuzi na usimamizi wa mikataba yaliyotokana na watekelezaji wa miradi kutozingatia Sheria na Kanuni za manunuzi kama vile manunuzi ya bidhaa na huduma bila kushindanisha wazabuni pamoja na kufanyika kwa manunuzi pasipo ruhusa ya bodi za manunuzi.

Mapungufu kwenye manunuzi hupelekea matatizo kwenye utekelezaji wa miradi kutokana na ucheleweshaji wa manunuzi ya vifaa na huduma za miradi. Ukaguzi unaishauri Serikali kuhakikisha kuwa miradi inaanzishwa, inatekelezwa na inasimamiwa kwa usahihi ili thamani ya fedha ipatikane kwa Serikali na jamii.

## Mapendekezo ya Ujumla ya Utekelezaji wa Miradi

Katika ukaguzi wangu kwenye miradi ya Maendeleo nimetoa mapendekezo kadhaa kwa watekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuwawezesha kuongeza uwajibikaji katika rasilimali za umma ikiwemo:-

(a) Maafisa Masuuli wanaohusika na udhibiti wa fedha za umma na usimamizi wa miradi ya maendeleo wanashauriwa kuweka juhudi zaidi katika kuhakikisha kwamba mapendekezo ya ukaguzi yanashughulikiwa ipasavyo ili kuondoa uwezekano wa kujirudia kwa mapungufu hayo katika ukaguzi ujao.

(b) Uongozi na wasimamizi wa miradi ya maendeleo tunawashauri wawe na desturi ya kutembelea mara kwa mara maeneo ya utekelezaji wa miradi ili kupunguza uwezekano wa kutofikiwa kwa malengo ya mradi yaliyokusudiwa.

(c) Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo wanatakiwa kuhakikisha kwamba fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kwa wakati ili kutekeleza miradi iliyokusudiwa hatimae kuleta tija kwa jamii.

(d) Uongozi na wasimamizi wa miradi ya maendeleo wahakikishe wanafuata masharti ya mkataba wa maelewano (MoU), hasa katika ufuatiliaji wa mara kwa mara wa ukaguzi wa taarifa za hesabu na utendaji wa miradi ya maendeleo na mapitio ya taarifa za robo mwaka na tathmini ili kurekebisha makosa.

(e) Uongozi na wasimamizi wa miradi ya maendeleo unashauriwa kufanya manunuzi kwa watoa huduma ambao wanatoa stakabadhi za kielectroniki za Mamlaka ya Mapato (ZRA) kwa njia hii Wizara pamoja na watoa huduma kuhakikisha kwamba wanafuata Kanuni za kodi. Aidha, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha kuwa zuio la kodi linawasilishwa kwa Mamlaka ya Mapato (ZRA) ndani ya muda muafaka.

(f) Maafisa Masuuli, Bodi za Zabuni na Vitengo vya Manunuzi vinapaswa kuhakikisha kwamba manunuzi ya kazi za ujenzi, bidhaa na huduma yanazingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na Kanuni zake za 2020.

(g) Maafisa masuuli kuhakikisha wanafanya manunuzi na watoa huduma waliosajiliwa kisheria ili kuepusha kujitokeza kwa upotevu wa fedha za kodi ya zuio.

(h) Kuhakikisha upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi unafanyika kwa ufanisi na kuidhinishwa kwa usahihi kabla ya kuanza kwa miradi.

# SURA YA KWANZA



# 1.0 TAARIFA ZA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOKAGULIWA

Sura hii inaelezea kwa kina taarifa za utekelezaji wa miradi iliyokaguliwa ambapo jumla ya miradi 32 ilikaguliwa, kati ya miradi hiyo miradi 17 iliwasilisha taarifa za hesabu kwa mujibu wa matakwa ya kisheria na miradi 15 ilishindwa kuandaa na kuwasilisha taarifa za hesabu jambo ambalo lilipelekea kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi.

Jumla ya sekta kumi (10) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilikaguliwa na kupewa Hati za Ukaguzi kutokana na utekelezaji wa miradi iliyotekelezwa na sekta hizo kwa kutumia fedha inayotokana na michango ya washirika wa maendeleo pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kimuhtasari miradi hiyo imetekelezwa kwa kiwango cha kuridhisha ingawa ipo baadhi ya miradi imebainika kuwa na dosari kubwa za kiutendaji iliyopelekea kutokukamilika kwa wakati na baadhi yake kutumia gharama kubwa ikilinganishwa na mikataba ya awali ya gharama za utekelezaji wa miradi hiyo.

## 1.1 Utangulizi

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kutekeleza miradi ya Maendeleo na kimkakati kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa lengo la kuimarisha mageuzi ya kiuchumi ambapo mpango huu una lengo la kuiwezesha Nchi kutumia kikamilifu fursa zilizopo kwa kuongeza uwezo wa uzalishaji, kujenga uchumi shindani, na kuboresha maendeleo ya watu. Mpango huo unalenga kufikia malengo haya kwa kuboresha miundombinu, kuimarisha sera za biashara na uwekezaji pamoja na kurekebisha mifumo ya Elimu.

## 1.2 Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 iliwasilishiwa jumla ya miradi Thelathini na Mbili (32) ya Maendeleo iliyofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika wa Maendeleo na kukaguliwa kwa Wizara/Taasisi kumi (12) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyowasilishwa na kukaguliwa imefanywa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo Kitaifa na Kimataifa kwa lengo la kutoa picha halisi ya namna ya miradi mbali mbali ya Serikali inavyotekelezwa, ili kuhakikisha kwamba taratibu na Sheria kuhusu usimamizi katika utekelezaji wa miradi hiyo unatekelezwa kwa mujibu wa Sheria zilizopo pamoja na kuhakikisha kwamba fedha na rasilimali za umma zinatumika kama ilivyokusudiwa.

Miradi iliyowasilishwa na kukaguliwa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi MKuu wa Hesabu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 1: Orodha ya Miradi iliyowasilishwa na kukaguliwa kwa mwaka 2022/2023

| Namba | Jina la Mradi | Mfadhili wa Mradi |
|---|---|---|
| **Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali** | | |
| 1. | Mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa kwa Elimu GPE II | Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA) |
| 2. | Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari Zanzibar (ZISP) | Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) |
| 3. | Mradi wa BADEA II | Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika (BADEA) |
| 4. | Mpango wa Chakula Katika Skuli za Msingi | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shirika la Maendeleo la 'Table for Two International' (TFT) |
| **Chuo Kikuu Cha Taifa (SUZA)** | | |
| 5. | Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET). | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) |
| **Ofisi ya Rais Fedha na Mipango** | | |
| 6. | Mradi wa Msaada wa Kitaasisi wa Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani na Utawala wa Maliasili (ISP-DRMNRG) | Mfuko wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) |
| 7. | Mradi wa Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z) | Benki ya Dunia (WB) |
| **Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo** | | |
| 8. | Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (AFDP) | Shirika la Maendeleo la IFAD |
| **Wizara ya Afya** | | |
| 9. | Programu ya Chanjo – EPI (GAVI) | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Wahisani wa Maendeleo wakiwemo WHO, UNICEF |

| Namba | Jina la Mradi | Mfadhili wa Mradi |
|---|---|---|
| 10. | Mfuko wa fedha wa huduma ya Afya Zanzibar (Zanzibar Health Basket Fund) | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika wa Maendeleo kama vile HIPZ, DANIDA na UNICEF |
| **Wizara ya Maji, Nishati na Madini** | | |
| 11. | Mradi wa Mabadiliko na upatikanaji wa Sekta ya Nishati Zanzibar (ZESTA) | Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) na Clean Technology Fund |
| 12. | Mradi wa Msaada wa Sekta ya Nishati Zanzibar - ZESS. | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA) |
| **Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi** | | |
| 13. | Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi na Ukuaji wa Pamoja Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) | Benki ya Maendeleo ya Kimataifa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| **Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** | | |
| 14. | Mradi wa Kusaidia Sekta ya Uchukuzi -TSSP | Mfuko wa ADB |
| **Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais** | | |
| 15. | TASAF | Serikali ya Tanzania, Mashirika ya Maendeleo ikiwemo IDA, OFID, UN Agencies , USAID, DFID, SIDA, BMGF na FSDT. |
| **Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ** | | |
| 16. | Mradi wa Ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi – Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| 17. | Mradi wa Ujenzi wa Soko la Machomanne - Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba | |
| 18. | Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga – Baraza la Mji Mkoani | |
| 19. | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi – Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | |

## 1.3 Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 inazitaka Taasisi zote za Serikali zitayarishe na kuwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwaka, zinazojumuisha Mapato na matumizi ya Taasisi husika. Tunatoa pongezi kwa Taasisi zenye kusimamia Miradi ya Maendeleo kwa jitihada walizochukuwa za kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka kwa mujibu wa Sheria.

## 1.4 Miradi iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha 2022/23 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Zanzibar ilipokea jumla ya Hesabu Kumi na Saba (17) za miradi ya Maendeleo kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali, Miradi ambayo inachangiwa fedha zake na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika wa Maendeleo. Miradi ya maendeleo iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ni kama inavyooneka katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 2: Uwasilishaji wa hesabu za Miradi ya Maendeleo wa mwaka 2022/2023**

| Namba | Jina la Mradi | Tarehe ya Uwasilishaji |
|---|---|---|
| | **Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali** | |
| 1. | Mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa kwa Elimu GPE II | 29/02/2023 |
| 2. | Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari Zanzibar (ZISP) | 23/02/2023 |
| 3. | Mradi wa BADEA II | 29/09/2023 |
| 4. | Mpango wa Chakula Katika Skuli za Msingi | 29/09/2023 |
| | **Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA)** | |
| 5. | Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET). | 29/09/2023 |
| | **Ofisi ya Rais Fedha na Mipango** | |
| 6. | Mradi wa Msaada wa Kitaasisi wa Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani na Utawala wa Maliasili (ISP-DRMNRG) | 27/12/2023 |
| 7. | Mradi Wa Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z) | 29/09/2023 |
| | **Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali** | |
| 8. | Mradi wa Uendeshaji wa Takwimu Zanzibar (ZSDP) | Haikuwasilisha |
| | **Tume ya Mipango** | |
| 9. | Mradi wa Kuimarisha Rasilimali na Biashara ya Wanyonge Tanzania (MKURABITA) | Haikuwasilisha |
| | **Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo** | |
| 10. | Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (AFDP) | 30/09/2023 |
| 11. | Mradi wa Umwagiliaji Maji | Haikuwasilisha |
| 12. | Mradi wa Kudhibiti Upotevu wa Mazao. | Haikuwasilisha |
| | **Wizara ya Afya** | |
| 13. | Programu ya Chanjo – EPI (GAVI) | 20/09/2023 |
| 14. | Mfuko wa Fedha wa Huduma ya Afya Zanzibar (Zanzibar Health Basket Fund) | 28/11/2023 |
| 15. | Mradi wa Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa Tiba | 28/09/2023 |

| Namba | Jina la Mradi | Tarehe ya Uwasilishaji |
|---|---|---|
| 16. | Mradi wa Ununuzi na Usambazaji wa Gari za Kubebea Wagonjwa | 29/09/2029 |
| 17. | Mradi wa Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa vya Kusafishia Damu | 29/09/2023 |
| 18. | Mradi Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto | Haikuwasilisha |
| 19. | Mradi wa kutokomeza Malaria Zanzibar - Zanzibar (ZAMEP) | Haikuwasilisha |
| 20. | Mradi wa Kudhibiti VVU, Kifua Kikuu na Ukoma Zanzibar (ZIHTLP) | Haikuwasilisha |
| **Wizara ya Maji, Nishati na Madini** | | |
| 21. | Mradi wa Mabadiliko na upatikanaji wa Sekta ya Nishati Zanzibar (ZESTA) | 29/09/2023 |
| 22. | Mradi wa Msaada wa Sekta ya Nishati Zanzibar- ZESS. | 29/09/2023 |
| 23. | Mradi wa Uhuishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) | Haikuwasilisha |
| **Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi** | | |
| 24. | Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi na Ukuaji wa Pamoja Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) | 08/12/2023 |
| **Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** | | |
| 25. | Mradi wa Kusaidia Sekta ya Uchukuzi -TSSP | Haikuwasilisha |
| 26. | Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu | Haikuwasilisha |
| **Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais** | | |
| 27. | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) | 23/09/2023 |
| 28. | Mradi wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF III) | Haikuwasilisha |
| **Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ** | | |
| 29. | Mradi wa Ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi – Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba | Haikuwasilisha |
| 30. | Mradi wa Ujenzi wa Soko la Machomanne - Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba | Haikuwasilisha |
| 31. | Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga – Baraza la Mji Mkoani | Haikuwasilisha |
| 32. | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi – Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Haikuwasilisha |

## 1.5 Miradi ambayo haikuandaliwa Taarifa za fedha za mwisho wa mwaka (Financial Statement) kwa ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Zanzibar ikiwa inatekeleza Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP:2021-2026), Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2022/2023 ni muendelezo wa utekelezaji wa Program na Miradi ya Maendeleo.

Kwa mwaka wa fedha 2022/23 ukaguzi ulipitia taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo na kubaini uwepo wa Miradi ya Maendeleo ambayo taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka hazikuandaliwa na kuwasilishwa katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ukaguzi.

Aidha, ukaguzi umebaini taarifa za fedha kwa baadhi ya miradi hiyo zimeingizwa katika Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka za Taasisi/Wizara zilizowasilishwa kwa ukaguzi wakati taarifa hizo zilipaswa kuwasilishwa mbali 'Financial Statement' zake kutokana na taarifa za utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayofadhiliwa kwa fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kujumuishwa na fedha za Washirika wa Maendeleo (WD) katika utekelezaji wa miradi ya aina moja.

Orodha ya miradi ambayo hesabu zake hazikuandaliwa na kuwasilishwa kwa ukaguzi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 3: Miradi ambayo haikuwasilisha taarifa za ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa mwaka wa fedha 2022/2023

| Namba | Jina la Mradi | Kiasi cha fedha Kilichopangwa | | | Kiasi cha Fedha Kilichotoka Julai 2022 - Machi 2023 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mchango wa fedha kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar **(TZS "000")** | Mchango wa fedha kwa Wafadhili wa Maendeleo **(TZS "000")** | Jumla **(TZS "000")** | Mchango wa fedha kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar **(TZS "000")** | Mchango wa fedha kwa Wafadhili wa Maendeleo **(TZS "000")** | Jumla **(TZS "000")** |
| **Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo** | | | | | | | |
| 1. | Mradi wa Umwagiliaji Maji | 325,000 | 13,000,000 | 13,325,000 | 0 | 15,742,248 | 15,742,248 |
| 2. | Mradi wa Kudhibiti Upotevu wa Mazao. | 1,426,651 | 252,356 | 1,679,007 | 0 | 134,000 | 134,000 |
| **Wizara ya Afya** | | | | | | | |
| 3. | Mradi Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto | 986,432 | 1,115,386 | 2,101,818 | 387,691 | 2,115,445 | 2,503,136 |
| 4. | Mradi wa kutokomeza Malaria Zanzibar - Zanzibar (ZAMEP) | 333,679 | 2,224,574 | 2,558,253 | 0 | 1,438,820 | 1,438,820 |
| 5. | Mradi wa Kudhibiti VVU, Kifua Kikuu na Ukoma Zanzibar (ZIHTLP) | 61,287 | 3,213,805 | 3,275,092 | 639,747 | 5,673,911 | 6,313,658 |

| Namba | Jina la Mradi | Kiasi cha fedha Kilichopangwa | | | Kiasi cha Fedha Kilichotoka Julai 2022 - Machi 2023 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mchango wa fedha kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar **(TZS "000")** | Mchango wa fedha kwa Wafadhili wa Maendeleo **(TZS "000")** | Jumla **(TZS "000")** | Mchango wa fedha kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar **(TZS "000")** | Mchango wa fedha kwa Wafadhili wa Maendeleo **(TZS "000")** | Jumla **(TZS "000")** |
| **Tume ya Mipango** | | | | | | | |
| 6. | Mradi wa Kuimarisha Rasilimali na Biashara ya Wanyonge Tanzania (MKURABITA) | 2,600,000 | 325,000 | 2,925,000 | 0 | 307,113 | 307,113 |
| **Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi** | | | | | | | |
| 7. | Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu | 24,665,550 | 137,644,000 | 162,309,550 | 8,581,493 | 2,459,570 | 11,041,063 |
| **Wiazara ya Maji,Nishati na Madini** | | | | | | | |
| 8. | Mradi wa Uhuishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) | 2,275,000 | 43,456,125 | 45,731,125 | 2,500,000 | 32,567,316 | 35,067,316 |
| **Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali** | | | | | | | |
| 9. | Mradi wa Uendeshaji wa Takwimu Zanzibar (ZSDP) | 325,000 | 8,298,222 | 8,623,222 | 0 | 5,900,000 | 5,900,000 |
| **Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais,Sera,Uratibu na Baraza la Waakilishi** | | | | | | | |
| 10. | Mradi wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF III) | 65,000 | 9,518,882 | 9,583,882 | 25,000 | 5,652,798 | 5,677,798 |

## 1.6 Wajibu wa Maafisa Masuuli

Kifungu nambari 4 cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinawataka Maafisa Masuuli kuandaa taarifa za fedha kwa mujibu wa viwango vya uhasibu vinavyokubalika kwa ujumla (GAAP) ambazo zitajumuisha taarifa sahihi za fedha kwa kila mwaka wa fedha zinazoonesha mapato na matumizi ya miradi hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha husika.

Aidha, Maafisa Masuuli wahakikishe kwamba, kumbukumbu sahihi za kihasibu za miradi zinatunzwa vizuri pamoja na kuhakikisha mfumo thabiti wa udhibiti wa ndani katika Taasisi unakuwepo.

Zaidi ya hayo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuhakikisha uendeshaji wa miradi unazingatia masharti na makubaliano ya mradi husika kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, na sheria na kanuni zinazotumika.

## 1.7 Wajibu wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa Sheria mbali mbali zikiwemo Sheria za fedha, Sheria za manunuzi na Sheria nyenginezo.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112(3) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kufanya yafuatayo:-

"a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumzi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi. ”

Ukaguzi wa hesabu umefanywa kwa kuzingatia Miongozo na vigezo mbali mbali vya ukaguzi ili kukidhi matarajio ya wadau wetu na wananchi kwa ujumla. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi kwa kufanya ukaguzi utakaoleta tija na kuongeza wigo na maeneo yanayokaguliwa kwa lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta za umma.

## 1.8 Upeo na Viwango vya ukaguzi vinavyotumika

### 1.8.1 Upeo wa Ukaguzi

Upeo wa ukaguzi unahusisha tathmini ya ufanisi wa mfumo wa fedha wa kihasibu, udhibiti wa ndani juu ya shughuli mbalimbali, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kutembelea maeneo ya utekelezaji ili kujionea hali halisi ya utekelezaji huo.

Ukaguzi unafanyika ili kujiridhisha kwamba kulikuwepo na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni zilizopo, kuongeza tija na ufanisi na kupunguza gharama za uendeshaji katika matumizi ya umma pamoja na kuzingatia kwamba taarifa za fedha kwa ujumla wake hazina dosari kutokana na udanganyifu na zimeandaliwa kwa mujibu wa mfumo wa utoaji wa taarifa za kifedha. Wakati wa ukaguzi kasoro zinazojitokeza zinawasilishwa kwa Afisa Masuuli anayehusika na utekelezaji wa mradi kupitia kikao cha kumaliza ukaguzi (Exit meeting). Maafisa Masuuli wanapewa fursa ya kujibu hoja na kutekeleza mapendekezo na maoni ya ukaguzi. Baada ya hapo masuala yote ambayo hayakupata ufumbuzi/ufafanuzi yanajumuishwa kwenye taarifa ya mwisho kwa Afisa Masuuli na ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inayoonyesha hati ya ukaguzi kwa taasisi husika.

### 1.8.2 Viwango vya ukaguzi vilivyotumika

Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni mwanachama wa Jumuiya ya Kimataifa ya Taasisi Kuu za Ukaguzi wa Hesabu (INTOSAI) na Jumuiya ya Taasisi Kuu za Ukaguzi kwa Nchi za Afrika Zinazozungumza Kiingereza (AFROSAI-E).

Aidha, taratibu zilizotumika zimezingatia viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi kama vile ISSAI vinavyotolewa na INTOSAI na Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu na Wakaguzi (IFAC). Viwango hivi vinanitaka kuzingatia maadili katika kuandaa na kutekeleza ukaguzi wangu ili kupata uhakika kwamba taarifa za fedha ni sahihi na hazina makosa makubwa.

## 1.9 Mbinu za ukaguzi zilizotumika

Mbinu za ukaguzi zilizotumika pamoja na kutathmini kumbukumbu za uhasibu na taratibu zingine ili kukidhi malengo ya ukaguzi. Taratibu za ukaguzi zilijumuisha hatua zifuatazo;

a) Kupanga ukaguzi ili kutambua na kutathmini hatari za kuwa na taarifa zisizo sahihi, ama kutokana na udanganyifu au dosari; na kwa kuzingatia uelewa wa taasisi na mazingira yake, ikiwa ni pamoja na mifumo ya udhibiti wa ndani ya kila taasisi.

b) Kupata uthibitisho sahihi na toshelevu iwapo kuna taarifa zisizo sahihi kwa kusanifu na kutekeleza hatua stahiki dhidi ya viashiria vyote vya hatari vilivyoainishwa.

c) Kutembelea shughuli za miradi na kutathmini utendaji na utekelezaji wake.

d) Kutathmini ili kuona iwapo sheria, kanuni, na matakwa ya miradi yamezingatiwa kikamilifu.

e) Kutoa maoni juu ya taarifa za kifedha zilizokaguliwa kulingana na hitimisho linalotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana.

f) Kufuatilia utekelezaji wa matokeo ya ukaguzi wa mwaka uliopita na kuhakikisha kwamba hatua sahihi zimechukuliwa kuhusiana na masuala yote yaliyoainishwa.

# SURA YA PILI



# 2.0 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA UKAGUZI KWA MWAKA ULIOPITA NA HATI ZA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Sura hii inaonesha muhtasari wa mapendekezo na hatua zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli katika mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa uongozi katika taarifa za ukaguzi uliyopita.

Mapendekezo ya ukaguzi yanayotolewa yanakusudia kusaidia Watekelezaji wa miradi ya Maendeleo kurekebisha mapungufu ambayo yamebainika wakati wa ukaguzi na kupendekeza suluhisho husika kwa uboreshaji wa siku zijazo. Aidha, Hati za ukaguzi zilizotolewa na matokeo ya ukaguzi yanayohusiana na usimamizi wa fedha na udhibiti wa ndani katika miradi mbali iliyokaguliwa. Kwa ujumla, sura hii inatoa taarifa muhimu ambazo Serikali inaweza kutumia kufanya maamuzi sahihi kuhusu usimamizi wa kifedha, udhibiti wa ndani ili kuboresha utendaji wa kifedha, kukuza uwajibikaji na kuhakikisha kunakuwepo uwazi katika kuripoti masuala ya kifedha.

## 2.1 Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya ukaguzi uliopita

Kama inavyoonekana katika Jadweli la hapo chini, kati ya mapendekezo 62 yaliyotakiwa kutekelezwa kutoka katika taarifa 15 za ukaguzi wa miradi ya Maendeleo iliyowasilishwa na kukaguliwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 mapendekezo 22 sawa na asilimia 35.5 yalitekelezwa, mapendekezo 8 sawa na asilimia 12.9 yanaendelea kutekelezwa, mapendekezo 22 sawa na asilimia 35.5 hayakutekelezwa, mapendekezo 10 sawa na asilimia 16.1 yamejirudia.

Aidha, hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi hutolewa katika taarifa ya ukaguzi kwa kila Afisa Masuuli kwa hatua za utekelezaji.

**Jadweli Nambari 4: Utekelezaji wa Mapendekezo katika Taarifa za ukaguzi uliyopita**

| Maelezo | Mwaka wa fedha 2020/2021 | | Mwaka wa fedha 2021/2022 | |
|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Asilimia (%) | Jumla | Asilimia (%) |
| Mapendekezo yaliyotekelezwa | 63 | 52.5 | 22 | 35.5 |
| Mapendekezo yanayoendelea kutekelezwa | 21 | 17.5 | 8 | 12.9 |
| Mapendekezo yaliyojirudia | 22 | 18.3 | 10 | 16.1 |
| Mapendekezo ambayo hayakutekelezwa | 14 | 11.7 | 22 | 35.5 |
| **Jumla Kuu** | **120** | **100** | **62** | **100** |

*Chanzo: Taarifa za ukaguzi za mwaka 2022/23*

## 2.2 Hati za Ukaguzi

Hati ya ukaguzi inatolewa kwa kuzingatia tathmini ya hitimisho inayotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana, kama taarifa za fedha kwa ujumla wake zimeandaliwa kwa kuzingatia viwango vya taarifa za kifedha vinavyotumika (kama vile Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji Hesabu katika Sekta ya Umma IPSAS na Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Kifedha). Hati hiyo imetolewa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi kwenye Sekta za Umma (ISSAI 1200).

Katika kufanya ukaguzi wa fedha za miradi ya maendeleo, hati ya ukaguzi imetolewa kulingana na mifumo ya taarifa za fedha inayotumika katika utayarishaji wa taarifa za fedha za hesabu za mwisho wa mwaka. Maeneo haya yanajumuisha uhakiki wa taarifa za fedha, udhibiti wa ndani na kuzingatia utekelezaji wa sheria na kanuni.

### 2.2.1 Aina ya Hati za ukaguzi

- **Hati inayoridhisha**

Hati inayoridhisha hutolewa pale ambapo taarifa za fedha zilizowasilishwa hazikuwa na upotoshaji pia ziliandaliwa kwa kufuata mfumo ulioelekezwa, ikiwa ni pamoja na Sheria na Kanuni zinazokubalika.

### ❖ Hati yenye Shaka

Hati hii hutolewa wakati nimejiridhisha kuwa kuna makosa kwenye taarifa za Hesabu ya Mwisho wa Mwaka, ama moja moja au kwa ujumla wake. Hata hivyo, makosa yaliyobainika husababisha athari sehemu maalumu tu na si taarifa nzima ya fedha.

### ❖ Hati Mbaya

Hati hii hutolewa pale ambapo nimejiridhisha kuwa, kulingana na ushahidi uliopatikana wakati wa ukaguzi, taarifa za fedha zilizokaguliwa zina makosa makubwa na yaliyoathiri sehemu kubwa ya taarifa za fedha hivyo kusababisha taarifa hizo kutokuwa sahihi.

Hii inamaanisha kuwa tofauti na hati yenye shaka, taarifa za fedha zilizoandaliwa zina makosa makubwa yatokanayo na kutokukubaliana au kushindwa kukidhi mawanda ya ukaguzi na makosa hayo hayajajikita sehemu moja bali yameathiri maeneo mengi katika taarifa za fedha na hivyo kuathiri kueleweka kwa taarifa hizo kwa watumiaji wake kwa ajili ya kufanyia maamuzi.

### ❖ Kushindwa kutoa Maoni

Mazingira ya ukaguzi yanaweza kusababisha kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi. Hii inatokea pale ambapo nimeshindwa kupata ushahidi wa kutosha au taarifa muhimu ili kufikia malengo ya ukaguzi, na endapo madhara ya kushindwa kupata ushahidi au nyaraka hizo ni makubwa sana.

Kama ilivyo kwa hati mbaya, ukaguzi unaposhindwa kutoa maoni, maana yake ni kuwa sehemu kubwa ya kiasi kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha hakiaminiki hivyo taarifa za fedha zilizokaguliwa hazifai kwa ajili ya kufanyia maamuzi mbalimbali.

## 2.3 Msingi wa Hati za Ukaguzi

Ili kufikia kwenye hati zilizotolewa, ukaguzi ulizingatia hali halisi ya matokeo ya ukaguzi kwa kila Mradi uliokaguliwa. Ukaguzi huo ulifanyika kulingana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi (ISSAIs). Viwango hivyo vinanitaka kuandaa mpango wa ukaguzi, kufanya ukaguzi, na kutoa ripoti ya matokeo ya ukaguzi huo.

Pia, vinanitaka kufuata maadili ya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa ukaguzi uliofanyika una ubora unaokubalika kwa hali ya juu.

Ukaguzi ulijumuisha uchunguzi wa nyaraka mbalimbali zinazohusiana na kiasi cha fedha kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha. Pia, ulijumuisha tathmini ya makadirio na maamuzi yaliyofanywa na uongozi wa Taasisi wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha za Miradi iliyotekelezwa, utoshelezi wa mambo yaliyoripotiwa kwenye taarifa za fedha, iwapo sera za uhasibu zinazotumika zinaendana na hali halisi ya utekelezaji wa Miradi hiyo inayokaguliwa na kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu.

## 2.4 Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, nilikamilisha ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo **32** ambapo miradi hiyo imetekelezwa katika Taasisi **12** za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kutoa hati za ukaguzi kwa Miradi **32**. Kati ya hati hizo, hati **17** ni hati zinazoridhisha sawa na asilimia **53.13** ya hati zilizotolewa, na hati **15** ni hati za Kushindwa Kutoa Maoni sawa na asilimia **46.87** ya hati zilizotolewa. Mchanganuo wa mwenendo wa hati hizo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 5: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

| Namba | Jina la Mradi | Hati za ukaguzi |
|---|---|---|
| **Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali** | | |
| 1. | Mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa kwa Elimu GPE II | Hati inayoridhisha |
| 2. | Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari Zanzibar (ZISP) | Hati inayoridhisha |
| 3. | Mradi wa BADEA II | Hati inayoridhisha |
| 4. | Mpango wa Chakula katika Skuli za Msingi | Hati inayoridhisha |
| **Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA)** | | |
| 5. | Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET). | Hati inayoridhisha |
| **Ofisi ya Rais Fedha na Mipango** | | |
| 6. | Mradi wa Msaada wa Kitaasisi wa Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani na Utawala wa Maliasili (ISP-DRMNRG) | Hati inayoridhisha |
| 7. | Mradi Wa Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z) | Hati inayoridhisha |

| Namba | Jina la Mradi | Hati za ukaguzi |
|---|---|---|
| **Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali** | | |
| 8. | Mradi wa Uendeshaji wa Takwimu Zanzibar (ZSDP) | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| **Tume ya Mipango** | | |
| 9. | Mradi wa Kuimarisha Rasilimali na Biashara ya Wanyonge Tanzania (MKURABITA) | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| **Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo** | | |
| 10. | Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (AFDP) | Hati inayoridhisha |
| 11. | Mradi wa Umwagiliaji Maji | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| 12. | Mradi wa Kudhibiti Upotevu wa Mazao. | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| **Wizara ya Afya** | | |
| 13. | Programu ya Chanjo – EPI (GAVI) | Hati inayoridhisha |
| 14. | Mfuko wa fedha wa Huduma ya Afya Zanzibar (Zanzibar Health Basket Fund) | Hati inayoridhisha |
| 15. | Mradi wa Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa Tiba | Hati inayoridhisha |
| 16. | Mradi wa Ununuzi na Usambazaji wa Gari za Kubebea Wagonjwa | Hati inayoridhisha |
| 17. | Mradi wa Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa vya Kusafishia Damu | Hati inayoridhisha |
| 18. | Mradi Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| 19. | Mradi wa kutokomeza Malaria Zanzibar - Zanzibar (ZAMEP) | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| 20. | Mradi wa Kudhibiti VVU, Kifua Kikuu na Ukoma Zanzibar (ZIHTLP) | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| **Wizara ya Maji, Nishati na Madini** | | |
| 21. | Mradi wa Mabadiliko na upatikanaji wa Sekta ya Nishati Zanzibar (ZESTA) | Hati inayoridhisha |
| 22. | Mradi wa Msaada wa Sekta ya Nishati Zanzibar- ZESS. | Hati inayoridhisha |

| Namba | Jina la Mradi | Hati za ukaguzi |
|---|---|---|
| 23. | Mradi wa Uhuishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar (INDIA) | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| **Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi** | | |
| 24. | Mradi wa Usimamizi wa Uvuvi na Ukuaji wa Pamoja Kusini Magharibi mwa Bahari ya Hindi (SWIOFish) | Hati inayoridhisha |
| **Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi** | | |
| 25. | Mradi wa Kusaidia Sekta ya Uchukuzi -TSSP | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| 26. | Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| **Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais** | | |
| 27. | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) | Hati inayoridhisha |
| 28. | Mradi wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF III) | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| **Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ** | | |
| 29. | Mradi wa Ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi – Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| 30. | Mradi wa Ujenzi wa Soko la Machomanne - Baraza la Manispaa Chake Chake Pemba | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| 31. | Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga – Baraza la Mji Mkoani | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |
| 32. | Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi – Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | **Hati ya Kushindwa Kutoa Maoni** |

# SURA YA TATU



# 3.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI NA UTENDAJI WA KIFEDHA

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea utekelezaji wa miradi na utendaji wa kifedha ambapo imefafanua kuhusu hali ya ufadhili wa miradi pamoja na matumizi ya fedha zilizoingizwa kwa kila mradi. Kwa ujumla, sura hii inatoa taarifa muhimu ambazo Serikali inaweza kutumia kufanya maamuzi sahihi kuhusu usimamizi wa kifedha, udhibiti wa ndani ili kuboresha utendaji wa kifedha, kukuza uwajibikaji na kuhakikisha kunakuwepo uwazi katika kuripoti masuala ya kifedha.

### 3.1.1 MRADI WA ISP - DRMNRG

**Utendaji wa kifedha**

Katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ikishirikiana na washirika wa maendeleo iliwezesha kupatikana kwa kiasi cha USD 644,663.29 hata hivyo kulikuwa na bakaa ya kiasi cha USD 29,568.82 katika akaunti ya Mradi wa ISP-DRMNRG hivyo kufanya jumla ya USD 674,232.11 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo.

Mradi wa ISP-DRMNRG kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ulifanya matumizi jumla ya USD 632,815.24, kati ya fedha hizo jumla ya USD 29,568.82 zililipwa kama ahadi za Mwaka wa Fedha uliopita 2021/2022 na USD 603,246.42 zilikuwa ni malipo halisi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, hivyo kubaki na bakaa ya USD 41,416.87 ilipofikia tarehe 30 Juni, 2023 kama ilivyoanishwa katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 6: Utendaji Kifedha katika Akaunti ya Mradi wa ISP-DRMNRG**

| Maelezo | Kiasi cha fedha (USD) |
|---|---|
| Salio la ufunguzi tarehe 1 Julai, 2023 | 29,568.82 |
| **Ongeza**: Mfuko wa Benki ya Maendeleo ya Afrika | 630,121.24 |
| : Mchango wa Serikali ya SMZ | 14,542.05 |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | **674,232.11** |
| **Toa**:Malipo ya Moja kwa Moja yanayofanywa na AfDB | 603,246.42 |
| :Malipo Mengine | 29,568.82 |
| **Salio lililobakia hadi tarehe 30 Juni, 2023** | **41,416.87** |

### 3.1.2 MRADI WA UKUZAJI UCHUMI JUMUISHI ZANZIBAR - (BIG-Z)

#### Utendaji wa kifedha

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Mradi wa BIG-Z ulipokea jumla ya USD 8,651,091.3 ambapo kiasi hiki kilijumuisha bakaa ya USD 3,701,193.08 ya mwaka uliyopita pamoja na mapokezi ya USD 4,949,061.63 kutoka Benki ya Dunia kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Hadi kufikia tarehe 30/06/2023 kulikuwa na salio la USD 7,886,055.55 hii inamaanisha USD 765,035.79 zilitumika katika utekelezaji wa shughuli za miradi kama ilivyoanishwa katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 7: Utendaji Kifedha katika Akaunti ya Mradi wa BIG-Z**

| Maelezo | Kiasi cha fedha (USD) |
|---|---|
| Salio anzia 1 Julai, 2023 | 3,701,193.08 |
| **Kiasi cha fedha kilichopokelewa:** | |
| : Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) | 4,949,061.63 |
| : Mapato Mengineo | 836.63 |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | **8,651,091.3** |
| Toa : Kiasi cha fedha iliyotumika | 765,035.79 |
| **Bakaa ya 30 Juni, 2023** | **7,886,055.55** |

### 3.1.3 MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA SEKONDARI ZANZIBAR (ZISP)

#### Matumizi ya Fedha za Mradi wa ZISP

Tathmini ya taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za mradi wa ZISP katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 inaonyesha kuwa Mradi ulikadiriwa kutumia jumla ya USD 35,000,000 kutoka Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (IDA) kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Mradi.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mradi wa ZISP ulifanya matumizi ya USD 32,960,127 na kupelekea uwepo wa salio la bakaa la mwisho wa mwaka la USD 2,039,873 kama ilivyoonyeshwa katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 8 : Mapokezi ya Fedha na Matumizi

| Namba | Maelezo | Fedha zilizotumika (USD) | Fedha zilizopatikana (USD) |
|---|---|---|---|
| 1. | Fedha zilizopatikana | | **35,000,000** |
| | **Vifungu vya matumizi** | | |
| 2. | Ufanisi wa Hisabati, Sayansi na Kiingereza | 5,011,193.11 | |
| 3. | Uboreshaji wa mazingira ya shule na mazingira ya kujifunza | 7,247,686.29 | |
| 4. | Vituo kwa ajili ya Kuimarishwa Hisabati, Sayansi na Kujifunza Kiingereza | 17,833,482.61 | |
| 5. | Mabadiliko ya Mifumo na Usimamizi wa Mradi | 2,535,782.42 | |
| 6. | Jukwaa la Mpango wa itiko la UVIKO- 19 (COVID-19). | 331,982.14 | |
| **Fedha zilizotumika kwa mwaka** | | **32,960,126.57** | **32,960,126.57** |
| **Salio tarehe 30/6/2023** | | | **2,039,873.43** |

## 3.1.4 MRADI WA ELIMU YA JUU KWA MABADILIKO YA KIUCHUMI (HEET)

### Matumizi ya Fedha za Mradi wa HEET

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi ulikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 7,171,630,333 ambapo mradi uliweza kupokea jumla ya Shilingi 3,870,897,961 sawa na asilimia 53.98 ya fedha iliyopangwa.

Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mradi ulitumia jumla ya shilingi 730,412,273.24 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mradi na kupelekea uwepo wa bakaa la shilingi 3,140,485,688 sawa na asilimia 81.13 ya fedha iliyopokelewa. Mchanganuo wa matumizi ni kama unavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 9:Vyanzo na Matumizi ya Fedha za Mradi wa HEET

| Namba | Maelezo | Fedha zilizotumika (Tsh.) | Fedha zilizopatikana (Tsh.) |
|---|---|---|---|
| 1. | **Fedha zilizopatikana** | | 3,870,897,961 |
| 2. | **Vifungu vya matumizi** | | |
| 3. | Kukuza mtaala na kuanzisha mbinu bunifu za ufundishaji | 103,734,417.23 | |
| 4. | Kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kidijitali | 40,484,987.58 | |
| 5. | Kuwajengea uwezo wa kitaalamu wafanyakazi pamoja na uongozi wa Chuo Kikuu | 586,192,868.43 | |
| **Fedha zilizotumika kwa mwaka** | | **730,412,273.24** | **730,412,273.24** |
| **Salio tarehe 30/6/2023** | | | **3,140,485,687.76** |

### 3.1.5 MRADI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA WA ELIMU AWAMU YA PILI (GPE II)

#### Vyanzo vya fedha za mradi

Mradi huu unafadhiliwa na "Global Partnership for Education" ambapo Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (SIDA) lilitoa jumla ya USD 2,249,990 kwa Mradi wa GPE, kukiwa na salio la anzia la jumla ya USD 211 na kufanya jumla ya USD 2,250,201. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 mradi ulitoa jumla ya USD 2,000,000 na kufikia jumla ya USD 4,550,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi.

Aidha, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 mradi ulitoa jumla ya USD 3,000,000 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi na kufikia jumla ya USD 7,550,000. Katika mwaka 2022/2023 Mradi haukuingiziwa fedha hivyo zilitumika fedha hizo kwa ajili ya kukamilisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizopangwa.

### 3.1.6 MRADI WA UJENZI NA UWEZESHAJI WA SHULE ZA SEKONDARI (BADEA II)

#### Vyanzo vya fedha za mradi

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Mradi wa BADEA II ilikadiriwa kupata mkopo wa jumla ya USD 13,500,000 kwa kipindi cha miaka mitatu ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikubali kuchangia jumla ya USD 1,500,000 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa ujenzi wa Skuli na ununuzi wa vifaa. Mchanganuo wa fedha kwa mujibu wa vipengele vilivyopangwa ni kama ifuatavyo:-

### Jadweli Nambari 10: Vyanzo vya fedha za mradi wa BADEA II

| Namba | Vipengele | Fedha zilizopatikana (USD) |
|---|---|---|
| 1. | Kazi za ujenzi | 8,784,000 |
| 2. | Ununuzi wa Mabasi na Samani za Skuli | 1,758,000 |
| 3. | Huduma za Ushauri | 900,000 |
| 4. | Posho kwa watekelezaji wa Mradi | 180,000 |
| 5. | Warsha ya uzinduzi wa Mradi | 50,000 |
| 6. | Ukaguzi wa Mradi | 50,000 |
| 7. | Fedha zisizotengewa fungu | 1,778,000 |
| **Jumla** | | **13,500,000** |

**Utendaji wa Kifedha**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mradi wa BADEA II ulipokea jumla ya shilingi 267,960,100 kutoka Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika (BADEA).

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mradi wa BADEA II ulitumia jumla ya shilingi 261,403,758 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi na kupelekea uwepo wa bakaa la shilingi 6,556,342.

## 3.2 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

### 3.2.1 MRADI WA USIMAMIZI WA UVUVI NA UKUAJI WA PAMOJA KUSINI MAGHARIBI MWA BAHARI YA HINDI (SWIOFish)

**Utekelezaji Kifedha**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi wa SWIOFish ulipokea jumla ya USD 1,217,029.19, ukijumuisha na Salio anzia la USD 657,344.40 na USD 559,684.79 kutoka Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mradi.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mradi wa SWIOFish ulifanya matumizi ya USD 1,222,885.13 na kupelekea uwepo wa ziada ya matumizi ya USD 5,855.94. Hali halisi ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 11: Utekelezaji wa Kifedha

| Maelezo | Kiasi cha Fedha (USD) |
|---|---|
| Salio anzia 1 Julai, 2022 | 657,344.40 |
| **Kiasi cha fedha kilichopokelewa:** | |
| Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) | 559,684.79 |
| **Jumla ya Fedha iliyopatikana** | **1,217,029.19** |
| Toa : Kiasi cha fedha iliyotumika | 1,222,885.13 |
| **Ziada ya fedha 30 Juni, 2023** | **(5,855.94)** |

## 3.2.2 MRADI WA MAENDELEO YA KILIMO NA UVUVI (AFDP)

### Utendaji wa Kifedha

Mradi wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi (AFDP) ulikadiriwa kupokea jumla ya shilingi 2,697,946,345 kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 kutoka Shirika la Maendeleo la IFAD ambapo kwa kipindi hicho Mradi ulipokea jumla ya shilingi 1,251,821,969 sawa na asilimia 46.4 ya fedha iliyokadiriwa.

Katika kutekeleza shughuli za Mradi za mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi ulitumia jumla ya shilingi 479,675,918 sawa na asilimia 17.8, kiasi hicho kinajumuisha fedha iliyotumika ya shilingi 359,421,837.20 na bakaa ya masurufu ya shilingi 120,254,080.80 ambayo hayakurejeshwa katika kipindi cha mwaka 2021/2022 na kubakiwa na bakaa ya shilingi 772,146,051 hadi kufikia tarehe 30/6/2023.

## 3.2.3 MRADI WA MABADILIKO NA UPATIKANAJI WA SEKTA YA NISHATI ZANZIBAR (ZESTA)

### Vyanzo vya fedha vya Mradi

Mradi wa Mabadiliko na Upatikanaji wa Sekta ya Nishati Zanzibar (ZESTA) umepokea jumla ya USD 752,091.10 kutoka Benki ya Dunia Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mradi ulitumia jumla ya USD 521,191.88 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi na kupelekea uwepo bakaa la USD 230,899.22.

## 3.2.4 MRADI WA MSAADA WA SEKTA YA NISHATI ZANZIBAR - ZESS

### Utendaji wa kifedha

Katika kipindi cha mwaka 2022/2023 Mradi wa Msaada wa Sekta ya Nishati Zanzibar - ZESS ulipokea na kutumia jumla ya USD 418,111.2 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi wa ununuzi wa mita 130 za AMR, matumizi hayo ilikuwa kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 12: Utendaji wa Kifedha wa mradi

| Tarehe | Maelezo | Kiasi cha Fedha (USD) |
|---|---|---|
| Novemba, 2021 | Malipo ya awamu ya mwanzo kwa Hexing Electrical Co. Limited | 92,913.60 |
| Aprili, 2022 | Malipo ya awamu ya Pili kwa Hexing Electrical Co. Limited | 325,197.60 |
| **Jumla** | | **418,111.2** |

### 3.2.5 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TANZANIA (TASAF)

#### Utendaji wa Kifedha

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi wa TASAF kwa Unguja PAA ulikuwa na jumla ya shilingi 5,371,699,443.78, fedha hizo zilijumuisha salio anzia la shilingi 284,133,677.97 na shilingi 5,087,565,765.81 kutoka kwenye Mfuko wa TASAF kwa ajili ya kutekeleza shughuli zilizoidhinishwa kwa upande wa Unguja.

Aidha, kwa Pemba PAA mradi wa TASAF ulikuwa na jumla ya shilingi 6,499,686,845 fedha hizo zilijumuisha salio anzia la shilingi 151,868,405 na shilingi 6,347,818,440 kutoka kwenye Mfuko wa TASAF kwa ajili ya kutekeleza shughuli ziliyoidhinishwa kwa upande wa Pemba.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 mradi wa TASAF kwa Unguja PAA ulitumia jumla ya shilingi 4,497,881,220.95 sawa na asilimia 84 na kupelekea uwepo wa bakaa ya shilingi 873,818,222.83 sawa na asilimia 16.

Aidha, kwa Pemba PAA mradi wa TASAF ulitumia jumla ya shilingi 6,499,349,046 sawa na asilimia 99.99 na kupelekea uwepo wa bakaa ya shilingi 337,799 sawa na asilimia 0.01 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 kama inavyoonekana kwenye jadweli la hapo chini:-

### Jadweli Nambari 13: Utendaji wa kifedha wa Mradi wa TASAF kwa Pemba PAA na Unguja PAA

| Maelezo | Utendaji wa Kifedha wa Pemba PAA (Tshs) | Utendaji wa Kifedha wa Unguja PAA (Tshs) |
|---|---|---|
| Salio anzia 1/7/2022 | 151,868,405 | 284,133,677.97 |
| **Jumlisha:** Fedha iliyopokewa | 6,347,818,440 | 5,087,565,765.81 |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | **6,499,686,845** | **5,371,699,443.78** |
| **Toa:** Fedha iliyotumika | 6,499,349,046 | 4,497,881,220.95 |
| **Bakaa ya 30/06/2023** | **337,799** | **873,818,222.83** |

*Chanzo: Ripoti ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2022/2023*

## 3.2.6 MFUKO WA FEDHA WA HUDUMA YA AFYA ZANZIBAR (ZANZIBAR HEALTH BASKET FUND)

### Utendaji wa Kifedha

Mfuko wa fedha wa huduma ya Afya Zanzibar unafadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, HIPZ, DANIDA na UNICEF. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya shilingi 1,042,300,000 zilikadiriwa.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mfuko wa fedha wa huduma ya Afya Zanzibar ulipokea jumla ya shilingi 242,300,000 kutoka kwa washirika wa maendeleo ambazo ni sawa na asilimia 23.25 ya makadirio.

Aidha, Mradi ulikuwa na salio la kuanzia shilingi 1,918,335,750 na kufanya jumla ya fedha zilizokuwepo kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kuwa jumla ya shilingi 2,160,635,750. Hali halisi ya Mchanganuo wa fedha ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 14: Utendaji wa kifedha wa Mradi wa Mfuko wa Fedha wa Huduma za Afya Zanzibar

| Maelezo | Kiasi cha Fedha (Tshs) | |
|---|---|---|
| Salio anzia 1/7/2022 | | 1,918,335,750 |
| **Jumlisha:** Fedha iliyopokewa | | |
| Shirika la Maendeleo la UNICEF | 232,300,000 | |
| Shirika la Maendeleo la HIPZ | 10,000,000 | **242,300,000** |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | | 2,160,635,750 |
| **Toa:** Fedha iliyotumika | | 2,002,661,040 |
| **Bakaa ya 30/06/2023** | | **157,974,710** |

## 3.2.7 PROGRAMU YA CHANJO – EPI (GAVI)

### Utendaji wa Kifedha

Programu ya Chanjo – EPI (GAVI) ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 2,322,425,276.49 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mradi ulitumia jumla ya shilingi 1,081,001,167.53 kwa ajili ya utekelezaji wa programu na kupelekea uwepo wa bakaa ya shilingi 1,241,424,108.96. Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo ni kama inavyoonekana kwenye jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 15: Taarifa ya Matumizi ya Mradi

| Maelezo | Makadirio (Shs) | Matumizi Halisi (Shs) | Bakaa (Shs) |
|---|---|---|---|
| Usafiri | 22,640,000 | 2,900,000 | 19,740,000 |
| Posho za Safari | 1,054,628,053.69 | 325,288,760 | 729,339,293.69 |
| Mikutano | 87,688,562.86 | 18,821,913.15 | 68,866,649.71 |
| Mafuta | 77,358,734 | 18,000,000 | 59,358,734 |
| Gharama za Uendeshaji | 322,307,400 | 21,113,598.25 | 301,193,801.75 |
| Malipo ya chanjo ya Polio | 757,802,525.94 | 694,876,896.13 | 62,925,629.81 |
| **Jumla** | **2,322,425,276** | **1,081,001,168** | **1,241,424,109** |

### 3.2.8 MRADI WA KUSAIDIA SEKTA YA UCHUKUZI -TSSP

#### Utekelezaji wa Mradi Kifedha

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 Mradi wa Kusaidia Sekta ya Uchukuzi - TSSP ulikuwa na jumla ya shilingi 7,059,927,871.1 ukijumuisha bakaa la shilingi 7,627,758.05 na shilingi 7,052,300,113.05 kutoka Mfuko wa ADB.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mradi wa Kusaidia Sekta ya Uchukuzi - TSSP ulifanya matumizi ya shilingi 6,903,889,709 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo na kupelekea uwepo ya bakaa la shilingi 156,038,161.45 kama ilivyoanishwa katika Jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 16: Utekelezaji wa mradi Kifedha**

| Maelezo | Kiasi Cha Fedha (Tshs) |
|---|---:|
| Salio anzia 1 Julai, 2023 | 7,627,758.05 |
| **Kiasi cha fedha kilichopokelewa:** | |
| Shirika la Maendeleo la Kimataifa (ADB) | 7,052,300,113.05 |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | **7,059,927,871.1** |
| **Toa**: Kiasi cha fedha iliyotumika | 6,903,889,709 |
| **Bakaa ya 30 Juni, 2023** | **156,038,161.45** |

### 3.2.9 MRADI WA MPANGO WA CHAKULA KATIKA SKULI ZA MSINGI

#### Utendaji wa Kifedha

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Mradi ulikuwa na jumla ya USD 228,708.41, fedha hizo zilijumuisha salio anzia la USD 195,149.59 na USD 4,765.01 kutoka Shirika la 'Table for Two International' (TFT) na USD 28,793.72 ni mchango kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kutekeleza shughuli ziliyoidhinishwa na mradi.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 mradi ulitumia jumla ya USD 193,701.59 sawa na asilimia 85 na kupelekea uwepo wa bakaa ya USD 35,006.82 sawa na asilimia 15 mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2023 kama inavyoonekana kwenye jadweli la hapo chini:-

### Jadweli Nambari 17: Utendaji wa kifedha wa Mpango wa Chakula katika Skuli za Msingi

| Maelezo | Utendaji wa Kifedha (USD) | |
|---|---|---|
| Salio anzia 1/7/2022 | | **195,149.59** |
| **Jumlisha:** Kiasi cha fedha kilichopokelewa: | | |
| Shirika la 'Table for Two International' (TfT) | **4,765.01** | |
| Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | **28,793.72** | **33,558.73** |
| **Jumla ya fedha iliyopatikana** | | **228,708.41** |
| **Toa:** Fedha iliyotumika | | **193,701.59** |
| **Bakaa ya 30/06/2023** | | **35,006.82** |

*Chanzo: Ripoti ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2022/2023*

# SURA YA NNE



# 4.0 DOSARI ZILIZOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA TAASISI ZA UMMA

Sura hii inaeleza dosari zilizobainika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa taasisi za umma ambapo imebainisha mapungufu yaliyojitokeza katika hatua za utekelezaji kwa kila mradi uliokaguliwa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Miongoni mwa dosari zilizobainika ni kutokuwasilishwa kwa rasimu za Mikataba katika Afisi ya Mwanasheria Mkuu jambo ambalo limepelekea kujitokeza utekelezaji wa miradi chini ya kiwango, kutokukamilika kwa wakati kwa baadhi ya miradi, ongezeko la gharama zisizo za msingi zilizopelekea baadhi ya taasisi kushindwa kuendeleza mradi kama ilivyokusudiwa na hatimae kutokupatikanwa kwa tija iliyokusudiwa. Pamoja na dosari hizo imebainika uwepo wa baadhi ya miradi kutokuendana na gharama halisi ya fedha iliyotumika (value for money) na kusababisha hasara kwa Serikali.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilikagua utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Washirika wa Maendeleo.

## 4.1 WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI

### 4.1.1 MRADI WA MABADILIKO NA UPATIKANAJI WA SEKTA YA NISHATI ZANZIBAR (ZESTA)

**Utangulizi**

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepokea ufadhili kutoka Benki ya Dunia kutekeleza Mradi wa Mabadiliko na upatikanaji wa Sekta ya Nishati Zanzibar (ZESTA) kwa kipindi cha miaka sita kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2027.

Mradi huo unatekelezwa na vitengo viwili ikiwemo Wizara ya Maji, Nishati na Madini (MoWEM-PIU) na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO-IU). Mpango huu chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia kwa sasa unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Januari, 2021. Fedha za Ruzuku kwa kipindi kilichotajwa zimepangwa kuwa ni USD 6,031,011.

**Malengo ya Mradi**

Mradi huu unasaidia mabadiliko ya Sekta ya Umeme Zanzibar kwa kuharakisha juhudi za upatikanaji wa umeme wa uhakika pamoja na kuongeza ufanisi wa uzalishaji wa nishati mbadala Zanzibar, pamoja na kuibadilisha ZECO kutoka Shirika la Usambazaji hadi kuwa la kusimamia mfumo wa kisasa wenye mfumo Jumuishi wa nishati mbadala, Mfumo wa Kuhifadhi Nishati ya Betri (BESS), na Mfumo wa Udhibiti wa Usimamizi pamoja na Upatikanaji wa Data ya gridi pana (SCADA).

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.1.1 Fedha za Mradi ambazo hazikutolewa USD 2,401,605.98

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 Mradi wa ZESTA ulipanga kutumia kiasi cha USD 3,079,147 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi. Hata hivyo, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 kiasi cha USD 677,541.02 zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia 22 na kupelekea USD 2,401,605.98 sawa na asilimia 78 ya fedha zilizoidhinishwa katika bajeti kutopokelewa.

Shughuli za mradi zenye jumla ya USD 2,401,605.98 zilizopangwa hazikufanyika na hivyo kusababisha malengo yaliyopangwa kutotekelezwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi wa ZESTA kuhakikisha unafanya ufuatiliaji ili kuhakikisha kuwa fedha zilizoidhinishwa kwenye bajeti zinatolewa. Pia, uongozi wa Mradi unashauriwa kuweka vipaumbele katika utekelezaji wa shughuli za mradi. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 18: Fedha za mradi ambazo hazikutolewa**

| Nam | Maelezo | Bajeti iliyoidhinishwa (USD) | Kiasi kilichotumika (USD) | Kiasi kisichotolewa (USD) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Msaada wa kiufundi na msaada wa utekelezaji wa mradi | 2,149,147 | 620,301.35 | 1,528,845.65 |
| 2. | Uboreshaji wa ufanisi wa nishati | 860,000 | 0 | 860,000 |
| 3. | Kuondoa Tofauti ya Jinsia katika sekta ya nishati | 70,000 | 57,239.67 | 12,760.33 |
| **Jumla** | | **3,079,147** | **677,541.02** | **2,401,605.98** |

#### 4.1.1.2 Kuchelewa kuwasilishwa kwa Rasimu ya Mkataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kwa mujibu wa Kanuni ya 47(1)(2) ya Kanuni ya Ununuzi na Undoshaji wa Mali za Umma ya mwaka 2020 inataka makubaliano yoyote yanayohusiana na manunuzi ambayo thamani itakuwa na kiwango cha juu yatathibitishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa na wahusika ambapo Afisa Masuuli ndani ya siku saba (7) baada ya kutoa uamuzi atawasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali rasimu ya mkataba ili kuthibitishwa.

Ukaguzi ulipitia Mikataba mbalimbali ya miradi ya ZESTA inayohusiana na usambazaji wa bidhaa na kubaini uwepo wa ucheleweshaji wa kuwasilisha rasimu ya mkataba kwa Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa na wahusika. Ucheleweshaji wa mikataba hiyo ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 19: Ucheleweshaji wa mikataba kwa Mwanasheria Mkuu**

| Kumbukumbu za Mkataba | Kiasi cha Mkataba (USD) | Tarehe ya Tuzo ya Mkataba | Tarehe ya uwasilishaji Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | Idadi ya siku zilizochelewa |
|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa Kompyuta na Vifaa kwa mkataba namba TZ-MOWEM-292675-GO-RFQ | 40,181.21 | 22/08/ 2022 | 04/10/2022 | 33 |
| Ununuzi wa Gari kupitia mkataba namba TZ-MOWEM-292723 -GO-RFQ | 81,356.96 | 22/08/2022 | 04/10/2022 | 33 |

*Chanzo: Jalada la Mikataba*

### 4.1.2 MRADI WA MSAADA WA SEKTA YA NISHATI ZANZIBAR - ZESS

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliomba msaada wa sekta ya Nishati kutoka Serikali ya Sweden mwaka 2003 ambapo Sweden ilifadhili Mradi wa Kusaidia Sekta ya Nishati Awamu ya Kwanza kuanzia mwaka 2007 hadi 2010.

Mradi wa ZESS unafadhiliwa na Serikali ya Sweden kupitia SIDA, na kutekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa msaada wa Multiconsult Norge AS ya Norway, kulingana na makubaliano jumla ya SEK milioni 47 zikiwemo gharama za ufuatiliaji za SIDA zilitolewa.

Malengo ya jumla ya Mradi wa ZESS awamu ya pili yalikuwa ni upatikanaji wa umeme endelevu Zanzibar ili kuchangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya jamii.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 4.1.2.1 Upungufu wa fedha za kugharamia shughuli za Mradi

Ukaguzi ulipitia ripoti za mpango wa mradi pamoja na kufanya majadiliano na wasimamizi wa Mradi na kubaini kwamba baadhi ya shughuli za Mradi ambazo zilipaswa kutekelezwa kwa mujibu wa fedha zilizolengwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 hazikuweza kutekelezeka kutokana na uhaba wa fedha za Mradi .

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 ukaguzi ulibaini Mradi ulikuwa na bakaa ya shilingi 128,719,936 katika Akaunti za benki za mradi wakati shughuli zilizopangwa kutekelezwa ziligharimu jumla ya shilingi 154,314,132.40 jambo ambalo limepelekea shughuli za mradi kutotekelezwa.

Kutokuwepo kwa fedha za kutosha za kugharamia shughuli za mradi kunaweza kusababisha uwepo wa madai kwa shughuli zilizokwisha kutekelezwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuhakikisha unafanya ufuatiliaji wa karibu kwa washirika wa maendeleo ili fedha iliyopangwa na kuidhinishwa ipatikane kwa wakati kutekeleza shughuli za Mradi zilizokusudiwa.

Hali halisi ya shughuli za Mradi pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa ni kama inavyonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 20: Fedha za Mradi ambazo hazijalipwa na Washirika wa Maendeleo**

| Nam | Jina la Mfadhili | Maelezo | Kiasi cha Fedha (SEK/USD) | Kiasi cha fedha (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mult Consult | Fedha ambazo hazijalipwa | SEK 196,000 | 46,209,158.8 |
| 2. | Hexing Electrical Co. Ltd | Malipo ya mwisho ya mkataba wa usambazaji wa mita za AMR | USD. 46,456.8 | 108,104,973.6 |
| **Jumla** | | | | **154,314,132.4** |

#### 4.1.2.2 Ukaguzi katika Maeneo ya Utekelezaji shughuli za Mradi

Ukaguzi ulifanya ziara ya kutembelea maeneo tofauti ya utekelezaji wa shughuli za mradi za uwekaji wa mita za AMR kwa upande wa Unguja na Pemba katika maeneo yafuatayo Wesha, Shumba, Makangale, Wete, Tibirinzi kwa upande wa Pemba na maeneo ya Nungwi, Matemwe, Pwani Mchangani, Michamvi, Chwaka, Pongwe, Paje, Makunduchi, Chukwani, Fumba na Kiembe Samaki kwa upande wa Unguja.

Aidha, ukaguzi umebaini Uwekezaji wa Mita aina AMR zilizowekwa hazikuwekewa Ulinzi kwa ajili ya kulinda uharibifu au madhara yanayoweza kutokea katika maeneo yaliyofungwa Mita hizo.

Maeneo yaliyowekwa Mita hizo ni Jadida Wete Pemba ambapo ufungaji wa Mita kwenye maeneo ya Barabara Kuu pamoja na eneo la Michamvi Unguja katika Hoteli ya Karafuu iliwekwa kwenye nguzo za Umeme ambazo watu hutumia kama sehemu za kutupa taka.

**Picha Nambari 1: Uwekaji wa Mita za AMR pasipokuwa na Ulinzi**



*Uwekaji wa AMR katika maeneo ya Barabara Kuu*



*Uwekaji wa Mita aina ya AMR kwenye Sehemu zenye Taka eneo la Michamvi*

## 4.2 OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

### 4.2.1 MRADI WA MSAADA WA TAASISI KWA UHAMASISHAJI WA RASILIMALI ZA NDANI NA UTAWALA WA MALIASILI (ISP-DRMNRG)

Mradi wa Msaada wa Kitaasisi wa Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani na Utawala wa Maliasili (ISP-DRMNRG) ulianzishwa tarehe 21/6/2017 na Rais wa Zanzibar kwa kutumia uwezo aliopewa chini ya kifungu nambari 42 cha Katiba ya Zanzibar ya 2010.

Utendaji wa Mradi huo umezingatia Dira ya 2050, Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs), Mpango Mkakati, Mpango Kazi wa Mfumo wa Matumizi ya Muda wa Kati (MTEF), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar (ZSGRP), Sera ya Serikali ya Mitaa ya Zanzibar ya 2014, na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 - 2025, ambayo inabainisha dira, dhamira na shabaha zinazoendana na sera na mikakati ya Serikali.

**Malengo ya Mradi**

Lengo kuu la mradi ni kukuza ukuaji jumuishi kwa kusaidia maendeleo ya sekta ya maliasili na kuimarisha uhamasishaji wa rasilimali za ndani. Mradi pia unaunga mkono juhudi zinazolenga kuongeza uwezo, uwajibikaji na uadilifu katika usimamizi wa rasilimali za umma kwa uangalizi muhimu na taasisi za kiuchumi.

**Wanufaika wa Mradi**

Taasisi zinazonufaika na Mradi zilichaguliwa kwa kuzingatia hitaji la kusaidia Wizara na Taasisi zinazohusika kikamilifu katika maeneo yanayoakisi majukumu ya kimsingi kama ilivyoainishwa katika Sera za Utawala Bora. Mambo makuu yaliyozingatiwa katika Taasisi hizo ni uwajibikaji, uwazi na uadilifu katika usimamizi wa rasilimali za umma.

**Taasisi zinazonufaika na mradi huu ni hizi zifuatazo:-**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wizara ya Maji, Nishati na Madini, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (PO-FP), Idara ya Sera ya Fedha za Nje (DFFP).

**Vipengele vya Mradi**

Mradi wa ISP-DRMNRG una vipengele vitatu (3):-

Kipengele cha 1: Kuimarisha Utawala katika Maliasili.

Kipengele cha 2: Kuimarisha Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani.

Kipengele cha 3: Kitengo cha Uratibu wa Mradi (PCU).

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 4.2.1.1 Fedha za mradi ambazo hazikutumika USD 93,765.99

Mradi wa Msaada wa Kitaasisi wa Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani na Utawala wa Maliasili (ISP-DRMNRG) ulikadiriwa kutumia jumla ya USD 713,212.22 ambapo hadi kufikia Juni, 2023 mradi uliingiziwa kiasi cha USD 713,211.20 na kutumia jumla ya USD 619,445.21 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali zilizoidhinishwa. Hata hivyo, ukaguzi umebaini kwamba pamoja na kuwepo kwa fedha hizo, baadhi ya shughuli za mradi hazikuweza kutumia kikamilifu fedha zilizopo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mradi kuhakikisha utekelezaji wa miradi ijayo fedha zilizotengwa ndani ya mwaka wa fedha husika zinatumika ndani ya muda uliopangwa ili lengo la Serikali katika kuwafikishia huduma wananchi kwa wakati inafikiwa. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

## Jadweli Nambari 21: Fedha ya mradi ambazo hazikutumika

| Namba | Shughuli ya Mradi | Lengo la mradi | Kiasi cha fedha kilichokadiriwa (USD) | Kiasi cha fedha kilichopatikana ( USD) | Kiasi cha fedha Kilichotumika ( USD) | Tofauti (USD) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kujenga uwezo wa usalama wa mifumo na mitandao. | Kuimarisha utawala bora katika sekta ya maliasili | 18,654.00 | 18,654.00 | 15,808.08 | 2,850.92 |
| 2. | Ununuzi na uingizaji wa programu za uendeshaji | Kuimarisha utawala bora katika sekta ya maliasili | 4350.00 | 4,350.00 | 4,156.28 | 193.72 |
| 3. | Ununuzi na ufungaji wa vifaa vya mtandao na TEHAMA LoT- na Lot-2 Mtawalia | Uhamasishaji wa Rasilimali za Ndani | 500,000 | 500,000.00 | 480,927.66 | 19,072.34 |
| 4. | Mafunzo | | 89,044.00 | 89,044.00 | 56,448.44 | 32,595.56 |
| 5. | Uhamasishaji wa ukusanyaji wa mapato | uhamasishaji wa rasilimali za ndani | 17,498.00 | 17,498.00 | 3,738.76 | 13,759.24 |
| 6. | | | 13,503.25 | 13,502.23 | 6,787.58 | 6,714.65 |
| 7. | Gharama ya uendeshaji | Utekelezaji na usimamizi wa mradi | 70,162.97 | 70,162.97 | 51,578.41 | 18,584.56 |
| **Jumla** | | | | | | **93,770.99** |

#### 4.2.1.2 Malipo yaliyofanyika bila stakabadhi za kielektroniki shilingi 35,253,200

Kifungu cha 23 (1) cha Sheria namba 7 ya Sheria ya Usimamizi na Uendeshaji wa Kodi ya mwaka 2009 kinamtaka mtu anayesambaza bidhaa au kutoa huduma iwe kwa mkopo au kwa fedha taslimu, au anapokea malipo ya bidhaa zinazotolewa au huduma iliyotolewa atatoa risiti ya kielektroniki ya malipo hayo.

Kwa mujibu wa barua yenye Kumb:WN/ORFM/2022/VOL.V/20 ambapo ukaguzi ulibaini Mradi wa ISP-DRMNRG ulitumia jumla ya shilingi 35,253,200 bila ya uwepo risiti ya EFD licha Mradi kutoa agizo la kuwataka wazabuni kuwasilisha stakabadhi za madai ya malipo (Ankara) na risiti kwa kutumia mashine za kielektroniki (EFD) jambo ambalo halikutekelezwa na wazabuni hao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi wa ISP-DRMNRG uhakikishe kwamba unafuata matakwa ya sheria ya usimamizi na utawala wa kodi kwa kudai na kuhifadhi risiti za kielektroniki kila baada ya kufanya malipo kwa ajili ya ukaguzi. Hali halisi ni kama inavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 22: Malipo yaliyofanyika bila ya stakabadhi za Kielektroniki**

| Tarehe ya Malipo | Maelezo | Hati Namba ya Malipo | Aliyelipwa | Kiasi cha fedha (Shs) |
|---|---|---|---|---|
| 25/11/2022 | Malipo ya Ada ya Mafunzo kwa Wafanyakazi 10 wa DFFP | 02/11 | University of Dar es Salaam | 35,253,200 |
| **Jumla** | | | | **35,253,200** |

### 4.2.2 MRADI WA UKUZAJI UCHUMI JUMUISHI ZANZIBAR - (BIG-Z)

Mradi wa Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (Boosting Inclusive Growth for Zanzibar) unalenga kuimarisha miundombinu na huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2026 kwa gharama za jumla ya shilingi za Kitanzania bilioni 346.5 na umefadhiliwa na Benki ya Dunia kwa ufadhili wa jumla ya USD milioni 150 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi kwa Unguja na Pemba.

**Vipengele vya Mradi**

Mradi huu una vipengele vinne (4) ambavyo ni kama vifuatavyo:-

**Kipengele cha 1: Maendeleo ya Pamoja ya Maeneo**

Kipengele hiki kina bajeti ya jumla ya Dola za Marekani Milioni 126 kwa lengo la kufadhili uwekezaji na shughuli mbalimbali ili kukabiliana na changamoto mbalimbali za maendeleo katika maeneo ya aina tatu: msingi wa Miji, maeneo ya mijini yanayokua kwa kasi, na Miji/Vijiji vinavyoibuka.

**Kipengele cha 2: Uimarishaji wa Kitaasisi, Ubunifu na Ushirikiano**

Sehemu hii ina jumla ya bajeti ya USD milioni 13 na itazingatia maendeleo ya Taasisi na kujenga uwezo, ikiwa ni pamoja na fedha za Manispaa, usimamizi wa Miji, na kuimarisha mazingira na udhibiti wa Maendeleo.

**Kipengele cha 3: Usimamizi wa Mradi, Uendeshaji, Ufuatiliaji naTathmini**

Kipengele hiki kina bajeti ya jumla ya USD Milioni 11 kwa lengo la kusaidia usimamizi wa Mradi.

**Kipengele cha 4: Kipengele cha Kukabiliana na Dharura**

Kipengele hiki kitakuwa kipengele cha Majibu ya Dharura kwa hali zenye uhitaji wa haraka wa usaidizi.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**4.2.2.1 Shughuli za Mradi ambazo hazijatekelezwa zenye thamani ya USD 1,051,546**

Katika tathmini ya utekelezaji na utendaji kazi wa shughuli mbalimbali zilizopangwa na Mradi, ukaguzi ulibaini uwepo wa baadhi ya shughuli za mradi ambazo hazikutekelezwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 zenye thamani ya USD 1,051,546.

Hali hii ya kutokutekeleza shughuli za mradi zilizokusudiwa kufanywa kunapelekea huduma iliyokusudiwa kutowafikiliya wananchi, jambo ambalo linaweza kuleta mfumko wa bajeti katika siku zijazo ili kukidhi mabadiliko ya bei ambao unaweza kuathiri malengo ya Mradi ya kutoa huduma kwa jamii kwa kiwango kinachohitajika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa mradi kuhakikisha kuwa shughuli zote zilizopangwa kwa mwaka husika zinatekelezwa kulingana na mpango wa Mradi kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 23: Shughuli ambazo hazikutekelezwa

| Namba | Shughuli | Kiasi cha fedha kilichopangwa (USD) |
|---|---|---|
| 1. | Kazi za Ujenzi | 521,700 |
| 2. | Mpango wa Utekelezaji wa Makazi mapya | 529,846 |
| **Jumla** | | **1,051,546** |

#### 4.2.2.2 Dosari iliyobainika katika hati ya Mkataba

Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Kampuni ya Diamond Motors Limited iliingia mkataba namba RFB No: TZ-POF-248687-GO-RFB kwa ajili ya usambazaji wa gari mpya aina ya Pick Up 4WD Double Cabin uliyosainiwa tarehe 28 Septemba, 2022 kwa thamani ya shilingi 413,392,200

Kifungu cha 16.5 cha masharti ya jumla ya mkataba, kinaeleza kwamba Kipindi cha ucheleweshaji wa malipo kitakuwa siku 60 ambacho Mnunuzi atastahiki kulipa riba kwa Msambazaji.

Ukaguzi ulipitia vifungu mbalimbali vya mkataba, na kubaini kuwa kifungu cha 16.5 kina manufaa zaidi kwa msambazaji endapo Mnunuzi atachelewa kufanya malipo kwa wakati kulingana na makubaliano ya mkataba. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa mkataba huu haukuwa na kipengele kinachoonyesha hatua zitachukuliwa iwapo msambazaji atashindwa kuwasilisha bidhaa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba au kuvunja mkataba bila makubaliano ya pande zote mbili.

Kutokuwepo kwa kifungu kinachoonesha hatua stahiki za kuchukuliwa endapo mtoaji huduma atachelewesha kusambaza bidhaa husika kunaweza kusababisha kutotekelezwa kwa shughuli za mradi zilizokusudiwa kwa muda uliopangwa.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mradi kuhakikisha kwamba mikataba inayosainiwa lazima ifanyiwa uhakiki wa kutosha kabla ya kusainiwa.

## 4.3 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

### 4.3.1 MRADI WA UIMARISHAJI WA ELIMU YA SEKONDARI ZANZIBAR (ZISP)

Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari Zanzibar (ZISP) umefadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (IDA) ambao unaboresha elimu ya Sekondari katika visiwa vya Zanzibar na kuweka mazingira mazuri ya kujifunzia na masomo yaliyokusudiwa Mradi huu unatarajiwa kuwanufaisha jumla ya watu 170,000 katika kipindi cha miaka mitano (5) ambapo walengwa Wakuu ni wanafunzi wa darasa la juu la msingi na sekondari ya chini pamoja na kuwanufaisha Walimu, Walimu Wakuu na wafanyakazi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

## Vipengele vya Mradi

Mradi una vipengele vinne ambavyo ni:-

**Kipengele cha 1:** Itahusu ufundishaji bora wa Hisabati, Sayansi na Kiingereza (USD milioni 7).

Kipengele hiki kitazingatia aina mbili za shughuli:-

- Kutoa mafunzo upya kwa walimu waliokazini waliochaguliwa ili kuongeza upatikanaji wa walimu wa Hisabati na Sayansi katika madarasa ya chini na ya sekondari.
- Marekebisho ya usimamizi wa walimu ili kuimarisha uwajibikaji wa walimu na miundo ya motisha.

**Kipengele cha 2:** Uboreshaji wa uhuru wa Skuli na Mazingira ya Kujifunza (USD milioni 9). Kipengele hiki kitazingatia aina mbili za shughuli:-

- Uboreshaji wa Ruzuku ya Skuli ambao utazingatia namba ya wanafunzi walioandikishwa katika kiwango cha Sekondari.
- Utendaji - Ruzuku ya Ufaulu ambayo itazawadiwa kwa skuli zitakazoonesha kufanya vizuri katika mitihani yao ya darasa la 6 na kidato cha pili katika Hesabu, Sayansi na Kingereza.

**Kipengele cha 3:** Vitovu vya Kuimarisha mafunzo ya Hisabati, Sayansi na Mafunzo ya Kiingereza (USD milioni 17). Kipengele hiki kitalenga kusaidia utoaji wa nyenzo/rasilimali za kujifunzia kwa ajili ya mafanikio yaliyoboreshwa ya Hesabu, Sayansi na Kingereza.

**Kipengele cha 4:** Mabadiliko ya Mifumo na Usimamizi wa Mradi (Dola za Marekani milioni 2). Kipengele hiki kitalenga maeneo manne:-

- Mageuzi ya mitihani;
- Mipango ya mifumo ya elimu;
- Kuimarisha mifumo ya data na kusaidia Mradi katika ufuatiliaji na tathmini (Hesabu na Kingereza).
- Msaada wa utekelezaji wa mradi.

## Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 4.3.1.1 Fedha za mradi zilizokopwa ambazo hazijarejeshwa USD 130,464

Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zinaongozwa na makubaliano ya ufadhili wa kifedha ambayo inawataka watekelezaji wa mradi kuhakikisha fedha zinazotolewa zinatumika kikamilifu katika shughuli za mradi zilizopangwa.

Ukaguzi ulipitia taarifa za fedha za Mradi wa ZISP na kubaini uwepo wa kiasi cha USD 130,464 hadi tarehe 30 Juni, 2023 zilikuwa ni bakaa ya fedha ambazo hazijatumika ambapo ukaguzi ulibaini Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar mnamo tarehe 28 Juni, 2023 ilianza mchakato wa marejesho ya fedha hiyo ( USD 130,464)

Lakini hadi ukaguzi unakamilika bado kiasi hicho cha fedha hakijarejeshwa. Hali hii ni kwenda kinyume na matakwa yaliyopo kwenye hati za mradi husika, kama vile Mkataba wa Fedha, Muongozo wa Utekelezaji wa Mradi, Hati ya Makubaliano (MoU) na miongozo mingine inayosimamia uendeshaji wa mradi, pia pamoja na uwepo wa mapungufu katika udhibiti wa ndani kwenye usimamizi wa fedha za mradi.

Kutokurejeshwa kwa fedha zilizokopwa kunaathiri utekelezaji wa shughuli zilizopangwa za miradi hiyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa mradi na watekelezaji kuhakikisha fedha zilizokopwa zinarejeshwa mara moja kwenye mradi husika ili kukwepa madhara ya kutotekelezeka kwa shughuli zilizopangwa.

### 4.3.1.2 Fedha ya mradi ambazo hazikutumika USD 140,399.97

Kwa mujibu wa Mkataba wa Fedha kutoka Benki ya Dunia inawataka watekelezaji wa mradi kuhakikisha kuwa fedha zilizotolewa zinatumika katika shughuli za mradi zilizokusudiwa.

Ukaguzi ulipitia kumbukumbu za matumizi ya fedha za mradi na kubaini jumla ya fedha za Kimarekani USD 140,399.97 kutoka Benki ya Dunia ambapo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imeshindwa kutumia fedha hizo kama zilivyotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi, hali hii imesabishwa kutokana na kuchelewa kwa fedha hizo kutoka Benki ya Dunia katika kipindi cha janga la Uviko-19 na kusababisha ugumu kwa baadhi ya shughuli kutotekelezwa jambo ambalo limesababisha kiasi hicho cha fedha kurejeshwa Benki ya Dunia ili kuzingatia masharti yaliyowekwa katika hati husika ya mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi wa ZISP kuhakikisha inachukua jitihada za makusudi za kuharakisha matumizi ya fedha za mradi kwa shughuli zilizopangwa kwa wakati.

#### 4.3.1.3 Dosari iliyojitokeza katika kituo cha Limbani - Pemba

Ukaguzi ulitembelea Kituo cha Ubunifu wa Sayansi cha Limbani - Pemba kilichojengwa kupitia mradi wa ZISP, na kubaini uwepo wa dosari iliyojitokeza katika kituo hicho ambayo ilisababishwa na bomba la kuteremshia maji lililofungwa vibaya kwa ajili ya ukusanyaji wa maji ya mvua ili kuruhusu mwelekeo wa mtiririko wa maji ya mvua kutoka nje ya eneo la kituo, ambalo limeweza kusababisha mmong'onyoko wa ardhi katika eneo la mradi. Kuendelea kujitokeza kwa dosari katika utekelezaji wa shughuli za mradi kunaweza kukasabisha hatari za usalama na uimara wa jengo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi kusimamia vizuri shughuli za mradi zilizopangwa ili malengo ya mradi yafikiwe ikiwemo tija, usalama na ubora kwa watumiaji. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha ifuatayo:-



*Dosari katika jengo la Kituo cha Ubunifu wa Sayansi cha Limbani: 9 Novemba, 2023*

### 4.3.2 MRADI WA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA WA ELIMU AWAMU YA PILI (GPE II)

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imekuwa ikitekeleza Mpango wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu (GPE) tangu mwaka 2014. Programu ya GPE II inafadhiliwa na Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu na inasimamiwa na Ubalozi wa Sweden kama Wakala wa Ruzuku (GA). Awamu ya kwanza ya programu ilikamilishwa kwa ufanisi mwaka 2016. Madhumuni ya jumla ya awamu ya kwanza ya programu ilikuwa kuboresha upatikanaji wa elimu kwa usawa na kuboresha umuhimu na ubora wa elimu katika sekta nzima ya elimu.

Utekelezaji wa Mradi wa awamu ya pili (GPE II) ulianza Julai, 2018 baada ya kusaini hati ya makubaliano kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) na Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu (GPE). WEMA inatarajia kutumia awamu ya pili (GPE II). ruzuku ya kuunganisha na kupanua maendeleo yaliyofikiwa chini ya ufadhili wa awamu ya pili, kuongeza upatikanaji wa elimu katika mfumo mzima kwa kuendeleza programu ya elimu jumuishi na kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote wa Zanzibar. Mradi huu unatarajiwa kufanya kazi kwa muda wa miaka minne, yaani kuanzia Aprili, 2018 hadi tarehe 30 Juni, 2022 lakini hutolewa kila mwaka; mfuko huo umegawanywa katika awamu zisizohamishika na zinazobadilika.

Mpango wa Mradi wa Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu awamu ya pili ulitangazwa rasmi kuanza kutumika tarehe 27 Machi, 2018. Mpango wa Zanzibar (GPE II) umepewa jumla ya Dola za Kimarekani 5,761,100 na Bodi ya Wakurugenzi ya Ushirikiano wa Kimataifa wa Elimu (GPE II). Ili kutekeleza shughuli kwa kipindi cha miaka minne, hadi tarehe 30 Juni, 2022 na sasa Mradi umeongezwa muda hadi Septemba, 2023.

**Lengo la Mradi**

Lengo kuu la mradi ni kuhakikisha watoto wanazidi kuingia skuli za msingi katika umri unaotakiwa na wakiwa na miaka 2 ya elimu ya awali na watoto wote wasiojiweza (hasa maskini na watoto waliokuwa na mahitaji maalum) wanaweza kufikia ngazi zote za elimu ya awali, msingi na sekondari. Inatarajiwa kuwa takriban watoto 35,000 watakuwa wanufaika wakuu pamoja na walimu, wazazi na jamii.

### Vipengele vya Mradi

Mradi uliratibu shughuli zilizotekelezwa kupitia vipengele vitatu(3) vifuatavyo:-

### Kipengele 1: Elimu ya Awali

Idara ya Elimu ya Awali na Msingi ina jukumu la utekelezaji wa kipengele cha 1 cha Mradi wa GPE II. Katika utekelezaji huo, Idara hiyo inafanya kazi kwa kushirikiana na Idara nyengine za Wizara ambazo ni Idara ya TEHAMA katika Elimu, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Taasisi ya Elimu Zanzibar, Mkaguzi Mkuu wa Elimu, Baraza la Mitihani Zanzibar na Idara ya Mafunzo ya Ualimu.

### Kipengele 2: Elimu Shirikisho (IE)

Kipengele hiki kinaelekea kuongeza idadi ya skuli na walimu wanaokidhi viwango vya elimu jumuishi.

### Kipengele 3: Usimamizi na Uratibu wa Mradi

Usimamizi wa miradi unaendelea na uratibu wa kila siku na ufuatiliaji wa utekelezaji wa mradi ambayo yafuatayo yalifanyika;

- Uongozi uliandaa na kufanyika warsha ya siku moja ya uhamasishaji wa mradi kwa Wilaya nne; Magharibi B, Kaskazini B, Wete na Chake - Chake.
- Vikao vinne vya Kamati ya Uongozi wa Mradi kujadili maendeleo ya utekelezaji wa mradi vilifanyika. Mikutano hiyo iliidhinisha ripoti ya maendeleo ya robo mwaka na mipango ya robo mwaka ya miradi. Uongozi pia ulifanya vikao sita na watekelezaji wakuu ili kujadili changamoto za utekelezaji wa mradi na kubadilishana mawazo juu ya njia ya kusonga mbele.
- Uongozi uliandaa mkutano wa mwaka wa mapitio ya pamoja ya sekta ya elimu mwezi Februari, 2019. Mkutano huo ulihusisha wadau kutoka ndani na nje ya Zanzibar wakiwemo washirika wa maendeleo wanaosaidia elimu.

### Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 4.3.2.1 Kasoro zilizobainika katika utekelezaji wa Mradi

Ukaguzi ulifanya ziara katika maeneo ya Mradi kwa ajili ya kuhakiki kazi za ukamilishaji wa madarasa kumi (10) ya awali, kati ya hayo jumla ya madarasa matano (5) yalijengwa ambayo ni Pagali, Guruweni, Pangani, Uwandani Kibonde Mzungu na Kibubwi kwa upande wa Unguja na madarasa matano (5) kwa upande wa Pemba ambayo ni Chanjaani, Chanjamjawiri, Ng'ombeni, Ngagu na Ndagoni na kubaini uwepo wa dosari katika utekelezaji wa mradi huo.

Hali hii ilisababishwa na kutokuwepo kwa usimamizi wa kutosha wa timu ya kutathmini zabuni za mradi ili kupata mzabuni anaefaa kwa mujibu wa makubaliano.

Kukosekana kwa usimamizi wa kutosha wa kazi za ukarabati zilizofanywa shuleni kulisababisha kasoro mbali mbali ambazo zilitakiwa kurekebishwa wakati wa usimamizi wa kila siku.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa mradi kuhakikisha kuwa unafanya jitihada za makusudi za kufuatilia shughuli za ukarabati kwa madhumuni ya kugundua kasoro yoyote iliyotokea wakati wa shughuli za ujenzi. Dosari hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Picha Nambari 2: Usimamizi usioridhisha wa Mradi




*Uwekaji wa mlango usioridhisha - Shule ya Msingi Guruweni*



*Mlango wa darasa katika shule ya awali - Matola imevunjika kabla ya kutumika*



*Kuanguka na dari katika shule ya awali Pangeni*



*Kutokamilika kwa Paa katika shule ya Msingi Kibumbwi*

### 4.3.3 MRADI WA ELIMU YA JUU KWA MABADILIKO YA KIUCHUMI (HEET)

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imepata mkopo kutoka Benki ya Dunia (WB) unaolenga kuboresha mfumo wa elimu nchini. Mradi huo unajulikana kama Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET).

Mradi wa HEET unagharimu USD milioni 425 kwa Tanzania Mradi huu unafadhiliwa na IDA. Mradi huo uliidhinishwa na Benki ya Dunia Mei, 2021 na utatekelezwa kwa muda wa miaka Mitano (5) na unatarajiwa kufungwa tarehe 15 Julai, 2026. Mradi wa HEET unalenga kuimarisha utoaji wa elimu ya juu kupitia mchanganyiko wa uwekezaji wa ngazi ya chuo kikuu katika kuboresha ubora wa mazingira na programu za kujifunzia na unaboresha usimamizi wa mfumo wa elimu ya juu na kusaidia mazingira bora ya sera.

**Vipengele vya Mradi**

Mradi huu unavipengele vitatu (3) kama vifuatavyo:-

**Kipengele cha 1**: Kuimarisha mazingira ya kujifunzia na mwelekeo wa soko la ajira wa programu katika taaluma za kipaumbele.

**Kipengele cha 2:** Kuimarisha usimamizi wa mfumo wa elimu ya juu.

**Kipengele cha 3:** Msaada kwa Uratibu na Usimamizi wa Mradi.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.3.3.1 Fedha za mradi ambazo hazikutumika shilingi 3,140,485,688

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (HEET) ulipanga kutumia jumla ya shilingi 7,171,630,333 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi.

Ukaguzi ulipitia nyaraka za mradi na kubaini jumla ya shilingi 3,870,897,961 zimeingizwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi zilizopangwa kwa kipindi cha miezi sita, ambapo mradi uliweza kutumia jumla ya shilingi 730,412,273 sawa na asilimia 18.87 ya fedha zilizopokelewa na kupelekea uwepo wa jumla ya shilingi 3,140,485,688 ambazo hazikutumika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi kuhakikisha kunakuwa na usimamizi mzuri wa matumizi ya fedha za mradi juu ya kutekeleza shughuli zote za mradi zilizopangwa kwa mwaka husika kwa mujibu wa bajeti iliyopangwa. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 24: Fedha za mradi ambazo hazikutumika

| Kipengele | Makadirio (Shs) | Matumizi Halisi (Shs) | Tofauti (Shs) |
|---|---|---|---|
| Ujenzi au ukarabati wa miundombinu | 2,082,731,131 | - | 2,082,731,131 |
| Kukuza mtaala na kuanzisha mbinu bunifu za ufundishaji | 114,700,000 | 103,734,417 | 10,965,583 |
| Kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kidijitali | 161,720,830 | 40,484,987 | 121,235,843 |
| Kujenga uwezo wa wafanyakazi wa kitaaluma na uongozi wa chuo kikuu | 1,511,746,000 | 586,192,869 | 925,553,131 |
| **Jumla** | **3,870,897,961** | **730,412,273** | **3,140,485,688** |

### 4.3.4 MRADI WA UJENZI NA UWEZESHAJI WA SHULE ZA SEKONDARI (BADEA II)

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (WEMA) ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeingia mkataba na Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Uchumi Barani Afrika (BADEA) kwa ajili ya kufanyia marekebisho mfumo wake wa elimu tarehe 1 Aprili, 2020 na unatarajiwa kumalizika tarehe 31 Machi, 2023. Mradi huo unalenga katika kuongeza mchango wa Zanzibar katika kufikia malengo ya maendeleo endelevu katika nyanja ya elimu pamoja na kutoa fursa za elimu kwa wanafunzi wa maeneo yanayokabiliwa na mapungufu katika Skuli za Sekondari.

**Vipaumbele vya Mradi wa Ujenzi na Uwezeshaji wa Shule za Sekondari kupitia mkopo wa BADEA II**

Wizara imeandaa mradi huu kwa ajili ya ujenzi wa Skuli za Sekondari na usambazaji wa samani za Skuli na Mabasi ili kukidhi mahitaji ya elimu kwa umma. Mradi huo unajumuisha kazi za ujenzi wa Skuli tatu katika maeneo ya Mfenesini Mjini Magharibi, Gamba Kaskazini Unguja na kijiji cha Kifundi kisiwani Pemba, pamoja na ununuzi wa vifaa.

## Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 4.3.4.1 Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa mradi

Ukaguzi umetembelea maeneo ya utekelezaji ya Mradi wa Ujenzi na Uwezeshaji wa Shule za Sekondari kupitia mkopo wa BADEA II kwa ajili ya kuhakiki kazi zilizotekelezwa za ujenzi wa Hosteli, Mikahawa na Jengo la Utawala huko Kifundi Pemba na Mfenesini pamoja na Gamba kwa upande wa Unguja, ambapo ukaguzi umebaini hali tofauti za ukamilishaji wa shughuli za Mradi kwa hatua ya awali ya utekelezaji, zinazoendelea vizuri na zisizoridhisha kwa hatua ya utekelezaji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi kusimamia vizuri juu ya utekelezaji wa mradi ili kuhakikisha kunakuwa na utekelezaji wa haraka wa ujenzi wa miradi iliyopangwa ili kufikia matarajio ya jamii. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika picha zifuatazo:-

**Picha Nambari 3: Dosari za usimamizi katika Miradi ya Ujenzi**




*Utekelezaji wa ujenzi kiwango cha chini Eneo la Kifundi Pemba*




*Kazi za ujenzi zinazoendelea vizuri maeneo ya Mfenesini Unguja*

### Picha Nambari 3: Dosari za usimamizi katika Miradi ya Ujenzi




*Kazi za ujenzi zisizoridhisha eneo la Gamba Unguja*

## 4.4 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

### 4.4.1 MRADI WA MAENDELEO YA KILIMO NA UVUVI (AFDP)

Mpango wa Maendeleo ya Kilimo na Uvuvi, ni programu inayofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD). Mpango huo utatekelezwa kwa muda wa miaka 6 kuanzia tarehe 9 Aprili, 2021.

Lengo kuu la mradi ni kuimarisha uzalishaji endelevu, kustahamili hali ya hewa na biashara ya mbegu zilizochaguliwa za mazao, uvuvi na ufugaji wa samaki, huku ikitoa kipaumbele maalum kwa uwezeshaji wa wanawake na ushiriki wa vijana. Lengo la jumla la programu ni kaya 260,000 zenye watu takriban 1,300,000 . Jumla ya ufadhili wa programu kwa kipindi cha miaka sita (kuanzia mwaka 2021 hadi 2027) ulikuwa takriban USD milioni 8.84.

**Vipengele vya Mradi**

Mradi una vipengele vitatu (3) muhimu:-

**Kipengele I**: Kuimarishwa kwa Tija ya Mbegu za Mazao, Uvuvi na Ufugaji wa samaki.

**Kipengele II**: Kuboresha ongezeko la thamani ya upatikanaji wa soko na maendeleo ya sekta binafsi.

**Kipengele cha III**: Usimamizi na Uratibu wa Mradi.

**Utekelezaji wa Mpango**

Utekelezaji wa mpango huo utasaidiwa na washirika wakuu wa utekelezaji wakiwemo; Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Taasisi ya Cheti Rasmi cha Mbegu Tanzania (TOSCI), Ushirikiano wa Uvuvi Tanzania (TAFICO), Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) na Kituo cha Maendeleo ya Kilimo cha Majini (ADCs).

#### 4.4.1.1 Uwepo wa matumizi kinyume na Bajeti

Bajeti ni zana muhimu za usimamizi ili kudhibiti matumizi. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 mradi ulikuwa na bajeti ya shilingi 3,603,258,558 ambayo ilitokana na Kazi za Kiraia, Warsha na Mafunzo, Magari, ununuzi wa Vifaa , Ushauri na Usaidizi wa Kiufundi, uboreshaji wa upatikanaji wa soko na gharama za Uendeshaji kwa PCU.

Ukaguzi ulihakiki hati za malipo na kubaini jumla ya shilingi 361,823,837 zilitumika na kupelekea uwepo wa kiasi cha shilingi 3,241,434,721 ambazo hazikutumika kwa shughuli za mradi ukilinganishwa na kiasi cha bajeti iliyopitishwa. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 25: Matumizi kinyume na Bajeti**

| Maelezo | Makadirio (Tshs.) | Matumizi halisi (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) |
|---|---|---|---|
| Kazi za ujenzi | 473,380,271 | 19,124,400 | 454,255,871 |
| Mafunzo na Warsha | 126,156,984 | 9,306,515 | 116,850,469 |
| Magari, Vifaa na Nyenzo | 1,491,248,510 | 28,097,800 | 1,463,150,710 |
| Ushauri na usaidizi wa kiufundi | 309,610,580 | 35,047,322 | 274,563,258 |
| Kuboresha upatikanaji wa soko | 905,312,213 | 2,402,000 | 902,910,213 |
| Gharama ya uendeshaji kwa PCU | 297,550,000 | 267,845,800 | 29,704,200 |
| **Jumla** | **3,603,258,558** | **361,823,837** | **3,241,434,721** |

#### 4.4.1.2 Kuchelewa kwa mchakato wa manunuzi

Kulingana na Mpango wa Mwaka wa Ununuzi wa Programu, katika mwaka wa fedha 2022/2023 programu ilipanga kuanzisha shughuli mbalimbali za ununuzi zinazohusu kazi, bidhaa na huduma za ushauri.

Ukaguzi ulipitia mpango wa manunuzi na kubaini uwepo wa ucheleweshaji wa shughuli zilizopangwa za manunuzi, ambapo shughuli nyingi za manunuzi zilizopangwa hazikuweza kutekelezwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

Ucheleweshaji wa kuanzisha na kukamilisha mchakato wa ununuzi unaweza kuathiri kukamilika kwa malengo mengine ya programu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi kuchukuwa jitihada za makusudi za kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Mradi hususan maafisa manunuzi katika kusimamia manunuzi ya Mradi. Hii inaweza kuhusisha mafunzo juu ya mifumo ya manunuzi ya IFAD. Mchanganuo wa wanunuzi hayo ni kama inavyooneka chini:-

### Jadweli Nambari 26: Ucheleweshaji wa shughuli za Manunuzi

| Namba | Maelezo ya Ununuzi | Tarehe | Dosari zilizobainika |
|---|---|---|---|
| 1. | Ununuzi wa mashine 4 za kukaushia jua kwa gugu bahari na Usakinishaji | 20 Mei, 2023 | Kutokuanza kwa Mchakato wa Ununuzi |
| 2. | Ununuzi wa vifaa viwili (2) kwa ajili ya mashamba ya kitalu kwa ajili ya miche | 20 Aprili, 2023 | |
| 3. | Ununuzi wa vifaa kwa ajili ya mashamba ya majaribio ya mwani katika kina kirefu cha maji | 11 Febuari, 2023 | |
| 4. | Ununuzi na Ufungaji wa Kiwanda cha Kutengeneza Barafu | 20 Mei, 2023 | |
| 5. | Ununuzi wa lori ya kufungia tani kumi. | 19 Machi, 2023 | Inasubiri idhini ya Ripoti ya Tathmini |
| 6. | Ununuzi wa Meli 1 ya Uvuvi wa Baharini iliyo na vifaa kamili | 10 Aprili, 2023 | Mchakato wa Ununuzi bado haujaanza |
| 7. | Ununuzi wa gari. | 29 Aprili, 2023 | Inasubiri kusainiwa kwa mkataba |
| 8. | Ujenzi na vifaa vya miundombinu ya vituo 2 vya mafunzo ya Uvuvi na Ufugaji wa Bahari. | 9 Aprili, 2023 | Inasubiri na hakuna Kipingamizi kwa michoro |
| 9. | Ukarabati wa Jengo la Maabara ya Utamaduni wa Tishu za Bahari. | 15 Machi, 2023 | Inasubiri ruhusa ya utekelezaji kutoka kwa Mshirika wa Maendeleo |
| 10. | Huduma za ushauri kwa ajili ya Kubuni, Kuchora na usimamizi wa Ujenzi wa maghala ya usindikaji na kuhifadhia samaki baridi | 29 Mei, 2023 | |

*Chanzo : Mpango wa Ununuzi wa Mwaka na Ripoti za Usimamizi wa Mradi*

## 4.5 WIZARA YA AFYA

### 4.5.1 MFUKO WA FEDHA WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR (ZANZIBAR HEALTH BASKET FUND)

Wizara ya Afya pamoja na DANIDA, ilianzisha Mfuko wa Huduma za Afya mwaka 2004 ili kushughulikia masuala ya uhaba wa fedha wa Wilaya, ufanisi na usawa.

Lengo la haraka la Mfuko wa Huduma za Afya lilikuwa ni kuongeza fedha za Wilaya ili kufidia gharama za kawaida ambapo lengo la kati lilikuwa ni kuongeza ufanisi kwa kupeleka maamuzi katika ngazi ya Wilaya.

Madhumuni ya Mpango Kamili wa Afya wa Wilaya ilikuwa ni kuhakikisha kuwa fedha za Sekta za Afya zinapangwa ipasavyo na hatimaye kuleta matokeo ya pamoja na kuboresha huduma za Afya kwa wananchi.

Kwa kuzingatia hatua iliyofikiwa na uwezo uliojengeka, mwaka 2012, Wizara ya Afya pamoja na Wizara ya Fedha iliamua kuunda hesabu ndogo ya pamoja ya Huduma za Afya za Wilaya ili kupatanisha na kuoanisha msaada wa Washirika wa Maendeleo kwa Mpango wa Afya wa Halmashauri na hivyo Mfuko wa Huduma za Afya kubadilika na kuwa Mfuko wa Fedha wa Afya wa Pamoja chini ya umiliki kamili wa Wizara ya Afya.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.5.1.1 Kuchelewa kuingizwa kwa fedha za mradi

Kifungu nambari 13 cha Makubaliano kinaelezea Usimamizi na utoaji wa fedha ambapo kifungu nambari 13.3 kinaelekeza kwamba washirika wa maendeleo wataingiza pesa za mradi kwenye akaunti ya pamoja mwezi wa kwanza wa robo ya kwanza wa mwaka wa fedha.

Ukaguzi umebaini kuchelewa kuingizwa kwa fedha za mradi kutoka kwa washirika wa maendeleo hali iliyosababisha kushindwa kutekeleza shughuli nyingi zilizopangwa.

Hali hii inaweza kusababisha ucheleweshwaji wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa za miradi na itapelekea matokeo yaliyokusudiwa kutofikiwa.

Ukaguzi unashauri washirika wa maendeleo kuingiza fedha za mradi kwa muda uliopangwa kwenye mwongozo wa utekelezaji wa mradi. Hii itarahisisha utoaji wa fedha kwa wakati kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi.

Jadweli lifuatalo linaonyesha muda na kiasi cha fedha kilichotolewa na washirika wa maendeleo kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni, 2023.

**Jadweli Nambari 27: Fedha zilizoingizwa na washirika wa maendeleo**

| Washirika wa maendeleo | Tarehe ya fedha zilivyoingizwa | Kiasi (Tsh.) |
|---|---|---|
| UNICEF | 18/11/2022 | 232,300,000 |
| HIPZ | 27/06/2023 | 10,000,000 |
| **Jumla** | | **242,300,000** |

### 4.5.1.2 Kuchelewa kuingizwa kwa fedha kwa walengwa wa mradi

Kulingana na Mpango wa Utekelezaji kila shughuli imepangwa kwa muda maalum wa kutekelezwa ndani ya kila robo mwaka. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2022/23. Ukaguzi umebaini kulikuwa na ucheleweshaji mkubwa wa kutolewa kwa fedha kutoka hesabu ya pamoja (JHA) kwenda kwenye hesabu za walengwa wa utekelezaji wa mradi.

Kuchelewa kuingiziwa fedha kwa walengwa kunaweza kusababisha kuchelewa kutimia kwa malengo ya mradi na kusababisha usumbufu katika utekelezaji wa mradi, na hatimaye kuathiri kufikia malengo ya mradi.

Kuchelewa kuingiza fedha kwa watekelezaji wa mradi hupelekea kuharibu mipangilio ya uendeshaji wa kazi za mradi zilizopangwa kutekelezwa.

Ukaguzi unapendekeza kurahisisha mchakato wa utoaji wa fedha ili kuharakisha utoaji wa fedha kwa wanufaika wa mradi. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 28: Fedha iliyoingizwa kwenye akaunti za watekelezaji wa Mradi**

| Jina la Hesabu | Tarehe Fedha Iliyoingizwa | Kiasi (Shs) |
|---|---|---|
| Katibu Mkuu Wizara ya Afya | 9/1/2023 | 45,513,503 |
| MOH Central Medical Store | 9/1/2023 | 146,190,000 |
| District Health Services Pemba | 9/1/2023 | 53,452,697 |
| DHMT North 'A' | 9/1/2023 | 14,115,774 |
| DHMT North 'B' | 9/1/2023 | 10,959,730 |
| DHMT Central | 9/1/2023 | 14,925,009 |
| DHMT South | 9/1/2023 | 8,259,763 |
| DHMT Town | 9/1/2023 | 27,001,101 |

| Jina la Hesabu | Tarehe Fedha Iliyoingizwa | Kiasi (Shs) |
|---|---|---|
| DHMT West 'A' | 9/1/2023 | 18,754,762 |
| DHMT West 'B' | 9/1/2023 | 20,953,441 |
| DHMT Chake Chake | 9/1/2023 | 21,187,982 |
| DHMT Mkoani | 9/1/2023 | 19,386,145 |
| DHMT Wete | 9/1/2023 | 21,134,084 |
| DHMT Micheweni | 9/1/2023 | 21,166,009 |
| **Jumla** | | **443,000,000** |

#### 4.5.1.3 Kutoingizwa kwa fedha za Mradi kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar shilingi 800,000,000

Kifungu nambari 6 cha Hati ya makubaliano (MoU) kinatafsiri majukumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo kifungu nambari 6.1(i) kinaitaka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchangia kiasi kilichokubalika kwenye mfuko wa Afya wa pamoja kwa mujibu wa hati ya makubaliano ya pamoja.

Ukaguzi umebaini kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliahidi kuchangia shilingi 800,000,000 kwenye mfuko wa Afya wa pamoja kupitia makubaliano ya pamoja na washirika wa maendeleo.

Mpaka mwaka wa fedha unamaliza Serikali haijachangia fedha hizo ambapo itapelekea kutokutekelezwa kwa baadhi ya shughuli za mradi, aidha ni kwenda kinyume na makubaliano ya pamoja.

Ukaguzi unaishauri Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuchangia fedha kwenye Mfuko wa Afya wa pamoja kama ilivyoahidi ili ziweze kutekeleza shughuli za mradi zilizopangwa.

#### 4.5.1.4 Vifaa ambavyo havijarikodiwa kwenye daftari la ghalani shilingi 37,687,635

Kwa mujibu wa kifungu nambari 31 (2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Afisa masuuli anatakiwa kuhakikisha anaanzisha mfumo wa uendeshaji na uwazi wa usimamizi wa fedha na vihatarishi na udhibiti wa ndani ili kusaidia usimamizi wa matumizi.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya shilingi 37,687,635 zilitumika katika ununuzi wa mafuta na vifaa mbalimbali kulingana na mahitaji ili kuwezesha shughuli za uendeshaji wa Mradi ambapo ukaguzi ulibaini uwepo wa bidhaa zilizonunuliwa ambazo hazikurikodiwa kwenye daftari la ghalani.

Kutokurikodi vifaa katika daftari la ghalani kunaweza kupelekea ukaguzi kua na mashaka na manunuzi hayo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZHBF kuimarisha udhibiti wa ndani kwa kurikodi bidhaa zote zinanzonunuliwa kwenye daftrari la ghalani kabla ya matumizi. Mchanganuo wa vifaa hivyo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 29: Vifaa ambavyo havijaingizwa kwenye daftari la ghalani

| Hati ya malipo | Eneo la matumizi | Kiasi cha fedha (Shs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1/4 18/4/2023 | DHMT West 'A' | 3,000,000 | Salum Transport Company | Ununuzi wa mafuta. |
| 6/5 31/5/2023 | Central Medical store (Unguja) | 3,130,300 | Miembeni Lubricant Center | Ununuzi wa vifaa vya magari. |
| 9/6 30/6/2023 | Central Medical store (Unguja) | 5,150,000 | Tahfif Auto Works | |
| 1/6 6/6/2023 | Central medical store (Pemba) | 15,000,000 | Africom Ltd | Ununuzi wa vifaa vya ICT |
| 10/6 30/06/2023 | Central medical store (Unguja) | 1,500,000 | Khamiar Enterprices Ltd | Ununuzi wa stationaries za ofisi |
| 4/6 30/6/2023 | DHMT Central | 1,788,250 | Adem Store | Ununuzi wa vifaa vya magari |
| 23/6/2023 | DHMT North 'A' | 1,632,000 | G.M Traders | |
| 3/6 23/6/2023 | DHMT Central | 2,000,000 | Atlas Graphics and Digital Advertisement | Ununuzi wa vifaa vya kuandikia. |
| 1/5 2/5/2023 | DHMT West 'A' | 1,987,085 | Quality Trades | |
| 2/6 23/6/2023 | DHMT Central | 2,500,000 | Atlas Graphic and Digital Advertisement | ununuzi wa vifaa vya magari services |
| **Jumla** | | **37,687,635** | | |

### 4.5.2 PROGRAMU YA CHANJO – EPI (GAVI)

Huduma za chanjo zilianzishwa Zanzibar ili kukabiliana na magonjwa ya Surua, TB na Ndui ambapo Zanzibar ilifanikiwa kutokomeza ugonjwa wa Kipindupindu na kuondoa baadhi ya magonjwa yanayoweza kuzuilika ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa chanjo. Huduma za EPI zilianzishwa mwaka 1981 Kisiwani Pemba na baadaye Kisiwani Unguja mnamo mwaka 1983.

Mradi huu unatekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na mashirika mengine ya maendeleo kama vile UNICEF, WHO na GAVI.

Kufikia kipindi cha mwaka 2020 huduma za kawaida za chanjo zilitolewa kupitia vituo 164 vya Afya vya Umma na vya kibinafsi vinavyotoa chanjo kwa wasafiri wa kimataifa kupitia huduma za Afya za Bandari.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.5.2.1 Kutotekelezwa kwa shughuli zilizopangwa zenye thamani ya shilingi 1,001,913,061.43

Wizara ya Afya Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi 1,001,913,061.43 sawa na USD 432,978.85 kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali za CDS kutoka Kitengo cha Idara ya chanjo kilicho chini ya Wizara ya Afya Tanzania Bara.

Ukaguzi ulibaini Mradi ulipitisha matumizi ya fedha hizo kwa mujibu wa barua yenye Kumb. namba CAC.261/433/03 ya tarehe 06 Machi, 2023 kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka 2022/2023, ambapo kiasi cha fedha cha shilingi 1,001,913,061.43 hakikuweza kutumika licha ya kupitishwa na kutengewa kiasi cha fedha katika utekelezaji wa shughuli za mradi. Mchanganuo wa shughuli za mradi zilipopangwa lakin hazikutekelezwa ni kama zinavyoonekana katika jedwali apo chini:-

**Jadweli Nambari 30: Shughuli za mradi ambazo zimepangwa na kutengewa fedha lakini hazikutekelezwa**

| Namba | Shughuli za Mradi | Kiasi kilichopangwa (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | **Uhamasishaji wa Jamii na Mawasiliano** | |
| | DSA kwa washiriki | 6,100,000 |
| | Viburudisho (PHCs) | 1,200,000 |
| | Kurushwa kwa Michezo ya Redio na TV | 1,800,000 |
| | **Jumla Ndogo (A)** | **9,100,000** |

| Namba | Shughuli za Mradi | Kiasi kilichopangwa (Tsh.) |
|---|---|---|
| 2. | **Usambazaji wa chanjo** | |
| | Usambazaji wa chanjo (Kutoka RVS hadi DVS) | 13,370,000 |
| | **Jumla Ndogo (B)** | **13,370,000** |
| 3. | **Utekelezaji wa kampeni** | |
| | DSA kwa Wasimamizi wa Mikoa na Halmashauri | 81,700,000 |
| | Posho za Ushuru wa ziada kwa Watoa Chanjo | 839,139,714 |
| | Mafuta | 58,603,347 |
| | **Jumla Ndogo (C)** | **979,443,061** |
| **Jumla Kuu (A+B+C)** | | **1,001,913,061** |

*Chanjo: Taarifa ya Bajeti*

### 4.5.2.2 Kiasi cha Dawa kilichokwisha muda wa matumizi

Kifungu cha 5(c) cha Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya Zanzibar ya 2006 kinasema kuwa "kulaani na kuamuru uharibifu au utupaji wa bidhaa yoyote iliyodhibitiwa chini ya Sheria hii inayoonekana kuwa haifai kwa matumizi yaliyokusudiwa".

Ukaguzi umebaini jumla ya dozi 834 za chanjo za MR na Covid 19 zilizoingia na kupokelewa Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ambazo zilikuwa zimeisha muda wake wa matumizi na wala hazikurikodiwa katika daftari lolote, licha ya dawa hizo kulimbikizwa katika duka la Ofisi ya Wilaya ya Kusini, ambapo hadi ukaguzi unamalizika Disemba, 2023 hakuna hatua zozote zilizochukuliwa juu ya Dawa hizo.

Kuendelea kuwepo kwa Chanjo zilizokwisha muda wake wa matumizi kunaweza kukapelekea kuhatarisha maisha ya binadamu iwapo zitatolewa na zitatumika bila kujua muda wa matumizi ya dawa hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi kuhakikisha unafuatilia kwa karibu kutoka kwa Mamlaka inayohusika ili kupata kibali cha kuzitokomeza dozi 834 ya chanzo zinatolewa pamoja na kuanzisha daftari la kurekodi orodha za madawa yalikwisha pita muda wake wa matumizi pamoja na kutenga eneo maalum ya uwekaji wa madawa yaliyokwisha muda wa matumizi kwa binaadamu.

### Jadweli Nambari 31: Chanjo zilizokwisha muda wake ambazo hazijateketezwa

| Kipengele | Unit Dose | Tarehe yakumalizika muda wa matumizi |
|---|---|---|
| Chanjo ya MR | 410 | Septemba, 2023 |
| Chanjo ya Sinovac COVID 19 | 330 | Juni, 2023 |
| Chanjo ya Sinopharm COVID 19 | 94 | Agosti, 2023 |
| **Jumla** | **834** | |

*Chanzo: Madaftari ya Ghalani*

### 4.5.2.3 Ushuru wa Ongezeko la Thamani kwa miamala ya benki yenye thamani ya shilingi 1,216,542.41

Kifungu cha 15 cha GAVI Alliance na Mkataba wa Mfumo wa Ubia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Chanjo na msaada wa fedha taslimu wa 2013 kinasema kuwa "Fedha za GAVI zitakazotolewa chini ya Mkataba huu hazitatumika kulipa kodi, forodha, ushuru, tozo au nyinginezo, gharama zinazotozwa kwa uingizaji wa chanjo na vifaa vinavyohusika. Serikali itatumia juhudi zake za kuridhisha kuweka utaratibu ufaao wa kuondoa ushuru na kodi kwenye manunuzi yote yanayofanywa ndani na nje ya nchi kwa fedha za GAVI".

Ukaguzi ulipitia taarifa ya Kibenki za Mradi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 na kubaini kuwa EPI Zanzibar wana akaunti katika benki ya PBZ yenye Namba 0404440000 ambapo benki ya PBZ inatoza VAT ya shilingi 1,216,542.41 kwa kila muamala unaofanywa na IVD ambapo ni kinyume na nukuu iliyonukuliwa hapo juu. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi kuchukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha hakuna VAT inayolipwa kwa mujibu wa makubaliano kwa kutumia mfuko wa GAVI pamoja na kurejesha kiwango cha VAT cha shilingi 1,216,542.41 kilicholipwa kwa kila mwezi. Maelezo yanaonyeshwa kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 32: Kiwango cha VAT kilichotozwa kwa miamala ya Kibenki kwa kila mwezi**

| Mwezi | Kiasi cha VAT Kilichotozwa (Tsh) |
|---|---:|
| Julai | 77,035.32 |
| Agosti | 457.62 |
| Septemba | 167,980.26 |
| Oktoba | 19,723.69 |
| Novemba | 6,406.77 |
| Disemba | 591,429.91 |
| Januari | 210,605.14 |
| Februari | 21,100.49 |
| Machi | 67,291.82 |
| Aprili | 37,608.01 |
| Mei | 9,797.96 |
| Juni | 7,105.42 |
| **Jumla** | **1,216,542.41** |

*Chanzo: Taarifa ya fedha ya benki kuanzia Julai, 2022 hadi Juni, 2023*

#### 4.5.2.4 Matumizi yaliyofanywa bila kuzingatia matumizi ya Risiti za Kielektroniki (EFD) Shilingi 5,184,270

Kifungu nambari 23 (1) cha Sheria namba 7 ya Usimamizi wa Ushuru ya 2021 kinamtaka mtu anayesambaza bidhaa au kutoa huduma iwe kwa mkopo au pesa taslimu au anapokea malipo kuhusiana na bidhaa zinazotolewa au huduma iliyotolewa atatoa risiti ya kielektroniki kwa huduma. Aidha, barua yenye Kumb: Nam WN/ORFM/2022/VOL.V/20 ilitoa agizo la kuwataka wazabuni kuwasilisha stakabadhi za madai ya malipo (Invoice) na risiti kwa kutumia mashine za kielektroniki (EFD).

Ukaguzi uliofanyika katika Mradi wa IVD GAVI umebaini kuwa Mradi ulitumia shilingi 5,184,270 kwa ajili ya kutoa huduma mbalimbali bila kuzingatia matumizi ya risiti za kielektroniki kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 33: Matumizi yaliyofanywa bila kuzingatia matumizi ya risiti za Kielektroniki**

| Tarehe | Hati Namba | Ruzuku | Kiasi (Shs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 30/01/23 | V/HSS/01/14 | HSS | 1,959,020 | BHCL Contractor Co Ltd | Maitenance of Store |
| 25/05/23 | V/HSS/05/07 | | 3,225,250 | Alim Consultant | Quick Book |
| **Jumla** | | | **5,184,270** | | |

### 4.5.2.5 Ununuzi uliofanywa bila kutumia mfumo wa E-Proz shilingi 39,340,503.78

Kifungu nambari 5(1) (i) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza "kuanzisha na kusimamia mfumo wa manunuzi wa kielektroniki".

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (eGAZ) ilitoa taarifa kupitia barua yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.156/370/01/27 ya tarehe 12/8/2022 kuhusu Matumizi ya Mfumo wa Manunuzi wa Kielektroniki (e-PROZ) na kuzifahamisha taasisi zote za manunuzi za Serikali kutumia mfumo huo.

Ukaguzi umebaini kuwa manunuzi yaliyofanywa na Mradi wa IVD GAVI yenye thamani ya Shilingi 39,340,503.78 yamefanywa nje ya mfumo huo, jambo ambalo ni kinyume na kifungu nambari 5(1)(i) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mradi kuzingatia miongozo iliyotolewa kwa kuhakikisha manunuzi yote yanafanyika kwa mfumo wa kielektroniki wa Ununuzi wa Umma.

**Jadweli Nambari 34: Ununuzi uliofanywa bila kutumia mfumo wa e-Proz**

| Tarehe | Hati Namba | Aliyelipwa | Maelezo | Kiasi (Shs) |
|---|---|---|---|---|
| 30/01/23 | V/HSS/01/14 | BHCL Contractor Co Ltd | Maitenance Of Store | 1,959,020.00 |
| 24/1//23 | V/HSS/01/15 | New Home Furniture | Office Equipment | 980,000.00 |
| 24/01/23 | V/HSS/01/16 | Zan Printing | Stationary | 768,627.00 |
| 24/01/23 | V/HSS/01/17 | Zanzibar Petroleum Ltd | Fuel EPI Pemba | 6,000,000.00 |
| 24/06/23 | V/HSS/01/18 | Zanzibar Petroleum Ltd | Fuel EPI Unguja | 12,000,000.00 |

| Tarehe | Hati Namba | Aliyelipwa | Maelezo | Kiasi (Shs) |
|---|---|---|---|---|
| 30/01/23 | V/HSS/02/02 | Jawaja Auto Parts | Vehicle Mentenance | 865,340.00 |
| 30/01/23 | V/HSS/02/03 | Jawaja Auto Parts | Vehicle Mentenance | 1,702,206.00 |
| 30/01/23 | V/HSS/02/04 | Jawaja Auto Parts | Vehicle Mentenance | 1,110,340.00 |
| 22/03/23 | V/HSS/04/02 | Safia Shaibu Baki | Refreshment | 4,582,941.18 |
| 23/03/23 | V/HSS/04/03 | Safia Shaibu Baki | Refreshment | 759,019.60 |
| 10/05/23 | V/HSS/05/02 | Jawaja Auto Parts | Vehicle Mentenance | 2,655,800.00 |
| 12/05/23 | V/HSS/05/03 | Coolpro Refrigeration And Engineering | Maintanance | 931,960.00 |
| 28/04/23 | V/HSS/05/04 | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni | Venue | 600,000.00 |
| 28/04/23 | V/HSS/05/05 | ZSSF | Venue | 1,200,000.00 |
| 25/05/23 | V/HSS/05/07 | Alim Consultant | Quick Book | 3,225,250.00 |

### 4.5.2.6 Upotevu wa ziada wa chanjo za Rotavac

Ukaguzi ulifanya uhakiki wa upotevu wa chanjo za Rotavac nakubaini uwepo wa upotevu wa Chanjo hizo kutokana na kutokufuatwa kwa Sera ya Vial Multidose ya chupa moja kwa dozi tano.

Pia ,ukaguzi ulibaini sababu za upotevu wa chanjo ni kutokana na chanjo kutumia kiwango kidogo cha Multidose Vial Policy ambapo chanjo hiyo huisha muda wake wa matumizi kila baada ya saa Sita pindipo inapofunguliwa kwenye chupa yake.

Ukaguzi ulifanya ziara ya kutembelea maeneo ya Hospitali ya Wete na Chakechake - Pemba na kubaini uwepo wa upotevu wa chanjo ya Rotavac ya 7007 na dozi 2721 mfululizo kwa mwezi wa Januari, 2023 hadi Juni 2023 kama inavyoonyeshwa katika majadweli hapo chini.

Kuendelea kuharibika kwa chanjo kunaweza kukapelekea hasara kubwa ya kifedha na lengo la Serikali la kuhakikisha Chanjo zilizoagizwa zinatumika kama ilivyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi inaweka udhibiti mzuri wa uwagiziaji Chanjo mpya ya Rotavac ambayo zitamudu kukaa hadi siku 28 kutoka wakati wa ufunguzi wa chupa za chanjo pia kuhakikisha Wahudumu wa Afya wanapewa mafunzo kuhusu mbinu bora zaidi za kupunguza upotevu wa chanjo. Hali halisi ya upotevu wa Chanjo hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli zifuatazo:-

## Jadweli Nambari 35: Orodha ya Chanjo ya Rotavac ya Wilaya ya Wete Pemba kutoka Jan, 2023 hadi Juni, 2023

| Vifaa vya Afya | Jumla ya kipimo Chanjo | Jumla ya kipimo kilichowekwa | Upotevu wa jumla wa dozi | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Bwagamoyo PHCU | 435 | 685 | 250 | 36.50 |
| Chwale PHCU | 275 | 555 | 280 | 50.45 |
| Finya PHCU | 367 | 585 | 218 | 37.26 |
| Fundo PHCU+ | 325 | 510 | 185 | 36.27 |
| Jadida PHCU | 1360 | 2200 | 840 | 38.18 |
| Junguni PHCU | 554 | 865 | 311 | 35.95 |
| Kambini PHCU | 402 | 635 | 233 | 36.69 |
| Kangagani PHCU | 514 | 785 | 271 | 34.52 |
| Kinyasini PHCU | 584 | 960 | 376 | 39.17 |
| Kisiwani PHCU | 419 | 595 | 176 | 29.58 |
| Kiungoni PHCU | 1329 | 1940 | 611 | 31.49 |
| Kojani PHCU+ | 519 | 815 | 296 | 36.32 |
| Makongeni PHCU+ | 446 | 740 | 294 | 39.73 |
| Mzambarauni Takao PHCU | 329 | 650 | 321 | 49.38 |
| Minungwini PHCU | 683 | 1120 | 437 | 39.02 |
| Pandani PHCU | 655 | 1150 | 495 | 43.04 |
| Ukunjwi PHCU | 283 | 475 | 192 | 40.42 |
| Uondwe PHCU | 615 | 985 | 370 | 37.56 |
| Vumba PHCU | 555 | 855 | 300 | 35.09 |
| Wete District Hospital | 989 | 1540 | 551 | 35.78 |
| **Jumla** | **11638** | **18645** | **7007** | **37.58** |

*Chanzo: Taarifa kutoka DIVO*

## Jadweli Nambari 36: Data ya Chanjo ya Rotavac ya Wilaya ya Chake Chake Jan hadi Juni, 2023

| Vifaa vya Afya | Rota 1 | Rota 2 | Rota 3 | Jumla ya kipimo Chanjo | Jumla ya dozi zilizofunguliwa | Upotevu | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ali Khamis Camp (JWTZ) | 84 | 77 | 67 | 228 | 290 | 62 | 21.4 |
| Chakechake District Hospital | 506 | 418 | 325 | 1249 | 2940 | 1691 | 57.5 |
| Chonga PHCU | 244 | 210 | 141 | 595 | 610 | 15 | 2.5 |
| Gombani PHCU | 392 | 366 | 303 | 1061 | 1140 | 79 | 6.9 |
| JKU Wawi | 101 | 88 | 83 | 272 | 405 | 133 | 32.8 |
| Kibokoni PHCU | 50 | 33 | 34 | 117 | 170 | 53 | 31.2 |
| Mbuzini PHCU | 124 | 92 | 73 | 289 | 365 | 76 | 20.8 |
| Mgelema PHCU | 25 | 27 | 19 | 71 | 85 | 14 | 16.5 |
| Mvumoni (Furaha) PHCU | 92 | 59 | 42 | 193 | 240 | 47 | 19.6 |
| Ndagoni PHCU | 108 | 87 | 86 | 281 | 315 | 34 | 10.8 |
| Ngomeni PHCU | 10 | 9 | 7 | 26 | 35 | 9 | 25.7 |
| Ole PHCU | 112 | 95 | 68 | 275 | 285 | 10 | 3.5 |
| Pujini PHCU+ | 323 | 277 | 269 | 869 | 875 | 6 | 0.7 |
| SDA - Wawi Dispensary | 70 | 63 | 40 | 173 | 215 | 42 | 19.5 |
| Shungi PHCU | 59 | 65 | 52 | 176 | 175 | -1 | -0.6 |
| Tundauwa PHCU+ | 81 | 72 | 67 | 220 | 420 | 200 | 47.6 |
| Uwandani PHCU | 89 | 68 | 40 | 197 | 240 | 43 | 17.9 |
| Vikunguni PHCU | 67 | 49 | 32 | 148 | 160 | 12 | 7.5 |
| Vitongoji Cottage Hospital | 95 | 113 | 90 | 298 | 375 | 77 | 20.5 |
| Wesha PHCU+ | 69 | 52 | 59 | 180 | 210 | 30 | 14.3 |
| Ziwani PHCU | 100 | 95 | 71 | 266 | 355 | 89 | 25.1 |
| **Jumla** | **2801** | **2415** | **1968** | **7184** | **9905** | **2721** | **27.5** |

*Chanzo : Taarifa kutoka DIVO*

## 4.6 WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI

### 4.6.1 MRADI WA KUSAIDIA SEKTA YA UCHUKUZI -TSSP

Mradi wa Kusaidia Sekta ya Uchukuzi (TSSP) unajumuisha afua katika sekta ndogo za barabara, reli na anga nchini. Katika sekta ndogo ya barabara, afua hizo ni pamoja na:- (a) kazi za kiraia za ukarabati na uboreshaji wa baadhi ya kilomita 462 za barabara kwa kiwango cha lami Tanzania Bara na Zanzibar, (b) huduma za ushauri kuhusiana na kazi za barabara na masomo ya barabara; c) kujenga uwezo; (d) fidia na makazi mapya, na (e) Miundombinu ya kijamii.

**Malengo ya Mradi**

Lengo la mradi ni kuboresha miundombinu ya usafiri Zanzibar ili kupunguza gharama za uendeshaji wa magari na muda wa usafiri katika viunganishi vya barabara na kukuza ushirikiano wa kikanda kwa kuboresha huduma za usafiri.

**Ufadhili wa Mradi**

Mradi huu unafadhiliwa kupitia ADB, ADF kwa Dola za Kimarekani milioni 270.95 na UA milioni 54 mtawalia na mchango wa Serikali ambao ni sawa na UA milioni 28.48 ambapo Mradi huu ulifungwa mkataba Novemba, 2015 na kuanza kutumika tarehe 27 Mei, 2016.

**Vipengele vya Mradi**

Mradi huu unahusika na ulipaji wa fidia kwa watu walioathirika na ukarabati wa barabara za lami kilomita 31 (Bububu-Mahonda-Mkokotoni) na kuboresha ukarabati wa barabara kiwango cha lami kilomita 21 katika maeneo ya Pale-Kiongele, Matemwe-Muyuni na Fuoni-Kombeni.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.6.1.1 Kuchelewa kuwasilishwa kwa Rasimu ya Mkataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Kanuni ya 47(1)(2) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2020 inataka makubaliano yoyote yanayohusiana na manunuzi ambayo thamani yake ni kubwa kwa mujibu wa njia za manunuzi au kiwango cha juu yatathibitishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa na wahusika. Afisa Masuuli, ndani ya siku saba (7) baada ya kutoa uamuzi, atawasilisha kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali rasimu ya mkataba ili kuthibitishwa.

Wakati wa ukaguzi katika mradi wa TSSP kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023. Mradi wa TSSP uliingia mkataba wa Ujenzi wa Bwalo la Chakula Kinyasini-Kaskazini 'A' ambapo ukaguzi ulibaini uwepo wa ucheleweshaji wa kuwasilisha rasimu ya mkataba kwa Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa na wahusika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa TSSP uhakikishe kuwa rasimu za Mikataba zinawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu ndani ya siku 7 baada ya kusainiwa na Wahusika. Maelezo ya mikataba ni kama inavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 37: Kuchelewa Kuwasilishwa kwa Rasimu ya Mkataba kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

| Rejea za Mkataba | Maelezo | Tarehe ya Tuzo | Tarehe iliyowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu | Idadi ya siku zilizocheleweshwa |
|---|---|---|---|---|
| SMZ/P01/W/NCB/2020-21/29 | Ujenzi Unaopendekezwa wa Jengo la Bwalo la Chakula katika Halmashauri ya Wilaya ya Kinyasini-Kaskazini 'A' | 20/05/ 2022 | 21/06/2022 | Siku 25 |

## 4.6.2 MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII TANZANIA (TASAF)

Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) unafadhiliwa na Benki ya Dunia (IDA), Ubalozi wa Norway, Ubalozi wa Ireland, Ubalozi wa Uswisi, SIDA, Bill & Melinda Gate Foundation (BMGF), FSDT, TACAIDS, ILO, UNICEF na UN-Women and Government.

Mradi huu ulitarajiwa kutekelezwa kwa muda wa miaka mitatu kuanzia Aprili, 2020 hadi 30 Septemba, 2023 ambapo umetengewa jumla ya fedha USD milioni 883.3 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za TASAF kwa Unguja na Pemba.

### Malengo ya Mradi

Lengo kuu la Mradi wa PSSN II ni kuboresha upatikanaji wa fursa za mapato na huduma za kijamii na kiuchumi kwa kaya zinazolengwa huku ikiimarisha na kulinda rasilimali watu na watoto wao.

### Walengwa wa Mradi

Programu ya PSSN II inafanya kazi kitaifa ikijumuisha Mamlaka za Maeneo ya Miradi 186 (PAAs) Tanzania Bara na Zanzibar. PSSN II inaendelea kulenga Kaya masikini zaidi na zilizo hatarini zaidi katika Vijiji, Mitaa na Shehia.

### Fedha za mradi

Mradi wa TASAF unapata Mkopo kutoka Shirika la Kimataifa la Maendeleo (IDA) na ruzuku kutoka Ubalozi wa Norway, Ubalozi wa Ireland, Ubalozi wa Uswisi, SIDA, FSDT, BMGF pamoja na Serikali ya Tanzania (GoT) ambapo Serikali ya Tanzania ilikubali kuchangia jumla ya USD Milioni 14 kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba uliotiwa saini tarehe 7 Oktoba, 2019.

### Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi

### 4.6.2.1 Malipo yasiyofanikiwa kwa walengwa kupitia mfumo wa malipo ya kielektroniki shilingi 52,115,000

Kifungu cha 56 cha Hati ya Tathmini ya Mradi (PAD) kinaeleza kwamba chini ya PSSN II, TASAF itakuwa na mabadiliko ya taratibu kutoka mfumo wa sasa wa malipo ya fedha taslimu kwenda malipo ya kielektroniki.

Ukaguzi ulipitia orodha ya malipo ya fedha zilizohamishwa kwa wanufaika wa Kaya Maskini kupitia mfumo wa kielektroniki na kubaini jumla ya shilingi 52,115,000 hazikuweza kupokewa kwa walengwa ambao fedha zao zilihamishiwa kupitia Tigo pesa, Mpesa na Airtel Money kutokana na sababu mbalimbali. Hali hii imesababisha wanufaika kuchelewa kupata fedha zao kwa muda uliopangwa na kupelekea kuvuruga mipango yao ya maendeleo na kuongeza malalamiko ya walengwa katika utekelezaji wa mpango huo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa TASAF kufanya usimamizi wa karibu katika ngazi ya PAA kwa kuhakikisha kuwa, changamoto zilizotajwa hapo juu zinatatuliwa kwa kushirikiana na NIDA na wadau wengine wa programu. Orodha ya Malipo ya kaya ambayo hayajawafikia walengwa kupitia mfumo wa malipo ya kielektroniki kwa upande wa Unguja ni kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 38: Fedha zilizohamishwa bila ya kuwafikia walengwa

| Kipindi cha Malipo | Shehia | Idadi ya Wanufaika | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| **Jan -Feb, 2023** | Charawe | 9 | 180,000 |
| | Donge Pwani | 58 | 7,855,000 |
| | Kibondeni | 34 | 640,000 |
| | Kijini Matemwe | 23 | 967,000 |
| | Kiungani | 44 | 3,808,000 |
| | Kizimkazi Mkunguni | 3 | 214,000 |
| | Magomeni | 8 | 86,000 |
| | Mgambo | 4 | 286,000 |
| | Migombani | 20 | 1,501,000 |
| | Mlandege | 6 | 460,000 |
| | Nungwi Banda Kuu | 57 | 4,542,000 |
| | Paje | 21 | 1,442,000 |
| | Uzi | 5 | 212,000 |
| **Mei - Juni, 2023** | Charawe | 9 | 180,000 |
| | Donge Pwani | 107 | 9,956,000 |
| | Kibondeni | 59 | 1,474,000 |
| | Kijini Matemwe | 26 | 308,000 |
| | Kiungani | 86 | 8,368,000 |
| | Magomeni | 7 | 182,000 |
| | Mgambo | 5 | 62,000 |
| | Mlandege | 6 | 484,000 |
| | Nungwi Banda Kuu | 74 | 5,992,000 |
| | Paje | 39 | 2684,000 |
| | Uzi | 6 | 232,000 |
| | **Jumla** | | **52,115,000** |

### 4.6.2.2 Fedha zisizokusanywa na kaya shilingi 185,240,100

Ukaguzi ulipitia hati mbali mbali zikiwemo hati za malipo, karatasi za malipo, fomu za usuluhishi na ripoti ya malipo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kubaini jumla ya shilingi 185,240,100 hazikukusanywa na wanufaika wakati wa malipo kwa Unguja PAA na Pemba PAA.

Kutokupokelewa kwa fedha na wanufaika wa Kaya kulichangiwa na utoro wa baadhi ya wanufaika na kutolingana kati ya jina la walengwa na nambari ya PSSN, hali iliyosabibisha fedha zinazohusika kuhamishiwa Makao Makuu ya TASAF.

Kutokusanywa kwa hazina ya Wanufaika wa Kaya kunazuia juhudi za Serikali katika kuboresha hali ya maisha ya Kaya.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuchunguza suala hilo na kuhakikisha kwamba malipo ya fedha ambazo hazijapokelewa kwawalengwa yanafanywa katika dirisha la malipo linalofuata. Fedha ambazo hazijakusanywa ni kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 39: Fedha zisizokusanywa na kaya Unguja PAA

| Mwezi | Kiasi kilicholipwa kwa Kaya (Tshs) | Kiasi kilichokusanywa na Kaya (Tshs) | Kiasi kisichokusanywa na Kaya (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Mei - Juni, 2022 | 517,878,875 | 446,034,060 | 10,938,000 |
| Julai - Agosti, 2022 | 818,934,261 | 802,228,261 | 16,706,000 |
| Septemba - Oktoba,2022 | 622,102,972 | 588,493,972 | 33,609,000 |
| Novemba– Disemba,2022 | 419,949,260 | 410,956,160 | 8,993,100 |
| Januari – Februari, 2023 | 410,664,609 | 406,079,609 | 4,585,000 |
| **Jumla** | **2,789,529,977** | **2,653,792,062** | **74,831,100** |

*Chanzo: Data za Mishahara na ripoti za usuluhishi wa Benki kwa mwaka 2022/2023*

Aidha, kwa upande wa Pemba PAA fedha ambazo hazijakusanywa ni shilingi 110,399,000 ambapo fedha hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 40: Pemba PAA Fedha zisizokusanywa

| Mwezi | Kiasi kilicholipwa kwa Kaya (Tshs) | Kiasi kilichokusanywa na Kaya (Tshs) | Kiasi kisichokusanywa na Kaya (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Mei - Juni, 2022 | 604,804,000 | 628,480,000 | 23,676,000 |
| Julai - Agosti, 2022 | 946,168,000 | 976,492,000 | 30,324,000 |
| Septemba - Oktoba 2022 | 773,204,000 | 819,844,000 | 46,640,000 |
| Novemba - Disemba,2022 | 436,280,233 | 441,864,233 | 5,584,000 |
| Januari - Februari 2023 | 752,806,000 | 756,981,000 | 4,175,000 |
| **Jumla** | **3,513,262,233** | **3,623,661,233** | **110,399,000** |

*Chanzo: Data za Mishahara na ripoti za usuluhishi wa Benki kwa mwaka 2022/2023*

#### 4.6.2.3 Kuchelewa kwa TMU kuhamisha Mfuko wa Walengwa wa CCT kwenda Unguja PAA shilingi 6,557,109,722

Mwongozo wa Uendeshaji wa TASAF III PSSN II unahitaji mfumo madhubuti wa usimamizi wa fedha kwa ajili ya utekelezaji bora wa programu na kwa ajili ya kuhakikisha uwajibikaji wa programu.

Mapitio ya mfuko uliopokelewa Unguja na Pemba PAA, ukaguzi umebaini uwepo wa wanufaika ambao hawakupata fedha kwa wakati kutokana na fedha hizo hazikulipwa kwa mujibu wa kalenda ya walengwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa TASAF kuhakikisha fedha inatolewa kwa wakati kwa walengwa. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama inavyoonyeshwa katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 41: Kuchelewa kuhamisha mfuko wa Walengwa kwenda Unguja PAA**

| Muda | Tarehe ya upokeaji fedha kwa PAA | Kiasi (TSh.) | Idadi ya siku zilizochelewa |
|---|---|---|---|
| Mei- Juni, 2022 | 23/7/2022 | 517,878,875 | 83 |
| Julai – Agosti, 2022 | 8/9/2022 | 818,934,261 | 69 |
| Septemba – Oktoba, 2022 | 7/11/2022 | 622,102,972 | 67 |
| Novemba – Disemba, 2022 | 2/2/2023 | 419,949,260 | 93 |
| Januari – Febuari, 2023 | 31/5/2023 | 410,664,609 | 150 |
| **Jumla** | | **2,789,529,977** | |

*Chanzo: Daftari Kuu la fedha na Taarifa za Fedha za Benki*

**Jadweli Nambari 42: Kuchelewa kuhamisha mfuko wa Walengwa kwenda Pemba PAA**

| Muda | Tarehe ya upokeaji fedha kwa PAA | Kiasi (Shs) | Idadi ya siku zilizochelewa |
|---|---|---|---|
| Mei- Juni, 2022 | 23.07.2022 | 666,330,170 | 83 |
| Julai – Agost, 2022 | 06.09.2022 | 1,029,510,171 | 69 |
| Sept – Oktoba, 2022 | 07.11.2022 | 872,894,171 | 67 |
| Nov – Disemba, 2022 | 06.02.2023 | 441,864,233 | 93 |
| Jan – Febuari, 2023 | 02.06.2023 | 756,981,000 | 150 |
| **Jumla** | | **3,767,579,745** | |

*Chanzo: Daftari Kuu la fedha na Taarifa za Fedha za Benki*

#### 4.6.2.4 Kutokamilika kwa ujenzi wa kituo cha Afya katika Shehia ya Uzi

Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Miundombinu ni moja ya vipengele vya Mpango wa Kusaidia Kaya Maskini, kwa lengo la kuchangia au kuimarisha utekelezaji wa miradi ya ujenzi katika sekta ya Afya, Elimu, na Maji, kwa mtazamo na matarajio ya kuwezesha upatikanaji wa huduma muhimu kwa jamii zenye uhitaji mkubwa wa huduma hizo.

Pamoja na kuwezesha upatikanaji wa huduma muhimu za jamii, utekelezaji wa miradi hii ya ujenzi unalenga kuhakikisha kuwa kaya zinazolengwa zinakidhi mahitaji ya elimu na afya.

Ukaguzi umebaini Mradi wa TASAF ulitekeleza ujenzi wa kituo cha afya katika Shehia ya Uzi kuanzia tarehe 28 Agosti, 2022 kwa thamani ya shilingi 288,416,626 na kukamilika kwake hadi tarehe 31 Agosti, 2023 ambapo Mradi huo ulikuwa umefikia asilimia 88. Aidha, ukaguzi umebaini fedha za utekelezaji wa mradi huo zilikwisha kabla ya kukamilika jambo ambalo limeibuwa wasiwasi kuhusu kushindwa kwa mradi kufikia malengo yake. Upangaji duni wa bajeti na usimamizi wa fedha unaweza kuwa umesababisha kupungua mapema kwa fedha za mradi, kushindwa kukamilika kwa mradi huo kunahatarisha upatikanaji wa kituo hicho muhimu cha afya kwa wakati, ambacho kilikusudiwa kunufaisha jamii.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi kuhakikisha kwamba kunakuwa na fedha ya kutosha katika utekelezaji wa miradi ili huduma iliyokusudiwa na Serikali inafikiwa katika jamii kwa wakati.

## 4.7 WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

### 4.7.1 MRADI WA USIMAMIZI WA UVUVI NA UKUAJI WA PAMOJA KUSINI MAGHARIBI MWA BAHARI YA HINDI (SWIOFish)

Mradi wa SWIOFish ni programu ya awamu 3 ya miaka 15 ambayo inasaidia ushirikiano wa kikanda wa usimamizi wa uvuvi. Mkataba wa ufadhili wa mradi kati ya Benki ya Maendeleo ya Kimataifa (Benki ya Dunia) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ulitiwa saini tarehe 12 Machi, 2015. Mradi wa SWIOFish ulitangazwa rasmi kuanza kutumika tarehe 22 Juni, 2015.

**Lengo la Mradi**

Lengo kuu la mradi wa SWIOFish ni kuongeza faida endelevu za kiuchumi zinazotokana na uvuvi wa baharini ambapo kwa awamu ya kwanza ulikuwa na lengo la kuboresha ufanisi wa usimamizi kwa kuchaguliwa kwa kipaombele cha uvuvi katika ngazi ya kikanda, kitaifa na jamii.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 4.7.1.1 Fedha ambazo hazikupatikana katika utekelezaji wa Miradi USD 1,470,982

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Mradi wa SWIOFish ilitakiwa kupokea jumla ya USD 11,520,000 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Mradi kwa muda wa miaka saba (7) kuazia kipindi cha mwaka 2015 hadi 2022.

Ukaguzi umebaini Mradi ndani ya kipindi hicho uliweza kupokea jumla ya Dola 10,049,018 na kupelekea upungufu wa jumla ya Dola 1,470,982 kiasi ambacho hakikuweza kupatikana kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa mujibu wa makubaliano.

Kutokupatikana kwa kiasi hicho cha fedha kunaweza kukapelekea baadhi ya shughuli za mradi kutokufanyika au kutokumalizika kwa wakati au kutokupatikana kwa huduma iliyokusudiwa kwa maendeleo ya jamii.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mradi kuhakikisha kwamba fedha za utekelezaji wa mradi zinapatikana kwa mujibu wa makubaliano.

## 4.7.2 MRADI WA MPANGO WA CHAKULA KATIKA SKULI ZA MSINGI

Mpango wa chakula katika Skuli za Msingi ni utoaji wa chakula chenye lishe kwa wanafunzi wakati wakiwa Skuli. Kwa upande wa Zanzibar, mradi unaendelea ikiwa ni mwanzo wa awamu ya tatu ambayo itadumu kwa muda wa miaka mitatu (kuanzia 2020/2021 hadi 2022/2023).

Awamu hii imepangwa kuwahudumikia wanafunzi 13,000 katika skuli ishirini na saba (27) katika Wilaya saba Unguja na Pemba. Hata hivyo, idadi halisi ya wanafunzi hivi sasa katika skuli hizo ni 14,751.

Awamu ya kwanza ya majaribio ya mwaka mmoja, 2014 ilihudumikia wanafunzi 5,255 katika skuli tisa Unguja na Pemba (skuli 5 Wilaya ya Kaskazini ‘A’ na skuli 4 Wilaya ya Micheweni).

Awamu ya pili mwaka 2016, mradi ulianza na skuli tisa kama ilivyokuwa wakati wa majaribio. Mwaka 2017, iliongezeka skuli ya Mgonjoni kutoka Wilaya ya Kaskazini ‘B’ na baadaye Agosti 2018, skuli kumi na saba (17) kutoka Wilaya saba za Unguja na Pemba ziliongezwa na kufikia jumla ya skuli 27 ambazo zinaendelea na mradi hadi hivi sasa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 4.7.2.1 Malipo yaliyofanywa kwa watu binafsi badala ya kikundi cha ushirika jumla ya USD 8,309.80

Ukaguzi ulipitia malipo yaliyolipwa katika vikundi vinavyotowa huduma katika Mradi wa utoaji wa chakula katika Skuli za Msingi kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/23 na kubaini jumla ya USD 8,309.80 zililipwa kinyume na makubaliano ambapo fedha hizo zilikuwa zilipwe kupitia Hesabu za vikundi hivyo na badala yake fedha hiyo ililipwa kupitia wananchama mmoja mmoja wa kikundi, hali ambayo ukaguzi umetia shaka juu ya njia za malipo zilizotumika ambapo zinaweza kupelekea uwepo udanganyifu wa matumizi ya fedha za mradi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mradi kuhakikisha malipo yote yanalipwa kwa mujibu wa makubaliano kwa kutumia akaunti ya vikundi vilivyosajiliwa na sio akaunti ya mtu binafsi. Jadweli hapo chini linaonyesha kiasi kilicholipwa kwa akaunti binafsi kama ifuatavyo:-

**Jadweli Nambari 43: Malipo ya mradi yaliyofanywa kwa watu binafsi**

| Namba | Aliyelipwa | Kiasi kilicholipwa (USD) |
|---|---|---|
| 1. | Amour Haji Ramadhani | 186.22 |
| 2. | Islah Faki Kona | 123.87 |
| 3. | Ally Hassan Haji | 197.35 |
| 4. | Islah Faki Kona | 491.30 |
| 5. | Ally Hassan Haji | 229.32 |
| 6. | Hassan Said Mzee | 1,084.21 |
| 7. | Ally Hassan Haji | 203.92 |
| 8. | Ally Hassan Haji | 247.95 |
| 9. | Ally Hassan Haji | 172.26 |
| 10. | Aley Suleiman Abdalla | 490.77 |
| 11. | Aley Suleiman Abdalla | 1,218.56 |
| 12. | Faki Hija Foum | 640.99 |
| 13. | Amour Haji Ramadhan | 247.35 |
| 14. | Islah Faki Kona | 292.06 |
| 15. | Aley Suleiman Abdalla | 570.40 |
| 16. | Faki Haji Foum | 272.80 |
| 17. | Amour Haji Ramadhani | 91.63 |
| 18. | Aley Suleiman Abdalla | 1,548.84 |
| **Jumla** | | **8,309.80** |

# SURA YA TANO



# 5.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTEKELEZWA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA PEMBA

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inatoa maelezo kuhusiana na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa Pemba ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa Bustani Mwanamashungi na Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga Machomanne iliyotekelezwa na Baraza la Manispaa Chake Chake, pamoja na Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga Mtambile uliotekelezwa na Baraza la Mji Mkoani. Aidha, sura hii imetoa ufafanuzi wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi uliotekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni.

Katika tathmini iliyofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwa kiasi kikubwa miradi inayotekelezwa inakiuka taratibu za ufungaji wa hesabu jambo ambalo linapelekea ugumu wa kufanya tathmini ya hati ya ukaguzi inayopaswa kutolewa kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo.

### 5.1.1 MRADI WA UJENZI WA SOKO LA SAMAKI NA MBOGAMBOGA MTAMBILE

Lengo la Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mboga mboga Mtambile ni kuwawekea wananchi mazingira mazuri ya upatikanaji wa huduma za kijamii na pia kutanua wigo wa ajira kwa wajasiriamali.

Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mboga mboga Mtambile umejumuisha milango ya maduka 10 vikuta/vibaraza 17 kwa ajili ya wafanyabiashara wa samaki na mboga mboga, mabucha 3 kwa ajili ya wafanyabiashara wa nyama, sehemu ya kusalia pamoja na mgahawa kwa lengo la kuzingatia huduma za jamii. Aidha, mradi huu umejumuisha vyoo 10 ambavyo vimezingatia mahitaji ya jinsia na watu wenye mahitaji maalum.

Katika utekelezaji wa mradi huo uligawika katika vipengele vitatu vikuu ambavyo ni Ukataji wa Mlima, Land Scaping na Ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga.

**KIPENGELE NAMBARI 1: UJENZI WA SOKO LA SAMAKI NA MBOGAMBOGA**

Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga Mtambile unafadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Baraza la Mji Mkoani. Mradi huo una thamani ya shilingi 588,963,760 pamoja na VAT kwa mujibu wa mkataba.

Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mradi wa Ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga ulitumia jumla ya shilingi 164,909,861 sawa na asilimia 28 ya fedha za jumla ya mradi, na hivyo kubakiza shilingi 424,053,899 sawa na asilimia 72 ya thamani ya mradi.

Mradi huu unatekelezwa na Baraza la Mji Mkoani likiwa kama mwajiri na Wakala wa Majengo Pemba akisimama kama mshauri elekezi. Baraza liliingia katika makubaliano ya mkataba namba SMZ/PD74/W/OQ/2022-2023/19 na Mkandarasi anaejulikana kwa jina la Ghase Investment Co. Ltd mnamo tarehe 28/12/2022. Mkataba huo wa ujenzi wa Soko la Samaki na Mboga mboga la Mtambile unaligharimu Baraza jumla ya shilingi 588,963,760 pamoja na VAT. Ujenzi wa mradi huu ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 6 kuanzia tarehe 15 Disemba, 2022 hadi 30 Juni, 2023.

**Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa Mradi:**

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 uliweza kubaini dosari mbali mbali katika utekelezaji wa ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga uliosimamiwa na Baraza la Mji Mkoani ambapo miongoni mwa dosari hizo ni kama zifuatazo:-

(a) Baraza lilishindwa kutangaza zabuni kupitia vyombo mbali mbali vya habari ili kuweza kutoa fursa kwa wazabuni mbali mbali kuomba zabuni hiyo kinyume na vifungu nambari 38 na 68 vya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

(b) Kukosekana kwa mihutasari ya vikao vya bodi ya zabuni iliyopitisha mradi pamoja na kile cha kumthibitisha Mkandarasi aliyeteuliwa na kamati ya tathmini kinyume na kifungu nambari 39 cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

(c) Kukosekana kwa nyaraka zinazoonyesha mchakato mzima wa kumpata mzabuni kinyume na kifungu nambari 35 (2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

(d) Kukosekana kwa muhutasari wa kikao cha kabla ya zabuni (Pre-bid meeting) kinyume na kifungu nambari 32(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

(e) Kukosekana kwa barua ya ruhusa kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma iliyoruhusu kufanyika kwa ununuzi huu pasipo kutangaza zabuni.

(f) Kukosekana kwa ripoti ya utekelezaji wa mradi.

(g) Kukosekana kwa ripoti ya kitaalamu baada ya kukabidhiwa mradi.

(h) Kukosekana kwa ripoti ya upembuzi yakinifu kinyume na kifungu nambari 2.3 cha Mwongozo wa Upangaji wa Miradi na Majadiliano ya Kuongeza Mikopo, Kutoa Dhamana na Kupokea Ruzuku ya Novemba, 2020.

(i) Kukosekana kwa hati ya dhamana ya mradi kinyume na Kanuni nambari 29(4) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma za mwaka 2020.

Uwepo wa dosari katika utekelezji wa mradi kunapelekea uwezekano wa Baraza kuingia katika miradi isiyo na tija kwa jamii iliyozunguka pamoja na Serikali kwa ujumla na pia hupelekea kutekelezwa mradi chini ya kiwango.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza kuhakikisha wanafuata taratibu zote za utekelezaji wa mradi kwa kufuata kikamilifu Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali ili kuepusha kutekelezwa kwa miradi isio na tija au utekelezaji wa miradi chini ya kiwango na hivyo kuitia hasara Serikali.

#### 5.1.1.1 Kukosekana kwa makisio ya siri ya mradi kutoka kwa Mhandisi wa Baraza (Confidential Engineering Estimate)

Katika utaratibu wa kawaida Mkadiriaji (Quarity Surveyor) majengo wa taasisi inayotakiwa kufanyiwa kazi ya ujenzi anatakiwa atayarishe makisio ya siri ya gharama za ujenzi (Confidential Engineering Estimate) kwa ajili ya kutoa mwelekeo wa bajeti ya mradi.

Katika kupitia kumbukumbu mbali mbali za mradi ukaguzi umeshindwa kuona makisio hayo yaliyoandaliwa na Mhandisi kutoka Afisi ya Baraza la Mji Mkoani ili iweze kuwa muongozo katika kuandaa bajeti kamili ya mradi, kuweza kulinganisha bei na pia kuweza kuweka mipango madhubuti inayohusu mradi. Aidha, ukaguzi uliona na kupitia makisio ya gharama za ujenzi (BoQs) iliyojazwa na Mkandarasi M/S Ghase Investiment Co. Ltd pekee.

Kutokuandaliwa kwa makisio ya siri ya gharama za ujenzi yaliyojazwa kutoka Afisi ya Baraza kunaweza kupelekea kushindwa kutambua bajeti sahihi ya mradi na pia kukosa nyenzo sahihi ya kumfanyia tathmini Mkandarasi aliyeshinda zabuni kwa kulinganisha bei ya vitu au bei ya kazi kwa jumla.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kuwa unajaza makisio ya siri ya gharama za ujenzi kwa miradi inayoendelea ili kuwepo kwa uwazi, mlinganisho wa gharama za mradi na mipangilio mizuri ya bajeti ya mradi ili kuepusha kukwama kwa mradi kwa kukosa mipango madhubuti ya awali.

#### 5.1.1.2 Kufanyika kwa kazi ambazo hazikuanishwa kwenye mkataba wa ujenzi

Baada ya kupitia kumbukumbu mbali mbali za mradi pamoja na kutembelea eneo la utekelezaji wa mradi wa soko la samaki na Mbogamboga Mtambile ukaguzi umebaini uwepo wa baadhi ya kazi ambazo zimefanywa na mkandarasi bila ya kuanishwa kwenye makisio ya gharama za ujenzi (BoQs) iliyofungamanishwa na mkataba. Aidha, ukaguzi umeshindwa kuona muhutasari wa kikao kilichopitisha na kuidhinisha kazi hizo kama nyongeza za kazi ili kujiridhisha juu ya uhalali wa kazi hizo. Mchanganuo wa kazi ambazo hazikuanishwa kwenye nyaraka za mkataba ni kama zifuatazo: -

a) Uwekaji umeme na vifaa vyake (Electric Installation and Wiring) uliogharimu shilingi 14,473,000

b) Uwekaji wa mfumo wa maji taka sehemu za kuuzia samaki (Drainage system) wenye urefu wa futi 127 ambazo mkaguzi alishindwa kujua gharama zake.

c) Uwekaji wa matofali 85 yalowekwa rangi (Decorated block) nje ya soko.

Kufanyika kwa kazi ambazo hazikuainishwa katika mkataba na ambazo hazijaidhinishwa na uongozi wa Baraza kunaweza kupelekea kulipwa kwa fedha ambazo hazimo kwenye makubaliano au kunaweza kupelekea migogoro ya madeni baina ya mkandarasi na Afisi ya Baraza la Mji Mkoani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kuwa wanasimamia mikataba yote ili kuepusha malipo ambayo hayakutarajiwa na wala hayamo kwenye makubaliano na pia kuepusha baadhi ya migogoro ya madeni yanayoweza kujitokeza.

#### 5.1.1.3 Kukosekana kwa nyaraka za umiliki wa eneo linalotekelezwa mradi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Baraza la Mji Mkoani halina nyaraka zinazoonyesha umiliki wa eneo linalotekelezwa mradi wa ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga lililopo Mtambile, hali inayopelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha umiliki halali wa eneo linalotekelezwa mradi huo.

Kutokuwepo kwa nyaraka zinazothibitisha umiliki halali wa eneo hilo kuwa ni mali ya Baraza kunaweza kupelekea kutokea kwa migogoro baina ya Baraza na wananchi pamoja na kupelekea upotevu wa mali hizo kwa kujimilikisha watu wengine bila ya ruhusa ya Baraza.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha wanachukua juhudi za makusudi za kuzitafutia nyaraka mali zote za kudumu ikiwemo eneo la kiwanja cha soko la samaki na Mbogamboga lililopo Mtambile ili kujikinga na migogoro inayoweza kujitokeza.

### 5.1.1.4 Kukosekana kwa ripoti ya Mkaguzi wa Ndani

Kwa mujibu wa kifungu nambari 117(5) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 inaeleza kwamba "Katika kutekeleza majukumu yao, wakaguzi wa ndani watatoa kwa maandishi taarifa za ukaguzi wa ndani pamoja na mapendekezo kwa Maafisa Wahasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Mkoani hawakuandaa taarifa za ukaguzi wa ndani zinazohusu mradi wa ujenzi wa soko la Mtambile.

Kukosekana kwa taarifa ya Mkaguzi wa ndani kunaweza kupelekea kutokubainika mapema kwa vihatarishi (Risk) pamoja na dosari mbali mbali za utekelezaji wa mradi ambavyo vinaweza kupelekea ucheleweshaji wa mradi pamoja na ukiukwaji wa sheria mbali mbali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kuwa Mkaguzi wa Ndani anakagua na kutoa ripoti kwa kazi zote zinazohusiana na Baraza ikiwemo kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

### 5.1.1.5 Kukosekana kwa cheti cha tathmini ya athari ya mazingira

Kwa mujibu wa kifungu nambari 39 cha Sheria nambari 2 ya Usimamizi wa Mazingira ya 1996 kinamtaka mtu yeyote anayetaka kufanya shughuli za ujenzi kuhakikisha anapata cheti cha tathmini ya athari ya mazingira kutoka Mamlaka kabla ya kuanza kwa shughuli husika.

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Mji Mkoani limeanzisha ujenzi wa soko la Samaki na Mbogamboga katika eneo la Mtambile bila ya kupata cheti cha tathmini ya athari ya mazingira kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira. Kufanya shughuli ya ujenzi bila ya eneo kutathminiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira na kupata cheti kinachoruhusu ujenzi kunaweza kupelekea kutokea kwa majanga yasiyotegemewa na pia ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii imesababishwa na uongozi wa Baraza kutokufuata Sheria na taratibu zinazohusiana na utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kuwa unafuata taratibu zote za utekelezaji wa miradi ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya athari za mazingira kabla ya kuanza ujenzi wa miradi ili kuepukana na athari zinazoweza kujitokeza.

#### 5.1.1.6 Kukosekana kwa ripoti ya tathmini ya ulipwaji wa fidia

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inaeleza kuwa Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Baraza la Mji Mkoani limewalipa fidia wananchi waliotoa maeneo yao kwa ajili ya kupisha ujenzi wa soko la Samaki na Mbogamboga lililopo katika eneo la Mtambile kwa hati namba 211PV24000053 ya tarehe 18/08/2023 yenye thamani ya shilingi 6,000,000 iliyolipwa kwa Meneja wa Benki ya Watu wa Zanzibar ikiwa ni malipo ya awamu ya mwanzo ya fidia kwa watu waliopisha ujenzi wa soko la Mtambile.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwalipa wananchi hao bila ya kuwepo ripoti ya tathmini ya mali zao kutoka Mamlaka husika hivyo ukaguzi kushindwa kuthibitisha juu ya uhalali wa malipo hayo. Ulipaji wa fidia bila ya kuwepo kwa nyaraka kamilifu kunaweza kupelekea kulipwa mwananchi asiyekuwa na sifa au kulipwa zaidi ya kiwango anachostahiki. Kufanya malipo bila ya kuambatanisha nyaraka kamili ni kwenda kinyume na kanuni iliyonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha kuwa vielelezo vyote vya malipo vinaambatanishwa katika hati za malipo kwa wakati.

#### 5.1.1.7 Kutokuandaa na kuwasilisha kwa hesabu za utekelezaji wa Mradi

Kwa mujibu wa kifungu namba 119(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, zinatakiwa Taasisi za Umma ziandae na ziwasilishe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba Baraza la Mji Mkoani halikuandaa wala kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi ya utekelezaji wa mardi wa maendeleo wa ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga la Mtambile, jambo ambalo limepelekea kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kwa mujibu wa utaratibu.

Kutokuandaa na kuwasilisha kwa taarifa za hesabu ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha unaandaa na kuwasilisha taarifa za hesabu zinazohusiana na utekelezaji wa miradi ili kuweza kutoa maoni ya ukaguzi juu ya hali ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**KIPENGELE NAMBARI 2: UKATAJI WA MLIMA**

Kipengele hiki kilikuwa na dhumuni la ukataji wa mlima ili kuweza kurahisha mandhari ya utekelezaji wa ujenzi wa Soko la Samaki na Mbogamboga kwa engo la kuwaekea wananchi mazingira mazuri ya upatikanaji wa huduma za kijamii karibu na maeneo yao na pia kutanua wigo wa ajira kwa wajasiriamali.

Katika utekelezaji huo Baraza la Mji Mkoani lilisaini hati ya makubaliano ya utekelezaji wa mradi huo yenye kumbukumbu nambari SMZ/PD74/W/OQ/2021-2022/22 ya tarehe 06/05/2022 baina ya Baraza na Mzabuni Talib Mohammed Said kwa thamani ya shilingi 75,417,000 pamoja na VAT kukiwa na makubaliano ya kukamilika kazi hiyo ndani ya kipindi cha miezi 12.

Ukaguzi ulifanya tathmini ya kina ili kuweza kujua thamani halisi ya fedha iliyotumika na hatua ya utekelezaji wa mradi ambapo ilibainika hadi kufika tarehe 30 Juni 2023, Mradi ulitumia shilingi 68,379,430 sawa na asilimia 90.67 ya fedha jumla ya mkataba hivyo kubakiza shilingi 7,037,570 sawa na asilimia 9.33 ya thamani jumla ya mkataba. Pamoja na matumizi hayo ya fedha ukaguzi umebaini uwepo wa dosari ifuatayo: -

### 5.1.1.8 Kukosekana kwa taarifa ya utekelezaji wa Mradi (Progress report)

Katika dosari hii ukaguzi ulidai kupatiwa taarifa mbali mbali zinazoendana na uhalisia wa matumizi ya fedha ili kupima na kujiridhisha thamani halisi ya fedha iliyotumika jambo ambalo limepelekea kutokupatiwa ripoti za utekelezaji wa mradi, hivyo ukaguzi kushindwa kufanya tathmini pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu unaohusiana na utekelezaji wa kipengele cha Ukataji wa Mlima.

Kutokuandaa ripoti ya utekelezaji ya mradi kunaweza kupelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa matumizi ya fedha za umma na kupelekea kwenda kinyume na kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha unasimamia na kutekeleza matakwa ya kisheria katika upatikanaji wa nyaraka za mradi kikamilifu.

## KIPENGELE NAMBARI 3: UWEKAJI WA MANDHARI NZURI YA ENEO LA MRADI "LAND SCAPING"

Baraza la Mji Mkoani lilifanya malipo ya shilingi 140,000,000 kwa ajili ya uwekaji wa mandhari ya Soko la Samaki na Mbogamboga ili kuzuwia mmong'onyoko wa ardhi ambapo ukaguzi ulibaini uwepo wa mapungufu yafuatayo: -

- Kukosekana kwa taarifa za makubaliano ya mkataba na mkandarasi ambae aliekabidhiwa kazi hiyo jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa matumizi ya fedha yaliyotumika.
- Kukosekana kwa taarifa za mkataba wa nyongeza (Addendum) kwa vile thamani ya fedha iliyotumika ilikwisha kuvuka kizingiti cha uitishwaji wa zabuni ya wazi.
- Kukosekana kwa taarifa ya uitishwaji wa zabuni pamoja na kukosekana kwa ripoti ya tathmini iliyotolewa na Bodi ya Zabuni jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni ya 99(1) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2020.
- Kukosekana kwa mchanganuo wa hati za makisio ya ujenzi (BoQs) ili kuweza kufanya tathmini ya mahitaji yaliyobainishwa kwenye BOQ kama yanaendana na uhalisia wa thamani ya fedha.
- Kukosekana kwa utaratibu wa malipo (Mode of payment) ili kuepusha kujitokeza kwa malalamiko pindi upande mmoja utakaposhindwa kuteleza makubalino ya malipo kwa mujibu wa mkataba.
- Kukosekana kwa nyaraka zinazothibitisha uhalali wa uwepo wa gharama za ziada.
- Kukosekana kwa taarifa za ushauri elekezi pamoja na uthibitisho wa mkataba kuwasilishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa lengo la kupatiwa ushauri wa kisheria ili kuepuka kuingia katika mkataba holela isiyokuwa na tija kwa Serikali na hatimae kuisababishia hasara Serikali.

Kutokana na mapungufu yaliyobainishwa hapo juu ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa kufanyika malipo ya ziada jambo ambalo ni kwenda kinyume na taratibu za manunuzi ya umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Mji Mkoani kuhakikisha unaongeza umakini katika kusimamia na kufuata misingi ya Sheria, ili kuepusha kujitokeza kwa uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za umma.

### 5.1.2 MRADI WA BUSTANI YA MWANAMASHUNGI

Mradi wa Ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi una lengo la kuwawekea wananchi mazingira mazuri ya upatikanaji wa huduma za kijamii na pia ni kutanua wigo wa ajira kwa wajasiriaamali.

Mradi huu unatekelezwa na Baraza la Manispaa Chake chake akiwa kama mwajiri na Wakala wa Majengo Pemba akisimama kama mshauri elekezi. Baraza liliingia katika makubaliano ya mkataba namba SMZ/D10/W/NCB/2022-2023/25 na Mkandarasi anaejulikana kwa jina la M/S Azras International Ltd na Faster Company Ltd mnamo tarehe 15/08/2022. Mkataba huo wa ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi unagharimu Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ jumla ya shilingi 1,395,168,820 pamoja na VAT.

Ujenzi wa mradi huu ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 8 kuanzia tarehe 15 Ogasti, 2022 hadi 20 Machi, 2023. Hata hivyo, mradi huu hadi ukaguzi unakamilika bado haujakamilika. Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo mradi umetekelezwa kwa kufuata Sheria na pia kuangalia thamani ya fedha iliyotumika iwapo inalingana. Kwa ujumla, ukaguzi ulihusisha shughuli zote za mradi na kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha uhai wa mradi. Thamani ya kazi zilizoidhinishwa hadi Juni 30, 2023 ilikuwa shilingi 768,069,928 sawa na asilimia 55.05 ya fedha jumla ya mkataba hivyo kubakiza shilingi 627,098,892 sawa na asilimia 44.95 ya thamani jumla ya mkataba.

**Matokeo na mapendekezo ya kazi za ukaguzi**

#### 5.1.2.1 Mradi kutokukamilika kwa wakati

Baraza la Manispaa Chake Chake liliingia mkataba wenye kumbukumbu nambari SMZ/B10/W/NCB/202-2023/25 wa tarehe 15/8/2022 na kampuni ya M/S Azras International Ltd na Faster Company Ltd kwa ajili ya Ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi kwa thamani ya shilingi 1,395,168,820 pamoja na VAT ambapo kwa mujibu wa mkataba huu, Mkandarasi alitakiwa kukamilisha mradi huo ndani ya kipindi cha miezi nane (8) kinachoanza utekelezaji wake mnamo tarehe 20/8/2022 na kuishia tarehe 20/3/2023.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni Mkandarasi kushindwa kufuata kikamilifu matakwa ya mkataba wa makubaliano ya kukamilisha Mradi huo kwa wakati kwani hadi ukaguzi huu unakamilika bado Mkandarasi huyo hajakabidhi kazi hio. Kutokukamilisha kazi kwa mujibu wa mkataba ni kwenda kinyume na makubaliano ya Mkataba niliounakili hapo juu.

Kutokukamilika kwa Mradi kwa wakati kunaweza kupelekea uwepo wa matumizi ya ziada ambayo sio ya msingi yanayoweza kusababishwa na kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa mradi huo kunakosababishwa na mfumko wa bei ya vifaa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake kuhakikisha unapotaka kuingia kwenye mkataba kuangalia kwa kina Mkandarasi mwenye uwezo.

#### 5.1.2.2 Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi (Performance Security) shilingi 139,516,882

Kwa mujibu wa kanuni nambari 29(4) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2020 inamtaka mzabuni aliyeshinda kuwasilisha hati ya dhamana ya utendaji kazi pamoja na hundi ambazo zimethibitishwa na benki anayotumia kwa Kitengo cha Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Aidha, kifungu nambari 26 cha masharti maalum ya mkataba (SCC) cha mkataba wa Ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi kinaeleza kwamba hati ya dhamana inatakiwa angalau kima cha chini kiwe sawa na asilimia 10 ya bei ya mkataba.

Katika kupitia kumbukumbu za mradi wa ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi, ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa Chake Chake liliingia katika mkataba wa Ujenzi wa Bustani wa Mwanamashungi na M/S Azras International Ltd na M/S Faster Company Ltd bila ya kuwasilishwa kwa hati ya dhamana (Performance Security). Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi ni kwenda kinyume na kanuni na kifungu cha masharti maalum ya mkataba nilivyovinakili hapo juu.

Hali hii huenda imesababishwa na Baraza la Manispaa kuchagua mkandarasi asiyekuwa na uwezo wa kutosha na hivyo kupelekea uwezekano wa kulisababishia hasara Baraza na Serikali kwa ujumla.

Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi kunaweza kupelekea kuitia hasara Serikali kwa kutokupata marejesho ya fedha zake pale ambapo mzabuni atashindwa kuwasilisha vifaa alivyotakiwa kuwasilisha au kushindwa kazi aliyopewa kwa mujibu wa mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa kuhakikisha unatekeleza vipengele vyote vya makubaliano ya mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa upotevu wa fedha za Serikali

### 5.1.2.3 Kukosekana kwa ripoti ya upembuzi yakinifu

Katika kupitia kumbukumbu za mradi wa ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa Chake Chake halikufanya upembuzi yakinifu wa kubaini asili ya udongo na vipengele vingine vinavyohitajika kabla ya ujenzi wa bustani ya Mwanamashungi.

Dosari iliyobainika ni kuchelewa kwa kazi ya ujenzi kutokana na uwepo wa udongo dhaifu unaokaa maji kwa kiwango kikubwa pindi mvua inaponyesha katika eneo lililoteuliwa kujengwa bustani. Hali hii inaweza kupelekea kuitia Serikali hasara kutokana na ucheleweshwaji wa mradi na uongezekaji wa bei za vifaa.

Kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu ni kwenda kinyume na kifungu nambari 2.3 cha Mwongozo wa Upangaji wa Miradi na Majadiliano ya Kuongeza Mikopo, Kutoa Dhamana na Kupokea Ruzuku ya Novemba, 2020.

Kukosekana kwa ripoti ya upembuzi yakinifu kunaweza kupelekea uchereweshaji wa kukamilika kwa mradi kwa wakati uliopangwa kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake kuhakikisha unafanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa miradi ya ujenzi ili kuepusha kuisababishia Serikali kutumia gharama kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo bila ya uwepo wa ulazima wa kufanya hivyo.

### 5.1.2.4 Kutozingatiwa kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu

Baraza la Manispaa Chake Chake limeingia mkataba wa Ujenzi wa Bustani na Kampuni ya M/S Azras International Ltd na M/S Faster Company Ltd wenye kumbukumbu nambari SMZ/D10/W/NCB/202-2023/25 wa tarehe 15/8/2022 kwa thamani ya shilingi 1,395,168,820 pamoja na VAT.

Ukaguzi umebaini kwamba mnamo tarehe 19 Julai, 2022 Afisi ya Baraza la Manispaa Chake Chake iliwasilisha rasimu ya Mkataba kwa Katibu Mkuu Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa lengo la kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutolewa ushauri na mnamo tarehe 2 Agosti, 2022 Mwanasheria Mkuu alirejesha mapendekezo na alishauri mambo mbali mbali kwamba yafanyike kabla ya kusainiwa kwa mkataba huo.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni Baraza la Manispaa Chake Chake kuingia katika mkataba huo bila ya kuzingatia baadhi ya ushauri uliotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali jambo ambalo linaweza kupelekea kutokea kwa migogoro baina ya Baraza na Mkandarasi na pia kuweka uwezekano wa kuingia mikataba isiyo na tija kwa taifa.

Kutokufuata maelekezo ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika usimamizi wa mikataba kunapelekea uwepo wa viashiria vya mgongano wa kimaslahi ambapo kunaweza kusababisha kutokutekelezwa kwa shughuli zilizopangwa kutokana na kutokuzingatia hali ya ubora na ufanisi jambo ambalo ni kwenda kinyume na lengo la Serikali la kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu, aidha ni kwenda kinyume na muongozo uliobainishwa hapo juu. Vipengele ambavyo Baraza la Manispaa walishindwa kuzingatia ushauri wa Mwanasheria Mkuu ni kama vifuatavyo: -

i. Kuondolewa kwa jina la Said Malik Ali badala yake liwekwe Wakala wa Majengo (ZBA) katika Kifungu nambari moja cha masharti maalumu ya mkataba (SCC 1).

ii. Kutoambatanishwa katika mkataba wa kazi mapendekezo ya rasimu kutoka ZBA.

iii. Kutokutofautishwa taarifa za kila kampuni katika fomu ya mkataba.

iv. Kutokuambatanishwa kwa makubaliano ya muungano wa kazi baina ya kampuni ya M/S Azras International na M/S Faster Company (Joint Venture Agreement).

v. Kutokukamilika kwa hati ya GCC katika sehemu ya ufafanuzi (definitions).

vi. Kutokusainiwa na kuambatanishwa muhutasari wa kikao cha mapatano (Negotiation Minutes) katika Mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake kuhakikisha unafuata Sheria, Kanuni na Miongozo yote inayotolewa na Serikali ikiwa ni pamoja na kufuata maelekezo yanayotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuleta tija katika utendaji wa taasisi.

#### 5.1.2.5 Kuchelewa kutekelezwa kwa shughuli za miradi zilizopangwa

Baraza la Manispaa Chake Chake lilisaini mkataba na Kampuni ya M/S Azras International Ltd na M/S Faster Company Ltd tarehe 5 Aprili, 2022 wenye thamani ya shilingi 1,395,168,820 pamoja na VAT kwa ajili ya ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi. Kulingana na mkataba wa ujenzi wa mradi huo kazi ambazo waliingia makubaliano ni kama zifuatazo: -

i. Ujenzi wa bustani za kisasa (Construction of modern garden)

ii. Ujenzi wa mito ya Pembeni (contruction of side stream)

iii. Ujenzi wa Majengo ya biashara (Contruction of Commercial building)

iv. Kupanda bustani (Planting the Garden)

v. Sehemu ya kupita kwa miguu (Perving interlock)

vi. Ujenzi wa sehemu za Maegesho katika bustani (Construction of Garden parking)

vii. Ujenzi wa chumba cha dharura (Contruction of emergency room)

viii. Ujenzi wa chumba kwa ajili ya usalama/Ulinzi (Contruction of security Room)

ix. Ujenzi wa sehemu/viwanja za kuchezea watoto (Construction children Play ground)

x. Ujenzi wa daraja (Contruction of Bridge)

xi. Pamoja na kazi zote ambazo zimo katika Michoro na "Bill of Quantity" (And all works described in drawing and BOQ).

Dosari iliyobainika na ukaguzi wakati wa kutembelea eneo la utekelezaji mradi mnamo tarehe 23/01/2024 ni kutokukamilika kwa kazi nyingi za ujenzi na nyengine kutokuanza kabisa licha ya mkandarasi kuomba nyongeza ya muda wa mkataba zaidi ya mara moja. Mchanganuo wa kazi ambazo hazijakamilika ni kama ufuatao: -

## Jadweli Nambari 44: Kazi ambazo hazijamalizika

| Nam | Shughuli ya mradi | Eneo la Mradi | Dosari na hatua ya utekelezaji | Picha ya mradi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa jengo la biashara (Commercial building) | Mwanamashungi | Kazi ya umaliziaji (Finishing) haijakamilika |  |
| 2. | Upandaji wa bustani ya kisasa (Modern garden) | Mwanamashungi | Kazi za umaliziaji hazijakamilika |  |
| 3. | Ujenzi wa chumba cha dharura (Emergency room) | Mwanamashungi | Kazi za kuweka madirisha, milango na baadhi ya vifaa haijakamilika |  |
| 4. | Ujenzi wa njia za miguu pamoja na njia za kupita maji(drainage system) | Mwanamashungi | Ujenzi wa njia za miguu umeanza kwa kuwekwa alama tu na ujenzi wa njia za maji(drainage system) haujaanza |  |

**Kazi za ujenzi ambazo hazijaanza utekelezaji ni kama zifuatazo: -**

i. Eneo la chini kwa ajili ya watembea kwa Miguu "Perving interlock": hili ni eneo ambalo kwa mujibu wa mkataba wa ujenzi kulitakiwa eneo la chini la mradi liwekwe vifaa maalum kwa ajili ya waenda na miguu hadi sasa lakini kazi hiyo haijafanyika.
ii. Ujenzi wa eneo maalum kwa ajili ya maegesho ya Gari "Construction of garden Parking", eneo hili ni maalum kwa ajili ya maegesho ya vyombo vya usafiri bado ujenzi wake haujaanza.
iii. Ujenzi wa sehemu za kuchezea watoto "Construction children play ground"
iv. Ujenzi wa daraja "Construction of bridge".
v. Ujenzi wa chumba kwa ajili ya usalama/Ulinzi (Contruction of security Room).

Ucheleweshaji wa miradi unaweza kupelekea kurejesha nyuma matumaini ya wananchi dhidi ya miradi inayosimamiwa na kutekelezwa na Serikali, kushuka kwa thamani ya mradi husika kulinganisha na malengo ya Serikali na kupelekea kuongezeka gharama za usimamizi na utekelezaji wa mradi pale mfumuko wa bei unapotokea.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake kupitia wasimamizi wa mradi kuhakikisha wanafanya upembuzi yakinifu (feasibility study) wakati wa uibuaji wa miradi ili kuepukana na viashiria vinavyoweza kupelekea miradi hiyo kuchelewa kwa utekelezaji wake vikiwemo viashiria vya hali ya hewa pamoja na uhaba wa fedha jambo ambalo linaweza kupelekea kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa miradi kutokana na mfumuko wa bei kwa ucheleweshaji wa mradi huo.

Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake chake kuhakikisha wanazingatia kipengele cha ulipaji faini kwa ucheleweshaji wa miradi pindi wanapoingia mikataba na kampuni za ujenzi ili kusudi kuhakikisha miradi inatekelezwa na kukamilika kwa muda uliopangwa.

### 5.1.2.6 Kutokuandaa na kuwasilisha kwa hesabu za utekelezaji wa Mradi

Kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, zinatakiwa Taasisi za Umma ziandae na ziwasilishe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba Baraza la Manispaa Chake Chake halikuandaa wala kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi ya utekelezaji wa mardi wa maendeleo wa Ujenzi wa Bustani ya Mwanamashungi jambo ambalo liemepelekea kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kwa mujibu wa utaratibu.

Kutokuandaa na kuwasilisha kwa taarifa za hesabu ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake kuhakikisha unaandaa na kuwasilisha taarifa za hesabu zinazohusiana na utekelezaji wa miradi ili kuweza kutoa maoni ya ukaguzi juu ya hali ya utekelezaji wa miradi hiyo.

### 5.1.3 MRADI WA SOKO LA MACHOMANNE

**Mwenendo wa mradi wa Soko la Machomanne**

Mradi wa Ujenzi wa Soko la Machomanne katika eneo la Machomanne una lengo la kuwawekea wananchi mazingira mazuri ya upatikanaji wa huduma za kijamii na pia ni kutanua wigo wa ajira kwa wajasiriaamali.

Mradi huu unatekelezwa na Baraza la Manispaa Chake Chake akiwa ndio mwajiri na Wakala wa Majengo Pemba akisimama kama mshauri elekezi. Baraza liliingia katika makubaliano ya mkataba na Mkandarasi anaejulikana kwa jina la Comfix & Engineering mnamo tarehe 28 Aprili, 2022.

Mkataba wa ujenzi wa soko la Machomanne uligharimu Baraza la Manispaa kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ jumla ya shilingi 1,053,441,374.98 pamoja na VAT. Ujenzi wa mradi huu ulitakiwa kukamilika ndani ya mwaka mmoja (1) kuanzia tarehe 28 Aprili, 2022 hadi 28 Aprili, 2023.

Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo mradi umetekelezwa kwa kufuata Sheria, udhibiti wa ndani na pia kuangalia thamani ya fedha iliyotumika iwapo inalingana. Kwa ujumla, ukaguzi ulihusisha shughuli zote za mradi na kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha uhai wa mradi. Thamani ya kazi zilizoidhinishwa hadi 30 Juni, 2023 ilikuwa shilingi 571,376,549 sawa na asilimia 54.24 ya fedha jumla ya mkataba hivyo kubakiza shilingi 482,064,825.98 sawa na asilimia 45.76 ya thamani jumla ya mkataba.

#### 5.1.3.1 Kutokuandaa na kuwasilisha kwa hesabu za utekelezaji wa Mradi

Kwa mujibu wa kifungu namba 119(1) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, zinatakiwa Taasisi za Umma ziandae na ziwasilishe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba Baraza la Manispaa Chake Chake halikuandaa wala kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi ya utekelezaji wa mardi wa maendeleo wa ujenzi wa Soko la Machomane jambo ambalo liemepelekea kushindwa kutoa maoni ya ukaguzi kwa mujibu wa utaratibu.

Kutokuandaa na kuwasilisha kwa taarifa za hesabu ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake kuhakikisha unaandaa na kuwasilisha taarifa za hesabu zinazohusiana na utekelezaji wa miradi ili kuweza kutoa maoni ya ukaguzi juu ya utekelezaji wa miradi hiyo.

#### 5.1.3.2 Kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa Soko la Machomanne

Baraza la Manispaa Chake Chake liliingia katika hati ya makubaliano ya mkataba tarehe 15/8/2022 na kampuni ya M/S Comfix & Engineering Ltd kwa ajili ya Ujenzi wa Soko la Machomanne kwa thamani ya shilingi 1,053,441,374.98 pamoja na VAT ambapo kwa mujibu wa mkataba huo, Mkandarasi alitakiwa kukamilisha mradi huo ndani ya kipindi cha mwaka mmoja (1) kinachoanza utekelezaji wake mnamo tarehe 28/4/2022 na kuishia tarehe 28/4/2023.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwa licha ya kufunguliwa kwa mradi huo mnamo tarehe 3/1/2024 lakini bado Mkandarasi ameshindwa kufuata kikamilifu matwaka ya mkataba wa makubaliano ya kukamilisha Mradi huo kwa wakati kwani hadi ukaguzi huu unakamilika bado Mkandarasi huyo hajakabidhi kazi hio. Kutokukamilisha kazi kwa mujibu wa mkataba ni kwenda kinyume na makubaliano ya Mkataba niliounakili hapo juu.

Mradi kutokukamilika kwa wakati kunaweza kupelekea kuwepo kwa matumizi ya ziada ambayo sio ya msingi yanayoweza kusababishwa na kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa mradi huo kunakosababishwa na mfumko wa bei ya vifaa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake kuhakikisha unapotaka kuingia kwenye mkataba kuangalia kwa kina Mkandarasi mwenye uwezo.

#### 5.1.3.3 Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji (Perfomance Security)

Kwa mujibu wa kanuni nambari 29(4) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2020 inamtaka mzabuni aliyeshinda kuwasilisha hati ya dhamana pamoja na hundi ambazo zimethibitishwa na benki anayotumia kwa Kitengo cha Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Aidha, kifungu nambari 26 cha masharti maalum ya mkataba (SCC) cha mkataba wa Ujenzi wa Soko la Machomanne kinaeleza kwamba hati ya dhamana inatakiwa angalau kima cha chini kiwe sawa na asilimia 10 ya bei ya mkataba.

Katika kupitia kumbukumbu za mradi wa ujenzi wa Soko la Machomanne, ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa Chake Chake liliingia katika mkataba wa Ujenzi wa Soko la Machomanne Chake Chake Pemba na Comfix & Engineering Ltd bila ya kuwasilishwa kwa hati ya dhamana (Performance Security). Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ni kwenda kinyume na kanuni na kifungu cha masharti maalum ya mkataba niliyoyanakili hapo juu.

Hali hii huenda imesababishwa na Baraza la Manispaa kuchagua mkandarasi asiyekuwa na uwezo wa kutosha na hivyo kupelekea uwezekano wa kulisababishia hasara Baraza na Serikali kwa ujumla.

Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kunaweza kuitia hasara Serikali kwa kutokupata marejesho ya fedha zake pale ambapo mzabuni atashindwa kuwasilisha vifaa alivyotakiwa kuwasilisha au kushindwa kazi aliyopewa kwa mujibu wa mkataba

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa kuhakikisha unatekeleza vipengele vyote vya makubaliano ya mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa upotevu wa fedha za Serikali.

#### 5.1.3.4 Dosari katika mkataba wa ujenzi wa soko la Machomanne

Baraza la Manispaa Chake Chake limesaini hati ya makubaliano ya mkataba na Kampuni ya M/S Comfix & Engineering Ltd mnamo tarehe 28 Aprili 2022 kwa ajili ya Ujenzi wa Soko la Machomanne lililopo Machomanne Chake Chake Pemba kwa thamani ya shilingi 1,053,441,374.98. Dosari zilizobainika baada ya kupitia mkataba huo ni kama zifuatazo: -

i. Kukosekana kwa nambari ya mkataba.

ii. Kutokuambatanishwa kwa nyaraka muhimu za mkataba kama vile, Barua ya kukubali kufanya kazi (Letter of acceptance), Michoro, Hati ya dhamana ya benki, Masharti ya jumla ya mkataba (GCC) na Masharti maalumu ya mkataba (SCC).

iii. Mkataba haukuonesha tarehe rasmi ya kuanza kwa kazi bali umeonesha tarehe ya kusaini mkataba.

iv. Mkataba haukuanisha kazi zitakazofanywa na Mkandarasi.

v. Mkataba haukuanisha asilimia ya hati ya dhamana ya benki anayotakiwa Mkandarasi kuiwasilisha kwa ajili ya malipo.

Uwepo wa dosari hizi kunapelekea ukaguzi kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa mkataba huo pamoja na uthibitisho wa uhalali wa malipo. Kutokuingiza baadhi ya vipengele muhimu katika mkataba kunaweza kuitia hasara Serikali na pia ni kwenda kinyume na Sheria, kanuni na Miongozo ya Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake unapotaka kuingia katika mkataba wahakikishe kwamba mkataba huo umepitiwa na kupata mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa lengo la kujiepusha na uingiaji wa mikataba isiyo na tija na hivyo kupelekea kuitia hasara Serikali.

### 5.1.3.5 Kutokuzingatiwa kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Baraza la Manispaa Chake Chake limeingia mkataba wa ujenzi na Kampuni ya Comfix & Engineering tarehe 28 April, 2022 kwa ajili ya ujenzi wa soko la Machomanne lililopo Chake Chake kwa thamani ya shilingi 1,053,441,374.98.

Ukaguzi umebaini kwamba mnamo tarehe 25 Machi, 2022 Afisi ya Baraza la Manispaa Chake Chake liliwasilisha rasimu ya Mkataba kwa Katibu Mkuu Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa lengo la kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa na kutolewa ushauri na mnamo tarehe 5 Aprili, 2022 Mwanasheria Mkuu alirejesha mapendekezo na alishauri kufanyiwa marekebisho wa baadhi ya vifungu vya mkataba kabla ya kusainiwa kwa mkataba huo.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni Baraza la Manispaa Chake Chake kuingia katika mkataba huo bila ya kuzingatia kikamilifu ushauri uliotolewa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali jambo ambalo linaweza kupelekea kutokea kwa migogoro baina ya Baraza na Mkandarasi na pia kuweka uwezekano wa kuingia mikataba isiyo na tija kwa taifa.

Kutokuzingatia ushauri wa Mwanasheria Mkuu ni kwenda kinyume na kanuni nambari 47(1-4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020. Vipengele ambavyo Baraza la Manispaa walishindwa kuzingatia ushauri wa Mwanasheria Mkuu ni kama vifuatavyo:-

- Kutoambatanishwa mapendekezo ya rasimu kutoka ZBA katika mkataba wa kazi.
- Kutokuambatanishwa kwa barua ya kumtaarifu Mkandarasi (Notification of Award) na hati ya technical specification katika rasimu ya mkataba.
- Kutokuambatanishwa kwa masharti maalumu ya mkataba (SCC).
- Kutokuanishwa kipengele cha performance security katika mkataba.
- Kutokutumika lugha ya Kiengereza kama ni lugha ya nyaraka za mkataba.

Kutokufuata maelekezo ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika usimamizi wa mikataba kunapelekea uwepo wa viashiria vya mgongano wa kimaslahi ambapo kunaweza kusababisha kutokutekelezwa kwa shughuli zilizopangwa kutokana na kutokuzingatia hali ya ubora na ufanisi jambo ambalo ni kwenda kinyume na lengo la Serikali la kuanzisha Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake kuhakikisha wanafuata Sheria na Kanuni na Miongozo yote inayotolewa na Serikali ikiwa ni pamoja na kufuata maelekezo yanayotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuleta tija katika utendaji wa taasisi.

### 5.1.3.6 Kukosekana kwa ripoti ya Mkaguzi wa Ndani

Kwa mujibu wa kifungu nambari 117(5) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 inasema kwamba "Katika kutekeleza majukumu yao, wakaguzi wa ndani watatoa kwa maandishi taarifa za ukaguzi wa ndani pamoja na mapendekezo kwa Maafisa Wahasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba Baraza la Manispaa Chake Chake hawakuandaa taarifa za ukaguzi wa ndani zinazohusu mradi wa ujenzi wa soko la Machomanne jambo ambalo linaweza kupelekea kutokubainika mapema kwa vihatarishi (Risk) vya mradi ambavyo vinaweza kupelekea ucheleweshaji wa ukamilikaji wa mradi pamoja na ukiukwaji wa sheria mbali mbali ikiwemo kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Baraza la Manispaa Chake Chake kuhakikisha kuwa Mkaguzi wa Ndani anakagua na kutoa ripoti kwa kazi zote zinazohusiana na baraza ikiwemo kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

### 5.1.4 MRADI WA UJENZI WA KITUO CHA MABASI KINOWE

**Mwenendo wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe**

Mradi wa ujenzi wa kituo cha Mabasi Kinowe katika eneo la Kinowe-Konde umeanzishwa kwa lengo la kuwawekea wananchi mazingira mazuri ya upatikanaji wa huduma za kijamii karibu na maeneo yao na pia ni kutanua wigo wa ajira kwa wajasiriaamali.

Mradi huu unatekelezwa na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni akiwa ndio mwajiri na Wakala wa Majengo Pemba akisimama kama mshauri elekezi. Halmashauri iliingia katika makubaliano ya mkataba na Mkandarasi anaejulikana kwa jina la M/S Comfix & Engineering Co. Ltd mnamo tarehe 13/5/2022 kupitia Mkataba nambari SMZ/D11-212/W/DP/2021-2022/15.

Mkataba huo wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe Konde unaigharimu Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ jumla ya shilingi 1,046,224,500. Ujenzi wa mradi huu ulitakiwa kukamilika ndani ya miezi 8 kuanzia tarehe 13 Mei, 2022. Hata hivyo, hadi ukaguzi huu unakamilika bado mradi huo haujakamilika.

Kwa ujumla, ukaguzi ulihusisha shughuli zote za mradi na kazi zilizotekelezwa katika kipindi cha uhai wa mradi. Thamani ya kazi zilizoidhinishwa hadi Juni 30, 2023 ilikuwa shilingi 849,494,900 sawa na asilimia 81.2 ya fedha jumla ya mkataba hivyo kubakiza shilingi 196,729,600 sawa na asilimia 18.8 ya thamani jumla ya mkataba.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.4.1 Kukosekana kwa ripoti ya utekelezaji wa Mradi

Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imesaini hati ya makubaliano ya mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe na Kampuni ya M/S Comfix & Engineering Co. Ltd wenye nambari SMZ/D11-212/W/DP/2021-2022/15 wa tarehe 13/5/2022 wenye thamani ya shilingi 1,046,224,500.

Katika kupitia kumbukumbu mbali mbali za mradi ukaguzi umeshindwa kuona na kupitia ripoti ya utekelezaji ya mradi huo hali iliyopelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa mwenendo wa utekelezaji wake, kukosekana kwa uwazi katika taarifa za kifedha na kutokubainika kwa changamoto na mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha utekelezaji.

Hali hii inaweza kupelekea ugumu katika kufanya tathmini ya maendeleo ya mradi na pia ni kwenda kinyume na kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri kuhakikisha unatayarisha na kuhifadhi vielelezo vyote vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Afisi ya Halmashauri.

### 5.1.4.2 Kukosekana kwa ripoti za Mkaguzi wa ndani

Kwa mujibu wa kifungu nambari 117(5) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 inasema kwamba "Katika kutekeleza majukumu yao, wakaguzi wa ndani watatoa kwa maandishi taarifa za ukaguzi wa ndani pamoja na mapendekezo kwa Maafisa Wahasibu."

Ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni hawakuandaa taarifa za ukaguzi wa ndani zinazohusu mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi. Hali inayopelekea Halmashauri kutokupata ushauri wa kitalaam unauhusiana na masuala ya kifedha na mambo mengine kwa wakati. Aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha kuwa Mkaguzi wa Ndani anakagua na kutoa ripoti kwa kazi zote zinazohusiana na Halmashauri ikiwemo kufanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kutoa ushauri wa kitaalam kwa wakati.

### 5.1.4.3 Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi (Performance Security) shilingi 104,622,450

Kwa mujibu wa kanuni nambari 29(4) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2020 inamtaka mzabuni aliyeshinda kuwasilisha hati ya dhamana pamoja na hundi ambazo zimethibitishwa na benki anayotumia kwa Kitengo cha Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Aidha, kifungu nambari 55.1 cha masharti maalum ya mkataba (SCC) cha mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi kinamtaka Mkandarasi kuwasilisha hati ya dhamana ya utendaji kazi ya asilimia 10 ya bei ya mkataba.

Katika kupitia kumbukumbu za mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi, ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni iliingia katika mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi na M/S Comfix & Engineering Co. Ltd bila ya kuwasilishwa kwa hati ya dhamana (Performance Security). Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ni kwenda kinyume na kanuni na kifungu cha masharti maalum ya mkataba nilivyovinakili hapo juu.

Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi kunaweza kuisababishia hasara Serikali kwa kutokupata marejesho ya fedha zake pale ambapo mzabuni atashindwa kuwasilisha vifaa alivyotakiwa kuwasilisha au kushindwa kazi aliyopewa kwa mujibu wa mkataba, aidha hupelekea uwezekano wa kuisababishia Halmashauri hasara na Serikali kwa ujumla pindipo Mkandarasi huyo akishindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha wanasimamia vyema matakwa ya Sheria na masharti ya mkataba ili kuiepushia Serikali hasara inayotokana na upotevu wa fedha za Serikali.

#### 5.1.4.4 Kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu kabla ya utekelezaji wa Mradi

Katika kupitia kumbukumbu za mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni haikufanya upembuzi yakinifu wa kubaini asili ya udongo na vipengele vingine vinavyohitajika kabla ya ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe.

Dosari iliyobainika ni kuchelewa kwa kazi ya ujenzi kutokana na uwepo wa udongo dhaifu unaokaa maji kwa kiwango kikubwa pindi mvua inaponyesha katika eneo lililoteuliwa kujengwa Kituo cha Mabasi. Hali hii inaweza kupelekea kuitia Serikali hasara kutokana na ucheleweshwaji wa mradi na upandaji wa bei za vifaa. Kutokufanyika kwa upembuzi yakinifu ni kwenda kinyume na kifungu nambari 2.3 cha Mwongozo wa Upangaji wa Miradi na Majadiliano ya Kuongeza Mikopo, Kutoa Dhamana na Kupokea Ruzuku ya Novemba, 2020.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha unafanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa miradi ya ujenzi ili kuepusha kuisababishia Serikali kutumia gharama kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo bila ya uwepo wa ulazima wa kufanya hivyo.

#### 5.1.4.5 Malipo ya awali yaliyolipwa kinyume na utaratibu shilingi 209,244,900

Kwa mujibu wa kifungu cha 54.1 cha masharti ya jumla ya mkataba (GCC 54.1) kikisomwa pamoja na kifungu cha 25 cha masharti maalum ya mkataba (SCC 25) namba SMZ/D11-212/W/DP/20212022/15 wa tarehe 13/5/2022 baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kama mwajiri na Kampuni ya Comfix & Engineering Co. Ltd kama Mkandarasi vinaeleza kwamba, kiwango cha juu cha malipo ya awali kitakua asilimia 20 ya thamani ya mkataba chini ya kiasi cha muda kinacholipwa na mwajiri baada ya kuwasilisha hati ya dhamana ya kibenki bila masharti.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanya malipo ya awali ya shilingi 209,244,900 sawa na asilimia 20 ya thamani ya mkataba kwa Mkandarasi kabla ya Mkandarasi huyo wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe kuwasilisha hati ya dhamana ya benki kwa mujibu wa matakwa ya mkataba wao. Hali hii inaweza kupelekea Afisi ya Halmashauri kuitia hasara Serikali pindipo mkandarasi akiamua kuiwacha kazi husika, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha wanafuata kikamifu Sheria, Kanuni na Matakwa ya mkataba ili kuepukana na hasara inayoweza kujitokeza pindipo Mkandarasi akiamua kuacha kazi.

#### 5.1.4.6 Kutokukatwa malipo ya kitangulizi katika vyeti vya malipo (Interim payment certificate) shilingi 128,050,000

Kwa mujibu wa kifungu cha 54.1 cha masharti ya jumla ya mkataba (GCC 54.1) kikisomwa pamoja na kifungu cha 25 cha masharti maalum ya mkataba (SCC 25) namba SMZ/D11-212/W/DP/20212022/15 wa tarehe 13/5/2022 baina ya Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kama mwajiri na Kampuni ya M/S Comfix & Engineering Co. Ltd kama Mkandarasi vinaeleza kwamba, kiwango cha juu cha malipo ya awali kitakua asilimia 20 ya thamani ya mkataba chini ya kiasi cha muda kinacholipwa na mwajiri baada ya kuwasilisha hati ya dhamana ya benki bila masharti na malipo hayo yatarejeshwa asilimia 20 kwa kila cheti cha malipo (interim payment certificate).

Ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni imefanya malipo ya shilingi 640,250,000 kwa awamu mbili tofauti ikiwa awamu ya mwanzo wamelipa shilingi 408,250,000 kwa ajili ya malipo ya cheti cha mwanzo na shilingi 232,000,000 ikiwa ni kwa ajili ya malipo ya cheti cha pili bila kukata asilimia 20 ya kurejesha malipo ya kitangulizi (Advance Payment) ambayo kwa ujumla wake ni shilingi 128,050,000 kama masharti ya mkataba yanavyoelekeza.

Kutokukatwa malipo ya kitangulizi katika vyeti vya malipo (Interim payment certificate) kunaweza kupelekea hasara kwa Serikali pindipo Mkandarasi akiamua kuacha kazi, aidha ni kwenda kinyume na kifungu tajwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha unasimamia vyema makubaliano ya mkataba kama Sheria zinavyoelekeza.

#### 5.1.4.7 Mapungufu katika mkataba wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe

Baada ya kupitia nyaraka mbali mbali za mradi ukaguzi umebaini uwepo wa barua ya malalamiko yenye kumbukumbu nambari Mac/com/23/315/50 ya tarehe 22/5/2023 kutoka Kampuni ya M/S Comfix Engineering limited kwenda Afisi ya Halmashauri ikilalamikia kupokea malipo yaliyokatwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kutoka katika bei ya mkataba ya shilingi 1,046,224,500.

Dosari iliyobainika katika mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi wenye kumbu kumbu nambari SMZ/D11-212/W/DP/2021-2022/15 wa tarehe 13/5/2022 uliosainiwa baina Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kama mwajiri na Kampuni ya M/S Comfix Engineering Co. Ltd kama Mkandarasi ni kutokuanisha iwapo malipo ya mkataba ya shilingi 1,046,224,500 yanajumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) au vyenginevyo. Hali hii imepelekea kutokea kwa tofauti ya uwelewa baina ya mwajiri na mkandarasi jambo lililopelekea kiashiria cha kutokea kwa mgogoro baina yao.

Kuwepo kwa mapungufu katika mkataba wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe kunaweza kupelekea uwezekano wa kutokea kwa migogoro baina ya muajiri na mkandarasi na pia inaweza kupelekea kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri kuhakikisha mikataba yote wanayoingia wanaipeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kupata maoni ya kitaalamu na hivyo kuingia mikataba ambayo haitaleta migogoro na pia yenye kuleta tija kwa taifa.

### 5.1.4.8 Mradi kutekelezwa bila ya uwepo wa hati ya dhamana ya benki

Kwa mujibu wa kanuni nambari 29(4) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2020 inamtaka mzabuni aliyeshinda kuwasilisha hati ya dhamana pamoja na hundi ambazo zimethibitishwa na benki anayotumia kwa Kitengo cha Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma.

Katika kupitia kumbukumbu za mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kinowe, ukaguzi umebaini kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni iliingia katika mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi na Kampuni ya M/S Comfix & Engineering Co. Ltd wenye kumbu kumbu nambari SMZ/D11-212/W/DP/2021-2022/15 bila ya kuwasilishwa kwa hati ya dhamana (Performance Security). Kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya benki ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Hali hii huenda imesababishwa na Halmashauri kuchagua mkandarasi asiyekuwa na uwezo wa kutosha na hivyo kupelekea uwezekano wa kuisababishia hasara Halmashauri na Serikali kwa ujumla.

Kufanya hivyo kunapelekea kuitia hasara Serikali kwa kutokupata marejesho ya fedha zake pale ambapo mzabuni atashindwa kuwasilisha vifaa alivyotakiwa kuwasilisha au kushindwa kazi aliyopewa kwa mujibu wa mkataba

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kuhakikisha kuwa wanasimamia vyema Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali ikiwa ni pamoja na kutokuanza kazi za ujenzi wa miradi mikubwa bila ya kuwepo kwa hati ya dhamana ya benki.

### 5.1.5 MRADI WA UJENZI WA JENGO JIPYA LA BIASHARA NA MAKAAZI MKUNGU MALOFA CHAKE CHAKE PEMBA

Ukaguzi huu umefanywa kufuatia uwepo wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Biashara na Nyumba za Makaazi linaloendelea kujengwa katika Eneo la Mkungu Malofa Chake Chake Pemba katika hatua ya awali (Phase 1)

Shirika la Nyumba Pemba lilikadiria kutumia jumla ya shilingi 500,000,000 kwa ajili ya Ujenzi wa Jengo la Biashara na Nyumba za Makaazi Mkungu Malofa Chake Chake Pemba katika hatua ya mwanzo (Phase 1). Hadi kufikia 30 Juni, 2023 Shirika la Nyumba limetumia jumla ya shilingi 200,537,197 sawa na asilimia 40.11 ya makadirio.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.5.1 Kukosekana kwa kibali cha mapokezi ya bidhaa za ujenzi zilizonunuliwa (certificate of acceptance) shillingi 110,101,040

Kwa mujibu wa mkataba baina ya Shirika la Nyumba Zanzibar na MDK Group Limited kifungu cha 18.7 (iii) Mkataba nambari SMZ/NO.108/G/NCB/2022/23/17-Pemba uliofungwa tarehe 05/05/2023 kinaeleza kwamba, "katika kukubaliwa (On acceptance)" asilimia 100 ya bei ya mkataba italipwa kwa msambazaji ndani ya siku 30 baada ya tarehe ya certificate of acceptance kwa uwasilishaji husika uliotolewa na Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 110,101,040 (VAT Exclusive) zimelipwa kwa ajili ya ununuzi wa bidhaa mbali mbali za ujenzi bila ya kuandaa kibali cha mapokezi ya bidhaa (certificate of acceptance) kama mkataba unavyoelekeza.

Kutokuandaa kibali cha mapokezi ya bidhaa (certificate of acceptance) kunaweza kupelekea kukosekana kwa ubora wa bidhaa zinazonunuliwa kutoka kwa wasambazaji, jambo ambalo pia hupelekea upotevu wa fedha unaotokana na kufanyika kwa ununuzi wa bidhaa chini ya kiwango kinachohitajika na hatimae kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba kuandaa kibali cha mapokezi ya bidhaa (certificate of acceptance) kama mkataba unavyoelekeza ili kuweza kufikia ufanisi wa ununuzi wa bidhaa na kupunguza athari zinazoweza kutokea zinazohusiana na ununuzi wa bidhaa au huduma kinyume na mkataba. Mchanganuo wa malipo ya ununuzi wa bidhaa za ujenzi bila ya kutolewa kibali cha mapokezi (certificate of acceptance) ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 45: Malipo ya ununuzi wa bidhaa ambazo hazina kibali cha mapokezi**

| Hati Namba | Hundi Namba | Fedha zilizolipwa | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 26/5 ya 24/5/2023 | T.T | 5,542,880 | MDK GROUP LTD | Malipo kwa ajili ya usambazaji wa vifaa mbali mbali vya ujenzi. |
| 27/5 ya 24/5/2023 | | 23,030,000 | | |
| 20/6 ya 26/6/2023 | | 31,556,000 | | |
| 21/6 | | 49,972,160 | | |
| **Jumla** | | **110,101,040** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za Malipo*

### 5.1.5.2 Malipo ambayo hayakupitia katika mfumo wa ununuzi wa kielektronoki (e-Proz) shilingi 63,789,180

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.156/370/01/27 ya tarehe 12/08/2022 kutoka Mamlaka ya Ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma inaeleza kuwa "kuanzia tarehe 15/08/2022 manunuzi yote ya Serikali yanatakiwa yafanywe kwa kutumia mfumo huo". Aidha, "Mamlaka inasisitiza changamoto yeyote itakayojitokeza katika matumizi ya mfumo ziwasilishwe Mamlaka haraka iwezekanavyo kwa ajili ya utatuzi".

Ukaguzi umeibaini kwamba jumla ya shilingi 63,789,180 zimelipwa kwa ununuzi wa vifaa mbalimbali kwa matumizi ya Shirika la Nyumba Pemba bila ya kutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (e-Proz).

Kutokutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (e-Proz) kunaweza kupelekea kuwakosesha wafanyabiashara wengine kutofanya biashara na Serikali pamoja na kufanya ununuzi wa bei ya juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba kufanya manunuzi kwa kutumia mfumo wa manunuzi wa kielektroniki uliowekwa na Serikali chini ya Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma. Malipo hayo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 46: zilizonunuliwa wa bidhaa bila ya kutumia mfumo wa ununuzi wa Kielektroniki**

| Hati Namba | Hundi | Thamani (Tshs) | Alielipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 6/3 ya 28/02/2023 | T.T | 1,529,780 | IDDI HAMAD ALI | Malipo kwa ajili ya usambazaji wa vifaa mbali mbali vya ujenzi |
| 2/3 ya 28/02/2023 | | 5,997,600 | | |
| 12/2 ya 23/02/2023 | | 4,498,200 | | |
| 18/6 ya 26/06/2023 | | 8,820,000 | | |
| 7/11 ya 08/11/2022 | | 2,998,800 | | |
| 7/10 ya 21/10/2022 | | 4,351,200 | KHADIJA AHMED OMAR | |
| 17/11 ya 24/11/2022 | | 6,311,200 | | |
| 22/3 ya 28/03/2023 | | 23,402,400 | MDK GROUP | |
| 23/3 ya 28/3/2023 | | 5,880,000 | | |
| **Jumla** | | **63,789,180** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za Malipo*

### 5.1.5.3 Malipo ambayo hayakufuata utaratibu wa utoaji wa zabuni shilingi 73,568,110

Kwa mujibu wa kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma ambayo haiwezi kufuata utaratibu wa sheria hii uliowekwa kwa mnunuzi na uondoshaji wa mali za umma, inaruhusiwa kuomba kwa mamlaka kutumia njia au utaratibu mwengine".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 73,568,110 zimelipwa na Shirika la Nyumba Pemba kwa njia ya ununuzi wa kuvunjavunja (Spliting) ili kutekeleza mradi wa ujenzi wa jengo la Biashara na Makaazi Pemba bila utoaji wa zabuni, hali ambayo hupelekea kufanya matumizi kwa gharama kubwa, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba kuhakikisha kuwa ununuzi wote unafanyika kulingana na Sheria na miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo utoaji wa zabuni pale kiwango cha utowaji wa zabuni kinapofikia. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 47: Malipo ambayo hayakufuata utaratibu wa utoaji wa zabuni

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 6/3 ya 28/02/2023 | T.T | 1,529,780 | IDDI HAMAD ALI | Malipo kwa ajili ya usambazaji wa vifaa mbali mbali vya ujenzi |
| 2/3 ya 28/02/2023 | | 5,997,600 | | |
| 12/2 ya 23/02/2023 | | 4,498,200 | | |
| 18/6 ya 26/06/2023 | | 8,820,000 | | |
| 7/11 ya 08/11/2022 | | 2,998,800 | | |
| 7/10 ya 21/10/2022 | | 4,351,200 | KHADIJA AHMED OMAR | |
| 9/11 ya 11/11/2022 | | 5,414,500 | | |
| 17/11 ya 24/11/2022 | | 6,311,200 | | |
| 22/3 ya 28/03/2023 | T.T | 23,402,400 | MDK GROUP | |
| 23/3 ya 28/3/2023 | | 5,880,000 | | |
| 11/01 ya 17/1/2023 | | 4,364,430 | RSM KOREA TIMBER AND HARDWARE | |
| **Jumla** | | **73,568,110** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za Malipo*

### 5.1.5.4 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 19,972,588

Kanuni nambari 55(1)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inamtaka "Afisa Masuuli kuhakikisha kwamba malipo yote lazima yaambatanishwe na vielelezo vilivyokamilika".

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 19,972,588 zimelipwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la biashara na makaazi la Mkungu Malofa lakini baadhi ya vielelezo vya matumizi hayo havikuambanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuhakikisha unaambatanisha vielelezo vyote vya malipo mara tu baada ya malipo kukamilika. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 48: Malipo yenye vielelezo pungufu

| Hati Namba | Hundi | Alielipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 10/4 ya 20/9/2023 | T.T | Shirika la Nyumba Pemba | 440,000 | Malipo kwa ajili ya ujenzi wa jengo la biashara na makaazi la Mkungu Malofa |
| 6/12 ya 19/12/2023 | | | 1,000,000 | |
| 15/6 ya 20/6/2023 | | Abdalla Adi Mohd | 2,035,631 | |
| 13/2 ya 23/12/2022 | | Hamoud Sanani Seif | 3,770,144 | |
| 12/5 ya 9/5/2023 | | Abdalla Adi Mohd | 2,998,192 | |
| 14/3 ya 22/3/2023 | 000366 | Machano Ali Machano | 3,759,773 | |
| 5/11 ya 4/11/2022 | T.T | Salum Ali Said | 1,544,424 | |
| 8/11 ya 10/11/2022 | | Salum Ali Said | 1,544,424 | |
| 9/6 ya 15/06/2023 | | Machano Ali Machano | 2,320,000 | |
| 5/4 ya 13/04/2023 | 000371 | Ahmada Mohd Ahmada | 560,000 | |
| **Jumla** | | | **19,972,588** | |

### 5.1.5.5 Kukosekana kwa vielelezo vya uwasilishaji wa kodi Serikalini shilingi 14,247,350

Kwa mujibu wa kifungu nambari 50(2) cha Sheria nambari 7 ya Usimamizi wa Kodi ya 2009 iliyofanyiwa marekebisho 2020 inaelezea juu ya umuhimu wa kukata kodi na kuiwasilisha Serikalini.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 14,247,350 ni kodi mbali mbali iliyopaswa kukatwa na kuwasilishwa Serikalini itokanayo na malipo yenye jumla ya shilingi 157,957,140 yaliyofanywa kwa watoa huduma mbali kwa ununuzi wa bidhaa na huduma kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Biashara, ambapo kati ya fedha hizo shilingi 10,030,775 ni VAT asilimia 15, shilingi 331,534 ni kodi ya stamp duty asilimia 2, na shilingi 3,885,041 ni withholding tax ya asilimia 5. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha kuwasilishwa kwa kodi hiyo katika Mamlaka husika jambo ambalo linaweza kupelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hizo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kukata kodi mbali mbali katika malipo ambayo yanapaswa kukatwa kodi kwa mujibu wa mkataba na kuziwasilisha Serikalini. Mchanganuo wa kodi hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 49: Kodi ambazo hazikuwasilishwa Serikalini

| Hati Namba | Alielipwa | Fedha zilizolipwa (Tshs) | VAT 15% | Stamp Duty 2% | TRA 5% | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 12/05 ya 09/05/2023 | Abdalla Adi Mohd | 2,998,192.4 | 0 | 64,408 | 157,799.6 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 39/5 ya 30/1/2023 | Maroo Master G. Supplier | 4,681,950 | 0 | 97,500 | 95,550 | |
| 15/3 ya 22/03/2023 | Khamis Yussuf Uyalo | 2,285,752 | 0 | 47,600 | 46,648 | |
| 8/2 ya 2/2/2023 | Abdalla Adi Mohd | 2,076,255 | 0 | 0 | 109,275 | |
| 14/3 ya 22/3/2023 | Machano Ali Machano | 3,759,773.92 | 0 | 78,296 | 76,730.08 | |
| 13/2 ya 23/12/2023 | Hamoud Sanani Seif | 3,770,144.4 | 0 | 0 | 194,255.6 | |
| 14/06 ya 20/06/2023 | Khamis Yussuf Uyalo | 3,270,137.5 | 0 | 0 | 172,112.5 | |
| 15/6 ya 20/6/2023 | Abdalla Adi Mohd | 2,035,631.5 | 0 | 43,730 | 107,138.5 | |
| 7/11 ya 08/11/2022 | Iddi Hamad Ali | 2,998,800 | 540,000 | 0 | 61,200 | |
| 18/06 ya 26/06/2023 | Iddi Hamad Ali | 8,820,000 | 0 | 0 | 180,000 | |
| 12/2 ya 23/02/2023 | Iddi Hamad Ali | 4,498,200 | 0 | 0 | 91,800 | |
| 21/3 ya 28/3/2023 | Iddi Hamad Ali | 5,997,600 | 1,080,000 | 0 | 122,400 | |
| 6/3 ya 23/02/2023 | Iddi Hamad Ali | 1,529,780 | 275,000 | 0 | 31,220 | |
| 11/01 ya 17/01/2023 | RSM Korea Timber and Hardware | 4,364,430 | 668,025 | 0 | 89,070 | |
| 22/3 ya 28/03/2023 | MDK GROUP LTD | 23,880,000 | 3,582,000 | 0 | 477,600 | |
| 23/3 ya 28/3/2023 | | 4,980,000 | 900,000 | 0 | 120,000 | |
| 9/11 ya 11/11/2022 | Khadija Ahmed Omar | 5,414,500 | 828,750 | 0 | 110,500 | |
| 7/10 ya 21/10/2022 | | 4,351,200 | 666,000 | 0 | 88,800 | |
| 17/11 ya 24/11/2022 | | 6,311,200 | 966,000 | 0 | 128,800 | |

| Hati Namba | Alielipwa | Fedha zilizolipwa (Tshs) | VAT 15% | Stamp Duty 2% | TRA 5% | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 26/5 ya 24/5/2020 | MDK GROUP LTD | 4,904,760 | 525,000 | 0 | 113,120 | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 21/6 ya 28/6/2023 | | 49,972,160 | 0 | 0 | 1,019,840 | |
| 9/6 ya 15/06/2023 | Machano Ali Machano | 2,320,440 | 0 | 0 | 119,560 | |
| 8/1 ya 9/1/2023 | Asaa Kheri Asaa | 1,400,000 | 0 | 0 | 0 | |
| 18/6 ya 17/05/2023 | Mkubwa Juma Shehe | 1,470,000 | 0 | 0 | 30,000 | |
| 2/6 ya 01/01/2023 | | 1,470,000 | 0 | 0 | 30,000 | |
| 5/11 ya 4/11/2022 | Salum Ali Said | 1,544,424 | 0 | 0 | 79,576 | |
| 8/11 ya 10/11/2022 | | 621,954 | 0 | 0 | 32,046 | |
| **Jumla** | | **142,155,217** | **10,030,775** | **331,534** | **3,885,041.28** | |

### 5.1.6 MRADI WA UKARABATI WA NYUMBA ZA MAENDELEO MTEMANI

Shirika la Nyumba Pemba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 lilikadiria kutumia jumla ya shilingi 200,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa Nyumba za Maendeleo Mtemani Wete. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023, Shirika limetumia jumla ya shilingi 157,109,250 sawa na asilimia 78.55 ya makadirio.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.6.1 Malipo ambayo hayakupitia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 19,732,273

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.156/370/01/27 ya tarehe 12/08/2022 kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma inaeleza kuwa "kuanzia tarehe 15/08/2022 manunuzi yote ya Serikali yanatakiwa yafanywe kwa kutumia mfumo wa kielektroniki". Aidha, "Mamlaka inasisitiza changamoto yeyote itakayojitokeza katika matumizi ya mfumo ziwasilishwe Mamlaka haraka iwezekanavyo kwa ajili ya utatuzi".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa jumla ya shilingi 19,732,273 zimelipwa kwa ununuzi wa bidhaa mbali mbali za ujenzi kwa ajili ya ukarabati wa Nyumba za Shirika za Mtemani Wete bila ya kutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (e-Proz).

Kutokutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (e-Proz) kunaweza kupelekea kufanyika kwa ununuzi wa bidhaa kwa gharama kubwa au kununuliwa bidhaa zilizo chini ya kiwango kinachokubalika, aidha ni kwenda kinyume na muongozo wa barua nilliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba kununua bidhaa na huduma kwa kutumia mfumo wa kielektroniki kama sheria inavyoelekeza. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 50: Malipo ambayo hayakutumia mfumo wa ununuzi wa Kielektroniki

| Hati Namba | Hundi Namba | Fedha Zilizolipwa (Ths) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 08/12 ya 20/12/2022 | 000354 | 2,080,737.5 | Abrahman Haji Abdalla | Ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 24/06 ya 28/06/2023 | 000376 | 2,080,737.5 | | |
| 09/05 ya 02/05/2023 | T.T | 2,249,100 | Iddi Hamad Ali | |
| 10/12 ya 20/12/2023 | | 3,957,225 | Ali Khamis Hamad | Malipo ya ufundi kwa awamu tofauti. |
| 28/06 ya 28/06/2023 | | 3,957,225 | | |
| 27/06 ya 28/06/2023 | | 2,703,624 | | |
| 16/06 ya 21/06/2023 | | 2,703,624 | | |
| **Jumla** | | **19,732,273.00** | | |

### 5.1.6.2 Malipo ambayo hayakufuata utaratibu wa utoaji wa zabuni shilingi 53,813,590

Kwa mujibu wa kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma ambayo haiwezi kufuata utaratibu wa sheria hii uliowekwa kwa ununuzi na uondoshaji wa mali za umma, inaruhusiwa kuomba kwa mamlaka kutumia njia au utaratibu mwengine".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 53,813,590 zimelipwa na Shirika la Nyumba Pemba kwa njia ya kuvunjavunja (Splitting) ili kutekeleza mradi wa ujenzi wa Ukarabati wa Nyumba za Mtemani Pemba bila utoaji wa zabuni, hali ambayo inaweza kupelekea kufanya matumizi kwa gharama kubwa, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba kuhakikisha kuwa ununuzi wote unafanyika kulingana na sheria na miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo utoaji wa Zabuni pale kiwango cha makadirio ya matumizi yatakapofikia kiwango kinachohitajika katika utoaji wa zabuni. Mchanganuo wa matumizi hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 51: Malipo ambayo hayakufuata utaratibu wa utoaji wa zabuni

| Hati Namba | Hundi Namba | Fedha | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 03/02 ya 17/01/2023 | T.T | 11,858,000 | Salim Hamdan Maalim | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi |
| 09/05 ya 02/05/2023 | | 2,249,100 | Idd Hamad Idd | |
| 16/05 ya 16/05/2023 | | 2,575,930 | Salim Hamdan Maalim | |
| 14/05 ya 08/05/2023 | | 27,038,200 | Khc Company Limited | |
| 26/06 ya 28/06/2023 | | 13,086,920 | | |
| 30/06 ya 30/06/2023 | | 7,332,360 | | |
| **Jumla** | | **53,813,590** | | |

### 5.1.6.3 Hati za malipo zilizokosa vielelezo shilingi 18,073,649

Kanuni nambari 55(1)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inamtaka "Afisa Masuuli kuhakikisha kwamba malipo yote lazima yawe na vielelezo vilivyokamilika". Aidha, kanuni nambari 57(2)(b) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inamtaka ''Afisa Masuuli kuhakikisha kwamba malipo yote yanaambatanishwa na vielelezo kamili kutokana na matakwa na maelekezo ya Hazina"

Ukaguzi umebaini jumla ya shilingi 18,073,649 zimelipwa kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Nyumba Pemba lakini baadhi ya vielelezo vya matumizi hayo havikuambanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo, aidha ni kwenda kinyume na kanuni nilizozinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Shirika kuhakikisha unaambatanisha vielelezo vyote vya malipo mara tu baada ya malipo kukamilika. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 52: Malipo yenye vielelezo pungufu

| Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 09/05 ya 02/05/2023 | T. T | 2,249,100 | Iddi Hamad Ali | Malipo mbali mbali kwa ajili ya ukarabati wa Nyumba za Maendeleo Mtemani |
| 08/12 | 000354 | 2,080,737.5 | Abrahman Haji Abdalla | |
| 24/06 ya 28/6/2023 | 000376 | 2,080,737.5 | | |
| 09/12 ya 20/12/2012 | T.T | 1,045,000 | Ali Khamis Hamad | |
| 10/12 ya 20/12/2023 | | 3,957,225 | | |
| 28/06 ya 28/6/2023 | | 3,957,225 | | |
| 27/06 ya 28/6/2023 | | 2,703,624 | | |
| **Jumla** | | **18,073,649** | | |

### 5.1.6.4 Kukosekana kwa vielelezo vya uwasilishaji wa Kodi Serikalini shilingi 11,395,727

Kwa mujibu wa kifungu nambari 50(2) cha Sheria nambari 7 ya Usimamizi wa Kodi ya 2009 ambayo imefanyiwa marekebisho mwaka 2020 inaelezea juu ya umuhimu wa kukata kodi na kuiwasilisha serikalini.

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 11,395,727 ni kodi mbali mbali iliyopaswa kukatwa na kuwasilishwa Serikalini inayotokana na malipo yenye jumla ya shilingi 149,227,575 yaliyofanywa kwa watoa huduma mbali kwa ununuzi wa bidhaa na huduma kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za Shirika za Mtemani Wete, ambapo kati ya fedha hizo shilingi 7,956,600 ni VAT ya asilimia 15, shilingi 116,160 ni kodi ya stamp duty ya asilimia 2, na shilingi 3,322,967 ni withholding tax ya asilimia 5.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa vielelezo vinavyothibitisha kuwasilishwa kwa kodi hiyo katika Mamlaka husika jambo ambalo linaweza kupelekea kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi hizo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kukata kodi ya zuio na kuiwasilisha Serikalini kwa mujibu wa utaratibu uliopo. Mchanganuo wa kodi hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 53: Malipo ya kodi yaliyokosa vielelezo vya uwasilishaji

| Hati Namba | Alielipwa | Fedha zilizolipwa (Tshs) | VAT 15% | Stamp Duty 2% | TRA 5% | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3/2 ya 18/01/2023 | Salim Hamdan Maalim | 13,915,000 | 1,815,000 | 0 | 242,000 | Malipo ya ununuzi wa vifaa mbali vya matengenezo ya nyumba za maendeleo Mtemani |
| 8/12 ya 20/12/2022 | Abrahaman Haji Abdalla | 2,190,250 | 0 | 0 | 109,512.50 | |
| 24/6 ya 28/6/2023 | | 2,190,250 | 0 | 0 | 109,512.50 | |
| 9/5 ya 2/5/2023 | Iddi Hamad Ali | 2,700,000 | 0 | 0 | 45,900 | |
| 9/12 ya 20/12/2022 | Ali Khamis Hamad | 1,100,000 | 0 | 0 | 55,000 | |
| 10/12 ya 20/12/2022 | | 4,165,500 | 0 | 0 | 208,275 | |
| 16/6 ya 21/6/2023 | | 2,904,000 | 0 | 58,080 | 142,296 | |
| 27/6 ya 28/6/2023 | | 2,904,000 | 0 | 58,080 | 142,296 | |
| 28/6 ya 28/6/2023 | Ali Khamis Hamad | 3,957,225 | 0 | 0 | 208,275 | |
| 29/6 ya 28/6/2023 | | 1,045,000 | 0 | 0 | 55,000 | |
| 14/5 ya 8/5/2023 | KHC Company Ltd | 31,728,500 | 4,138,500 | 0 | 551,800 | |
| 26/6 ya 28/6/2023 | | 13,354,000 | 2,003,100 | 0 | 267,080 | |
| 30/6 ya 30/6/2023 | | 7,482,000 | 0 | 0 | 149,640 | |
| 19/6 ya 26/6/2023 | Vista General Supplier | 59,591,850 | 0 | 0 | 1,036,380 | |
| **Jumla** | | **149,227,575** | **7,956,600** | **116,160** | **3,322,967** | |

# SURA YA SITA



# 6.0 UKAGUZI WA UFANISI KUHUSIANA NA UNUNUZI WA GARI ZA KUBEBEA WAGONJWA NA USAMBAZAJI WA VIFAA TIBA HOSPITALI

Sura hii inaelezea kuhusiana na miradi ya ununuzi wa gari za kubebea wagonjwa na usambazaji wa vifaa tiba hospitalini ambapo dosari mbali mbali zilibainishwa katika utekelezaji wa miradi hiyo. Miongoni mwa dosari hizo ni kutokuwepo kwa Meneja wa Mradi aliyeteuliwa kwa ajili ya kupokea Vifaa tiba jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa taarifa muhimu za mapokezi ya vifaa tiba vilivyowasilishwa katika hospitali mbali mbali.

## 6.1 Historia ya Mradi

Tarehe 11 Machi 2020, Shirika la Afya Duniani (WHO) lilitangaza rasmi mripuko wa Ugonjwa wa Virusi vya Corona (COVID-19) kuwa ni janga la kimataifa. Kufuatia hatari zilizotarajiwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipokea jumla ya shilingi bilioni 230 kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuweza kukabiliana kikamilifu na athari za janga hilo. Fedha hizo zilipatikana kutoka Shirika Fedha la Duniani (IMF) chini ya Mpango wa Mikopo ya Haraka (RCF).

Mripuko wa UVIKO-19 nchini umesababisha kuongezeka kwa mahitaji ya kupunguza msongamano wa watu hali ambayo iliongeza mahitaji ya ununuzi wa Vifaa tiba katika Hospitali. Ili kudhibiti kuenea kwa virusi vya ugonjwa huo kwa kuimarisha uwezo wa kudhibiti na kuzuia maambukizi.

Kwa mwaka wa fedha 2021, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitenga Shilingi Bilioni 15.9 kwa Sekta ya Afya kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali za Wilaya na Mkoa Unguja na Pemba, Hospitali ya Abdullah Mzee na Mpango wa Damu Salama, Ununuzi wa gari 12 za kubebea wagonjwa, Ununuzi wa Gari 5 za kubebea Dawa kwa ajili ya Bohari Kuu za Dawa Unguja na Pemba, Ununuzi, Usambazaji na ufungaji wa Jenereta pamoja na Usambazaji, Uwekaji na Uanzishaji wa Mitambo ya kuzalishia Oksijeni kwa ajili ya Hospitali za Wilaya na Mkoa Unguja na Pemba.

Hivyo, kutokana na maelezo yaliyotajwa hapo juu, na nia ya Serikali, nilifanya Ukaguzi wa Kiufundi kuhusu Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa Tiba ili kupima thamani halisi ya fedha iliyotumika na kutathmini utekelezaji wa taratibu za ununuzi kama zimefuatwa kikamilifu, kwa kuzingatia hatua za uundaji wa mradi, usanifu wa kiufundi, ufanisi wa usimamizi wa vifaa tiba, udhibiti wa ubora wa Vifaa Tiba, ufadhili wa mradi, usimamizi na utaratibu wa ufuatiliaji.

## 6.2 Malengo ya Ukaguzi

Lengo la ukaguzi huo lilikuwa ni kupitia na kutathmini iwapo Wizara ya Afya imesimamia ipasavyo mchakato wa Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa Tiba ili kuhakikisha kuwa vifaa vyote vinakidhi viwango vya Afya ili kuongeza kasi ya utoaji wa huduma bora za Afya nchini.

Malengo makhsusi ya ukaguzi yalikuwa ni kutathmini kama:-

(a) Upangaji na usanifu wa miradi ya vifaa tiba vya Hospitali za Mkoa na Wilaya ulifanyika ipasavyo ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo;

(b) Taratibu za Ununuzi na Mikataba kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Manunuzi ya Umma na Kanuni zake zilizingatiwa;

(c) Uwasilishaji, ufungaji wa Vifaa Tiba na taratibu za usimamizi wa muda wa mikataba, gharama na ubora vilikuwa katika hali nzuri kulingana na maelezo ya mkataba;

(d) Vifaa Tiba vyote vilizingatia masharti ya mikataba na viwango vya afya; na Ufuatiliaji wa Vifaa Tiba ulifanyika ipasavyo na kuwezesha kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

## 6.3 Upeo wa Ukaguzi

Wizara ya Afya ndio yenye dhamana ya kutunga na kutekeleza sera zinazohusu sekta ya Afya nchini na usimamizi mzima wa ujenzi wa Hospitali, huduma za Afya na ununuzi na usambazaji wa vifaa Tiba. Aidha, Wizara ya Afya ina jukumu la kupanga, kusanifu, ununuzi na usimamizi wa mikataba ya ujenzi wa Hospitali na ununuzi na usambazaji wa Vifaa Tiba.

Ukaguzi huu ulihusisha Miaka miwili ya Fedha kuanzia 2021/2022 hadi 2022/2023 na ilishughulikia awamu zote kuanzia kuanzishwa kwa mradi hadi utekelezaji (Deliver, Installation, test and Commission). Muda huo ulikuwa umechaguliwa ili kuruhusu Ukaguzi kupima kama malengo yaliyokusudiwa ya ununuzi na usambazaji wa vifaa Tiba umefikiwa na kutoa hitimisho na mapendekezo kulingana na matokeo yaliopatikana.

Ukaguzi ulihusisha vipengele vitatu vya usimamizi wa mradi: kupanga na kubuni, mchakato wa ununuzi na utoaji wa Mkataba, na usimamizi wa Mkataba katika suala la ubora, muda, upeo na usimamizi wa gharama. Vipengele hivi vimefafanuliwa zaidi hapa chini:-

## 6.4 Vipengele vya Upangaji na Usanifu

Chini ya kipengele hiki, timu ya ukaguzi ilitathmini, ufanisi wa upembuzi yakinifu, usanifu, na utayarishaji wa Hati za Zabuni ili kuthibitisha ufanisi wa Vifaa Tiba ulioidhinishwa.

### 6.4.1 Vipengele vya Mchakato wa Ununuzi na Utoaji wa Mikataba

Hii ilihusisha kutathmini ni kwa kiasi gani watekelezaji wa mradi walisimamia mchakato wa ununuzi kwa namna ambayo inapunguza gharama na ilikuwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Lengo ni kutathmini kama taratibu za ununuzi na utoaji wa mikataba zilizingatiwa na kufuatwa kama zilivyoainishwa katika Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma, 2016 na Kanuni zake za 2020.

### 6.4.2 Usimamizi wa Muda wa Mkataba, Ubora wa Vifaa, Gharama na Upeo wa Mradi

Chini ya kipengele hiki, ukaguzi ulitathmini utoshelevu wa mifumo na michakato ya kudhibiti muda, gharama na ubora wa mradi. Hii ilijumuisha upangaji wa utekelezaji wa miradi inayohusu tathmini ya mradi, upembuzi yakinifu, usanifu, makadirio ya muda na gharama na vipengele vya kuanzisha mradi. Masuala ya usimamizi wa mikataba, usimamizi na ufuatiliaji wa wazubuni na washauri elekezi, ufungaji wa mradi na ukabidhishwaji wa Vifaa pia vilitathminiwa.

Aidha, Ukaguzi ulitathmini ni kwa kiwango gani watekelezaji walihakikisha kuwa miradi inazingatia mahitaji (specifications) na viwango vya mradi pamoja na kutathmini ubora wa vifaa.

Vile vile, Ukaguzi ulitathmini hali ya ufanisi katika ulipaji na usimamizi wa matumizi ya fedha za miradi iliyopangwa na kuidhinishwa, utoshelevu na ufanisi wa udhibiti wa ndani wa fedha na uzingatiaji wa kanuni elekezi za fedha na masharti ya malipo, **Kiambatisho Nambari 1 Kinahusika.**

## 6.5 Vigezo vya Tathmini, mbinu na Sampuli zilizotumika

Vigezo vya tathmini na mbinu zilizotumika zilitokana na mapitio ya Mikataba, Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 pamoja na maagizo mbalimbali yanayohusu usimamizi wa Fedha za Umma zinazotokana na Mfuko wa ahueni ya UVIKO-19, hata hivyo Ukaguzi ulitumia njia ya Sampuli katika Ukusanyaji wa Taarifa za Ununuzi wa Vifaa Tiba pamoja na matumizi ya mbinu za Uchambuzi wa Taarifa.

Aidha, katika mbinu na Sampuli hizo zilizotumiwa zilijumisha Hospitali zote za Wilaya na moja ya Mkoa ambazo ziliwekwa katika mpango wa Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa Tiba.

Vilevile, Jumla ya Mbinu nne (4) za Ukusanyaji wa Taarifa ziliweza kutumika ikiwemo uhakiki wa nyaraka, mahojiano na utembeleaji wa maeneo ya utekelezaji wa Miradi na upimaji wa kazi zilizokamilika. Mbinu ni kama ilivyoelezwa hapa chini: -

### (a) Uhakiki wa Nyaraka

Ukaguzi ulifanya mapitio ya nyaraka mbalimbali ili kupata na kutathmini utoshelevu wa upangaji/uhitaji wa tathmini, utekelezaji na ufuatiliaji wa mradi. Taarifa zilizokusanywa zilitumika kuthibitisha hali halisi ya utekelezaji wa miradi na kutoa Mapendekezo yatakayopelekea kuongezeka kwa ufanisi wa utekelezaji wa miradi.

Aidha, Ukaguzi ulipitia nyaraka za mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023 ambazo zilihusika katika upangaji wa miradi, ununuzi, kumbukumbu za nyaraka za fedha na nyaraka zinazohusiana na utekelezaji wa miradi. Nyaraka zilizokaguliwa pamoja na sababu za mapitio zimefafanuliwa katika Majadweli hapo chini:

**Jadweli Nambari 54: Mchanganuo wa Gharama, Msambazaji na Hospitali zilizohusika**

| Maelezo | Jina la Msambazaji | Kiasi cha Mkataba |
|---|---|---:|
| Hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe na Kitogani | Lab Equip LTD | 1,364,068,000.00 |
| Hospitali Mpya za Mkoa na Wilaya | Zenj Motors CO Limited | 1,974,324,600.00 |
| Hospitali Mpya za Mkoa na Wilaya | Lab Equip LTD | 1,887,645,770.00 |
| Hospitali ya Wilaya Mwera Pongwe na Kitogani | Lab Equip LTD | 1,364,068,000.00 |
| Hospitali ya Wilaya Pangatupu na Kivunge | Lab Equip LTD | 1,364,068,000.00 |
| Kitengo cha Damu Salama | Nebula Health Care LTD | 90,192,119.00 |
| Hospitali ya Wilaya Micheweni, Kinyasini, Vitongoji, Mbuzini, Chumbuni na Magogoni | M&D Chemicals Surgical LTD | 3,940,818,000.00 |
| Hospitali Mpya za Mkoa na Wilaya | Alpha General Traders Limited | 1,809,548,000.00 |
| Usambazaji, Ufungaji na Uagizaji wa Mitambo ya Oksijeni (Bidhaa) kwa Hospitali mbili za Wilaya, Mwera Pongwe na Vitongoji (Lot No 3) | Hypermedia Healthcare Limited | 862,100,000.00 |

| Maelezo | Jina la Msambazaji | Kiasi cha Mkataba |
|---|---|---|
| Hospitali ya Abdulla Mzee | Edlink | 900,715,000.00 |
| Usambazaji wa gari tano za kubebea dawa za Bohari Kuu, Unguja na Pemba | Africarriers Limited | 354,587,722.60 |
| **Jumla** | | **15,912,135,211.60** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi, 2023*

## Jadweli Nambari 55: Nyaraka zilizopitiwa na Sababu za Mapitio

| Nyaraka zilizokaguliwa | Sababu za Kukaguliwa |
|---|---|
| Ripoti za Usanifu na Mipango | • Usahihi na ukamilifu wa hesabu za makisio<br>• Usahihi na ukamilifu wa maelezo ya kiufundi<br>• Usahihi na ukamilifu wa vipimo vya kiufundi |
| Hati za Mkataba (Nyaraka za Makubaliano, Barua ya Kukubalika, Zabuni ya Mkandarasi, Masharti Maalum ya Mkataba (SCC), Masharti ya Jumla ya Mkataba (GCC), Nyaraka za Makisio ya Gharama za Ujenzi (BoQ), mazungumzo ya kabla ya mkataba) | Kujua masharti yaliyotolewa katika mkataba yanaohusiana na malipo, Tofauti, masuala ya uhifadhi, uharibifu, Kuchelewa kwa Malipo na madai pamoja na kuangalia ikiwa vitu vyote vimewekewa bei. |
| Hati za malipo, Cheti cha malipo ya kukabidhi kazi na kumaliza kazi | Ili kuangalia jumla ya fedha zilizotumika |
| Hesabu za mwisho wa Mwaka | Kuangalia kama hesabu za mwisho za miradi ziliandaliwa kwa usahihi |
| Mpango Kazi | Kuangalia shughuli zilizopangwa ikiwa zimeendana na hali halisi ya utekelezaji kwa kuzingatia kipimo cha muda |
| Ripoti ya Utekelezaji wa mradi | Kuangalia mafanikio na changamoto zilizojitokeza |
| Nyaraka za malipo | Kuangalia jumla ya kiasi cha fedha kilichotumika |
| Maelekezo ya maeneo ya mradi | Kuangalia namna maagizo yaliyotolewa na kuyapima ili kuamua gharama na athari zilizoweza kujitokeza |
| Taarifa za Miradi baina ya Msambazaji na Wizara ya Afya (Correspondence) | Kuangalia masuala yanayohusiana na gharama, wakati na ubora |
| Taarifa za Vipimo za vifaa kabla ya matumizi | Kupata ubora wa bidhaa |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi, 2023*

**(b) Mahojiano**

Ukaguzi ulifanya mapitio ya Nyaraka pamoja na kutembelea maeneo ya utekelezaji wa miradi na kufanya mahojiano na mwakilishi wa mshauri elekezi, Mhandisi wa Wizara, Afisa Masuuli na wajumbe wa Kamati ya Tathmini kutoka Wizara ya Afya ili kuweza kupata ufafanuzi wa kina juu ya utekelezaji wa mradi.

## 6.6 Mbinu za Uchambuzi wa Taarifa

Ukaguzi ulitumia mbinu tofauti katika uchambuzi wa taarifa, kama zifuatazo;

a) Uchambuzi wa maelezo ambapo taarifa zilizopatikana ziliwasilishwa kwa kutumia michoro (pie chart na graph bar) na kuorodheshwa kwenye majadweli.

b) Uchambuzi wa mwenendo ambapo Ukaguzi ulichambuwa mwenendo wa taarifa iliyotolewa katika miaka mbalimbali na kuangalia iwapo taarifa zilizochambuliwa zilikuwa zikipungua au kuongezeka.

Taarifa zilizopatikana kutokana na mahojiano, mapitio ya nyaraka na taarifa zilizobainishwa kutokana na ziara kwenye miradi na upimaji zilichambuliwa kwa kuandaa, kuzilinganisha na kuzihusisha ili kuweza kupata hitimisho la kutosha.

Aidha, Taarifa zenye ubora zilipatikana na kubadilishwa kuwa taarifa kamili kwa kuchambua mahojiano/nyaraka zilizopitiwa na kuona matokeo yake ambapo taarifa hizo ziliweza kuoneshwa kwa asilimia au kwa kutolewa maelezo.

## 6.7 USIMAMIZI WA MIFUMO YA UNUNUZI NA USAMBAZAJI WA VIFAA TIBA

Katika eneo la usimamizi wa mifumo ya ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba ukaguzi umeelezea kwa kina kuhusiana na uwekaji na usimamizi wa mifumo katika majengo mapya ya Hospitali za Mkoa na Wilaya kwa Unguja na Pemba.

**Sheria Husika**

Sheria na kanuni mbalimbali zinaongoza ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba kama zilivyoelezwa hapa chini: -

### 6.7.1 Sheria na Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma

Sheria mbali mbali na miongozo inayosimamia ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba Zanzibar kama zilivyowasilishwa katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 56: Sheria ya Udhibiti wa Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa Tiba**

| Sheria | Utekelezaji |
|---|---|
| Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 | Sheria hueleza miongozo ya kufuatwa kipindi cha ununuzi, utekelezji wa mradi na kupaswa kutumia kwa Afisa Masuuli |
| Sheria Nambari 8 ya Usimamizi wa Kodi ya 2019 iliyofanyiwa maboresho | Miongozo inayohusiana na kodi |
| Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 | Miongozo inahusiana na fedha na mamlaka yake |

*Chanzo:Mapitio ya Sheria, 2023*

### 6.7.2 Kanuni zinazosimamia udhibiti wa gharama

Kanuni mbali mbali za udhibiti wa gharama katika ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba zimetumika kama ilivyoelezwa kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 57: Kanuni zinazosimamia Ununuzi na Usambazaji Vifaa Tiba**

| Kanuni | Utekelezaji | Taasisi inayowajibika |
|---|---|---|
| Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 | Kanuni zinaeleza kuwa taasisi zote za ununuzi zinapaswa kutunza taarifa zote, nyaraka na tafiti zote zinazohusiana na miradi. | Mamlaka ya Ununuzi na uondoshaji wa Mali za Umma |
| Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 | Kanuni zinaeleza kuwa maandalizi na udhibiti wa bajeti, taasisi zinapaswa kudumisha taarifa zote na nyaraka zinazohusiana na masuala ya fedha. Pia inasisitiza kuwa sehemu ya uhasibu na usimamizi inapaswa kuhakikisha malipo yanafanywa kwa wakati. | Ofisi ya Raisi Fedha na mipango |

*Chanzo: Uchambuzi wa kanuni uliofanywa na wakaguzi, 2023*

### 6.7.3 Majukumu na wajibu wa Wahusika wa Mradi

Wizara ya Afya ndiyo mhusika mkuu mwenye dhamana ya kusimamia ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba kwa hospitali na vituo vya afya nchini. Ina jukumu la kuratibu, ufuatiliaji na tathmini ya mchakato mzima wa Ununuzi na usambazaji wa Vifaa Tiba.


Taasisi shiriki mbalimbali zinazohusika katika Ununuzi na Usambazajii wa Vifaa Tiba ni Afisi ya Rais-Fedha na Mipango, Wizara ya Afya na Watoa Huduma kama ilivoelezwa kwa kina katika picha hapo chini: -

**Picha Nambari 4: Wadau wanaohusika katika Ununuzi na Usambazaji Vifaa Tiba**

| | |
|---|---|
| **Wizara ya Afya** | • Inawajibika katika kufanya upembuzi yakinifu, Maandalizi ya vipimo vya kiufundi, maandalizi ya Nyaraka za mkataba,mgao wa fedha kwa ajili ya vifaa Tiba, Ununuzi wa wasambazaji na Washauri, na Usimamizi wa utekelezaji wa miradi hiyo. Pia, wanajukumu la kuwalipa wazabuni na washauri elekezi kuhusiana na kazi iliyotekelezwa. |
| **Wasambazaji** | Wanawajibika katika usambazaji wa vifaa tiba kwa mujibu wa nyaraka za Mkataba. Kazi yao ilikuwa kuhakikisha vifaa tiba hutolewa kwa mujibu wa sheria na masharti ya Mikataba. |
| **Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma** | Inawajibika katika kuhakikisha kuwa sheria na Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za umma zinazingatiwa. |

### 6.7.4 Taratibu za Kusimamia Usambazaji wa Vifaa Tiba

Ununuzi na usambazaji wa Vifaa tiba hufuata hatua zote za utoaji wa mradi ambazo ni uanzishaji na upangaji/kubuni, ununuzi, uwasilishwaji wa bidhaa, ufungaji wa vifaa, ukaguzi na majaribio, kukamilika kwa mradi na kufungwa kwa mradi; na uendeshaji na matengenezo ya Vifaa tiba. Maelezo ya kila hatua yameonyeshwa kwenye Picha hapo chini:-




### 6.7.5 Utendaji wa Kifedha

Katika mwaka wa ukaguzi, Wizara ya Afya Zanzibar ilikuwa na jumla ya kiasi cha fedha cha shilingi 7,243,127,073.64 zilizopokelewa kutoka Afisi ya Rais fedha na Mipango kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba, ununuzi wa gari za kubebea wagonjwa (12) na gari 5 za kubebea dawa kwa ajili ya Bohari Kuu ya Dawa na usambazaji na ufungaji wa mtambo wa kuzalishia oksijini (Oxygen plant) katika Hospitali ya Wilaya ya Mwera Pongwe na Vitongoji Pemba. Hadi tarehe 30 Juni, 2023, Wizara ilitumia shilingi 7,243,127,073.64 sawa na asilimia 100 kama iinavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 58: Utendaji wa Kifedha**

| Maelezo | Kiasi (Sh) |
|---|---|
| Fedha zlizoingizwa mwanzo wa mwaka kwa tarehe 1/7/2022 | 0 |
| **Ongezeko:** Fedha zilizopokelewa wakati wa mwaka | 7,243,127,073.64 |
| Jumla ya fedha zinazopatikana wakati wa mwaka | 7,243,127,073.64 |
| **Punguza:** Jumla ya Matumizi kwa mwaka | **7,243,127,073.64** |
| **Salio lililobaki hadi tarehe 30/06/2023** | 0 |

*Chanzo: Taarifa ya mapokezi na Matumizi, 2023*

### 6.7.6 Utekelezaji wa Mradi

Mnamo Julai 2022, Wizara ya Afya Zanzibar iliingia makubaliano ya kimkataba ya usambazaji wa vifaa tiba kwa Hospitali mpya za Wilaya na Mikoa zilizojengwa, Ununuzi wa gari za kubebea wagonjwa, Ununuzi wa gari za kubebea dawa kwa Bohari Kuu ya Dawa (CMS) Unguja na Pemba na Hospitali Abdullah Mzee ya Mkoa wa Kusini Pemba.

Meneja wa mradi ilikuwa ni Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi (PMU) kutoka wizara Afya. Miradi yote ilitakiwa kukamilika ndani ya miezi sita, kuanzia tarehe ya kusainiwa kwa Mkataba. Upeo wa kazi ulihusisha ununuzi wa gari za kubebea wagonjwa (10) na gari za kubebea dawa (5), ununuzi na usambazajii wa vifaa tiba kwa hospitali mpya za Unguja na Pemba na Hospitali ya Abdullah Mzee Pemba na ununuzi na usambazaji wa Jenereta kwa hospitali za Wilaya na Mikoa Unguja na Pemba. Hali ya utekelezaji wa miradi hadi kufikia Juni, 2023 imetolewa kwa muhtasari katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 59: Hali halisi ya utekelezaji wa Mradi

| Jina la Mradi | Idadi ya Miradi | Miradi iliokamilika | Miradi inayoendelea | Miradi iliyokuwa haijaanza |
|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa gari 12 za kubebea wagonjwa kwa hospitali mpya zilizojengwa Unguja na Pemba | 10 | 10 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya bohari Kuu (CMS) kwa Unguja na Pemba | 5 | 5 | 0 | 0 |
| Ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba kwa hospitali mpya zilizojengwa katika Hospitali za Unguja na Pemba na Abdullah Mzee Pemba | 12 | 3 | 9 | 0 |
| Ununuzi na Usambazaji wa Jenereta kwa hospitali mpya zilizojengwa Unguja na Pemba | 20 | 10 | 0 | 10 |
| Usambazaji na ufungaji wa mtambo wa Oksijini katika Hospitali ya Wilaya ya Mwera Pongwe na Vitongoji | 2 | 0 | 1 | 1 |
| Utoaji wa vifaa tiba kwa ajili ya huduma za kuongezewa damu | 1 | 1 | 0 | 0 |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Taarifa ya Maendeleo, 2023*

Ukaguzi huu ulipitia jumla ya miradi (10) ambayo imetekelezwa na Wizara ya Afya, ambapo mradi mmoja ni ununuzi wa gari kumi na mbili (12) za kubebea wagonjwa, gari tano (5) za kubebea dawa pamoja na mradi wa ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba kama inavyofafanuliwa katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 60: Miradi iliyokaguliwa

| Jina la mradi | Idadi ya miradi | Miradi iliyokamilika | Miradi inayoendelea | Miradi iliyokuwa haijaanza kutekelezwa |
|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa gari 12 za kubebea wagonjwa kwa hospitali mpya zilizojengwa Unguja na Pemba | 12 | 12 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya bohari kuu (CMS) kwa Unguja na Pemba | 5 | 5 | 0 | 0 |
| Ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba kwa hospitali mpya zilizojengwa katika Hospitali za Unguja na Pemba na Abdullah Mzee Pemba | 12 | 3 | 9 | 0 |
| Ununuzi na Usambazaji wa Jenereta kwa hospitali mpya zilizojengwa Unguja na Pemba | 20 | 10 | 0 | 10 |
| Usambazaji na ufungaji wa mtambo wa Oksijini katika Hospitali ya Wilaya ya Mwera Pongwe na Vitongoji | 2 | 0 | 1 | 1 |
| Usambazaji wa vifaa tiba kwa ajili ya huduma za kuongezewa damu | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa gari za kubebea wagonjwa kwa hospitali mpya zilizojengwa Unguja na Pemba | 10 | 10 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa vifaa tiba kwa ajili ya Bohari kuu ya Dawa (CMS) kwa Unguja na Pemba | 5 | 5 | 0 | 0 |
| Ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba kwa hospitali mpya na Hospitali ya Abdullah Mzee Pemba | 1 | 1 | 0 | 0 |

| Jina la mradi | Idadi ya miradi | Miradi iliyokamilika | Miradi inayoendelea | Miradi iliyokuwa haijaanza kutekelezwa |
|---|---|---|---|---|
| Ununuzi na Usambazaji wa Jenereta kwa hospitali mpya zilizojengwa Unguja na Pemba | 20 | 10 | 0 | 10 |

*Chanzo: Uchambuzi wa Taarifa za Miradi ya Maendeleo uliofanywa na wakaguzi, 2023*

Hata hivyo, ukaguzi ulijumuisha mapitio ya miamala ya fedha, udhibiti wa ndani na uendeshaji kwa kiwango kinachoonekana ni muhimu kwa ufanisi wa ukaguzi ili kutoa maoni kwa kiasi halisi cha mkataba kilicholipwa na kiasi halisi cha nyongeza ya mkataba kwa kazi zilizoongezeka, zilizotolewa na zilitayarishwa kama nyongeza (addendum) ipasavyo kwa mujibu wa makubaliano ya kimkataba, **Kiambatisho Nambari 2 Kinahusika.**

**Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na Upangaji wa usambazaji wa vifaa Tiba**

**6.7.6.1 Kutokuwepo kwa Meneja wa Mradi aliyeteuliwa kwa ajili ya kupokea Vifaa**

Ukaguzi ulipitia mchakato wa utekelezaji wa mradi na kubaini kuwa hakukuwa na msimamizi wa mradi aliyeteuliwa kupokea vifaa vilivyotolewa ili kuhakikisha uwepo kwa usimamizi mzuri kulingana na mahitaji ya mkataba na kubaini kuwa mfumo uliopo wa upokeaji wa bidhaa kwenye eneo la mradi haukusimamiwa vizuri ili kuepusha uhamishaji wa jukumu (dhamana) kutoka kwa mzabuni kwenda kwa Wizara itapotokea migogoro.

Aidha, ukaguzi umebaini miradi ya usambazaji wa vifaa tiba haikua na msimamizi (manager) aliyopo kwenye mradi ambapo atawajibika moja kwa moja kwa kutokana na usambazaji wa vifaa tiba katika sehemu zinazohusika jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa uratibu, kuchelewa kufanya maamuzi na ufuatiliaji duni wa shughuli za mradi na hatimae kuathiri mafanikio ya jumla ya mradi na uwezo wa kufikia hatua muhimu.

Wizara ya Afya ilijibu kuwa, Bohari kuu ya Dawa iliteuliwa kusimamia masuala ya kiufundi kuhusu usambazaji wa vifaa tiba, hata hivyo ukaguzi umebaini kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba Wizara ilipaswa kumteua Afisa maalum ambae angekuwa na jukumu la kusimamia masuala yote yanayohusiana na vifaa tiba jambo ambalo hadi ukaguzi unakamilika Wizara imeshindwa kutekeleza matakwa ya mkataba ya usimamizi wa mradi.

Kutokana na kushindwa kutekeleza matakwa ya mkataba imepelekea Wizara kutokuwa na mipango mizuri ya kuhakikisha kuwa uwasilishaji wa bidhaa unasimamiwa ipasavyo ili kuepusha dosari zinazoweza kujitokeza kwenye eneo la mradi.

Kutokana na dosari hiyo ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara kuhakikisha unakwenda sambamba na matakwa ya mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa ongezeko la gharama za mradi zitakazosababishwa na usimamizi duni wa kutokuwepo kwa meneja wa mradi.

#### 6.7.6.2 Kukosekana kwa Mipango Iliyojitosheleza ya upatikanaji wa vipuri vya Mradi

Kanuni nambari 22(2) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inaeleza Masharti yoyote, vipimo, mipango, michoro, usanifu na mahitaji au maelezo ya bidhaa, ujenzi au huduma yatazingatia lengo husika, sifa za kiufundi na ubora wa bidhaa, ujenzi au huduma zitakazonunuliwa.

Ukaguzi ulipitia nyaraka za mikataba ya miradi yote ili kutathmini uwepo wa utayarishaji wa masharti ya mkataba na kubaini kuwa hakukuwa na maandalizi ya kutosha ya masharti maalumu ya mkataba wa usambazaji wa vifaa tiba. Kifungu cha 16.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba kinaeleza kuwa vipuri vya ziada vinahitajika, mtoa huduma anatakiwa kujua idadi ili kuhakikisha usambazaji wa awali wa vipuri vinavyoweza kutumika kwa bidhaa. Hata hivyo, muda uliowekwa maalumu kwa ajili ya upatikanaji wa vipuri baada ya kuagiza ni miezi 6 ambapo ukaguzi umeona muda huo ni mkubwa kulinganisha na mahitaji ya vifaa tiba vinavyohitajiwa kwa huduma za hospitali.

Hali hii imechangiwa na kutoandaliwa ipasavyo kwa mahitaji ya usimamizi wa mradi ambapo Wizara ilitakiwa kupima umuhimu wa vifaa katika utoaji wa huduma za afya kwa muda ambapo upatikanaji wa haraka wa vipuri wa vifaa tiba utatekelezwa.

Aidha, kuendelea kusubiria vifaa kwa muda mrefu pindipo vitakapoharibika kunaweza kupelekea hospitali kushindwa kutoa baadhi ya huduma za matibabu kutokana na kusubiri kwa muda mrefu upatikanaji wa vipuri na hatimae kupelekea usumbufu kwa wananchi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa unatoa ratiba na mahitaji ya kutosha kulingana na umuhimu wa hali hiyo na vile vile kuhakikisha vipuri vya ziada vinapatikana ili kufupisha muda wa uagiziaji na kuboresha uendelevu wa utoaji huduma.

#### 6.7.6.3 Maandalizi yasiyoridhisha ya Mpango wa Malipo ya Usambazaji wa Vifaa Tiba

Ukaguzi ulipitia hati ya mkataba wa usambazaji wa vifaa tiba na kutathmini namna ya makubaliano ya malipo ya ununuzi na usambazaji wa vifaa tiba na kubaini uwepo wa maandalizi yasiyoridhisha na yasiyo salama kwa fedha ya Serikali ambapo imebainika uwepo wa bidhaa hufanyiwa malipo ya asilimia 70 hadi 90 kabla ya bidhaa hizo kupokelewa na kufanyiwa ukaguzi wa kitaalamu wa ubora wa vifaa vilivyowasilishwa. Hali hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 61: Asilimia ya Malipo ya Usambazaji wa Vifaa Tiba**

| Jina la Mradi | Asilimia ya Malipo ya Awali | Asilimia ya Usafirishaji | Asilimia ya Kukubalika | Asilimia ya Udhamini | Asilimia ya Malipo ya Awali na Usafirishaji |
|---|---|---|---|---|---|
| Usambazaji wa gari za wagonjwa | 0 | 0 | 100 | - | |
| Usambazaji wa vifaa vya hospitali | 30 | 50 | 18 | 2 | 80 |
| Usambazaji wa bidhaa za afya kwa hospitali ya Pangatupu na Kivunge | 20 | 50 | 28 | 2 | 70 |
| Usambazaji wa vifaa tiba kwa ajili ya hospitali mpya ya Mkoa iliyopo Lumumba | 20 | 50 | 28 | 2 | 70 |
| Usambazaji wa bidhaa za afya kwa hospitali za Mwera Pongwe na Kitogani | 30 | 50 | 18 | 2 | 80 |
| Usambazaji na ufungaji wa jenereta kwa hospitali zote za wilaya | 30 | 50 | 18 | 2 | 80 |
| Usambazaji wa vifaa vya kusafishia damu kwa hospitali | 30 | 50 | 18 | 2 | 80 |
| Usambazaji wa vifaa vya hospitali | 30 | 50 | 18 | 2 | 80 |
| Usambazaji wa Mtambo wa oksijeni | 30 | 60 | 8 | 2 | 90 |
| Usambazaji wa gari 5 | 20 | 50 | 28 | 2 | 70 |

*Chanzo: Uchambuzi wa nyaraka za mkataba kutoka kwa wakaguzi*

Jadweli hapo juu linaonesha kuwa mikataba 3 ilitolewa kwa vigezo kuwa Wizara atatoa malipo ya asilimia 70 kwa mzabuni wakati wa usafirishaji na utoaji wa bidhaa, vile vile imebainika wazabuni 6 walifanyiwa malipo kwa zaidi ya asilimia 80 hadi 90 baada ya usafirishaji na utoaji wa bidhaa.

Kutokana na hali hiyo, kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma au ucheleweshwaji wa upatikanaji wa huduma pindipo mzabuni atawasilisha vifaa visivyo na ubora au vilivyokuwa havikukidhi viwango vya kitaalamu vya matumizi ya vifaa hivyo.

Ukaguzi unaushauri uonogozi wa Wizara ya Afya kuwa makini wakati wa upangaji wa malipo ya usambazaji wa vifaa tiba ili uweze kuendana na uhalisia wa upokeaji, uchunguzi na ukubalifu wa vifaa vilivyowasilishwa kwa mujibu wa utaratibu.

Hata hivyo ni vyema kuhakikisha wasambazaji waliopewa zabuni ya usambazaji wa vifaa tiba wanawasilisha hati ya dhamana kabla ya kuingia makubaliano ya mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa hasara itakayopatikana pindipo mzabuni atakaposhindwa kuendana na matakwa ya mkataba husika.

### 6.7.6.4 Malipo ya awali yaliyofanyika kabla ya kuwasilisha hati ya dhamana ya benki (advance payment guarantee) shilingi 4,382,391,774.22

Kwa mujibu wa Sehemu ya 18 ya Masharti Maalum ya Mkataba inasema malipo ya awali yatakuwa katika asilimia iliyotajwa katika mikataba ya mtu binafsi na yatalipwa baada ya kuwasilisha hati ya Dhamana ya Benki ya Malipo ya Awali.

Ukaguzi ulipitia taarifa za mawasiliano na kubaini kupitia tathmini za hatari zinazoweza kutokea na athari zinazohusiana na mpangilio huo wa malipo. Matokeo yanaonesha kuwa kukosekana kwa hati dhamana ya malipo ya awali kwa wahusika wote kwa mlipaji na mpokeaji inaathari mbalimbali za kifedha, kimkataba na kiutendaji.

Miamala ya malipo ina jukumu muhimu katika shughuli za kibiashara, kuhakikisha ubadilishaji wa bidhaa, huduma na fedha kati ya wahusika. Kutokuwepo kwa hati dhamana ya malipo ya awali katika malipo makubwa kunatia wasiwasi kuhusu udhaifu unaowezekana katika mchakato wa malipo kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.

## Jadweli Nambari 62: Malipo ya Awali yaliyofanywa bila Hati ya Malipo ya Awali

| Namba | Mzabuni | Mradi | Kiasi cha Mkataba (Sh) | Malipo ya Awali yaliyofanyika (Sh) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Zenji Motor | Usambazaji wa gari za wagonjwa | 1,974,324,600 | 789,729,840 |
| 2 | M&D Chemical & Surgical Ltd | Vifaa vya Hospitali | 3,940,818,000 | 1,182,245,400 |
| 3 | Lab Equipment Ltd | Usambazaji wa Bidhaa za Afya kwa Hospitali ya Pangatupu na Kivunge | 1,364,068,000 | 409,220,400 |
| 4 | Lab Equipment Ltd | Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa Hospitali Mpya ya Mkoa Lumumba | 1,887,645,770 | 377,529,154 |
| 5 | Lab Equipment Ltd | Usambazaji wa Bidhaa za Afya kwa Hospitali za Mwera Pongwe na Kitogani | 1,364,068,000 | 272,813,600 |
| 6 | Alpha General Trader Ltd | Usambaaji na Ufungaji wa Jenereta kwa Hospitali zote za Wilaya | 1,809,548,000 | 723,819,200 |
| 7 | Nebula Healthcare | Vifaa vya kusafishia damu vya Hospitali | 90,192,119 | 27,057,635.70 |
| 8 | Edlink | Vifaa vya Hospitali | 900,715,000 | 270,214,500 |
| 9 | Hypermade | Usambazaji wa mtambo wa Oksijini (oxygen Plant) | 862,100,000 | 258,844,500 |
| 10 | Africarriers Ltd | Usambazaji wa gari 5 | 354,587,722.60 | 70,917,544.52 |
| **Jumla** | | | **14,548,067,211.6** | **4,382,391,774.22** |

*Chanzo: Uchambuzi wa kumbukumbu za malipo uliofanywa na Wakaguzi, 2023.*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa kulikuwa na malipo ya shilingi 4,382,391,774.22 ya awali bila kuwepo kwa hati ya dhamana ya malipo ya awali kama inavyotakiwa na mkataba.

Hii imechangiwa na usimamizi duni wa mradi na wizara na pia usimamizi wa mkataba kabla ya malipo kutolewa. Kutokuwepo kwa masharti ya wazi ya hati ya dhamana ya malipo ya awali kunaweza kusababisha migogoro kati ya wahusika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba unazingatia masharti ya kimkataba wakati wa utekelezaji wa miradi.

### 6.7.6.5 Kukosekana kwa Mpango wa Mafunzo kwa wasimamizi wa Vifaa

Kwa mujibu wa kifungu nambari 15 cha Masharti Maalum ya Mkataba kinasema Masuala ya matukio yatabainishwa katika mkataba na masuala yote ya ziada yatatayarishwa na Wizara kwa usaidizi wa makubaliano kutoka pande zote. Hata hivyo, Masharti ya Jumla ya Mkataba yanafafanua kuwa masuala ya dharura yatajumuisha mafunzo ya wafanyakazi wa Wizara wakati wa ufungaji na wakati wa uangalizi (udhamini).

Ukaguzi ulipitia vifungu vyote vya mkataba kwenye gharama za usambazaji wa vifaa ili kutathmini uwajibikaji wa mafunzo ya wafanyakazi wa Wizara na kubaini kuwa mikataba hiyo haikujumuisha gharama za mafunzo.

Hali hii imechangiwa na tathmini isiyokidhi ya mahitaji kabla ya kusainiwa kwa mkataba, kutotimiza wajibu ipasavyo kwa Bodi ya Zabuni ambayo ilitakiwa kupitia na kuidhinisha nyaraka za zabuni kabla ya zabuni hiyo kutolewa.

Kutokupatiwa mafunzo kwa wasimamizi wa vifaa hivyo kunaweza kupelekea kushindwa kuvitumia kwa ufanisi au kujitokeza kwa matumizi yasiyo ya lazima ya fedha kwa kumtafuta mtaalamu pindipo dosari yoyote inapoweza kujitokeza katika vifaa hivyo.

Kutokana na umuhimu wa mafunzo kwa watumiaji na wasimamizi wa vifaa vilivyonunuliwa na kufungwa ukaguzi unaushauri uongozi kuhakikisha kuwa timu ya Wizara imepewa ujuzi na uelewa unaohitajika ili kusimamia, kuendesha na kudumisha kituo kilichojengwa kwa ufanisi.

## Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa Tiba

Sehemu hii inaelezea utaratibu wa ununuzi kuanzia hatua ya upangaji hadi utoaji wa mkataba wa hatua tofauti. Taratibu nyingi za ununuzi zilizingatia muongozo wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma huku kukiwa na kasoro chache kama ilivyoonekana hapa chini:

### 6.7.6.6 Nyaraka ya Zabuni ya Usambazaji, Ufungaji na Ukabidhishaji wa vifaa tiba ilitolewa kabla ya Idhini ya Bodi ya Zabuni

Kanuni ya 45(1) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma GN.6890 ya 2020 inaitaka Bodi ya Zabuni kuidhinisha rasimu ya nyaraka za zabuni kabla ya kuidhinisha suala la zabuni.

Baada ya kukagua nyaraka zinazohusiana na zabuni ya "Usambazaji, Ufungaji na Uagizaji wa Vifaa Tiba", imebainika kuwa hati ya zabuni ilitolewa kabla ya kupata idhini inayohitajika kutoka kwa Bodi ya Zabuni. Ukiukaji huu kutoka kwa mchakato ulioanzishwa wa ununuzi unaibua wasiwasi kuhusu uwazi, uwajibikaji, na uzingatiaji utaratibu wa udhibiti wa Bodi ya Zabuni, kuwa ni chombo kinachosimamia na kuidhinisha shughuli za ununuzi, ina jukumu muhimu katika kuhakikisha usawa, ushindani, na kufuata sheria na kanuni zinazotumika.

Kutoa hati ya zabuni kabla ya kupata idhini kunadhoofisha uadilifu wa mchakato wa ununuzi na inaweza kusababisha madai ya upendeleo au kutendewa isivyo haki.

Katika ukaguzi wa kumbukumbu za ununuzi na kuwasilisha kwa kumbukumbu za kikao cha Bodi ya Zabuni, hapakuwa na ushahidi wowote ulioonyesha kwamba rasimu iliwasilishwa kwa bodi ya zabuni kwa ajili ya ukaguzi na uidhinishaji.

Kutoa hati ya zabuni kabla ya kuidhinishwa kunaweza kupelekea hatari ya kutoa hati za zabuni ambazo hazikuelezea mahitaji yote yanayohitajika katika Usambazaji, Uwekaji na Uagizaji wa Vifaa tiba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafuata matakwa ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

### 6.7.6.7 Ongezeko la gharama za mkataba kwa shilingi 2,828,703,369

Kwa mujibu wa utaratibu ulivyofanywa na Bohari ya Dawa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (MSD). Ulinganishi wa bei kwa wazabuni ambao wanazingatia vigezo vyote. Hii imefanywa kwa sababu vifaa tiba ni maalum, ni ngumu kupata wazalishaji walioidhinishwa ambao wanaweza kuwasilisha ofa kwa vitu vingi na kuepuka kupata wauzaji ambao ni wa kati na wanaweza kutoa bei kubwa na ubora wa wenye shaka.

Mapitio ya ripoti ya tathmini ya usambazaji, ufungaji na uandaaji wa vifaa tiba katika hospitali 10 za wilaya, Hospitali ya Abdullah Mzee Mkoani, na Hospitali ya Mkoa ya Lumumba ilibaini kuwa ulinganishi wa bei kwa wazabuni waliotoa mahitaji ulifanyika, na mkataba wa jumla wa loti 1, 2, 3, 4, 5 na 6 ilifanyika kwa kuzingatia jumla ya kila mzabuni kwa kila eneo na si kwa kila kipengele kama inavyofanywa na Bohari ya Dawa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (MSD).

Hivyo, bei za mikataba ziliongezeka kwa shilingi 2,828,703,369 kwa sababu baadhi ya wazabuni waliopewa tuzo walikuwa na bei za juu licha ya kuwa ndiyo waliochaguliwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafanya ulinganisho wa bei kwa kila bidhaa wakati wa kufanya tathmini ili kuweza kunusuru upotevu mkubwa wa fedha za umma.

### 6.7.6.8 Ongezeko la Gharama za Mkataba kutokana na kutokuzingatiwa kwa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) wakati wa ulinganishaji wa bei shilingi 165,050,700

Kanuni ya 127 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 mzabuni mwenye zabuni iliokizi vigezo zaidi kwenye tathmini kuwa mzabuni aliyeshinda.

Mapitio ya ripoti ya tathmini, barua ya taarifa ya kupata zabuni na ukaguzi wa mkataba ulibaini kuwa Wizara ya Afya iliingia makubaliano na M/S M&D Chemical and Surgical Limited kwa loti 2 na 5.

Aidha, ilibainika kuwa wakati wa tathmini kamati ya tathmini ilifanya ulinganisho wa bei chini ya dhana hiyo, kwamba bei zilizotolewa zilijumuisha VAT kwa wasambazaji wote. Hata hivyo, ukaguzi uligundua kuwa bei iliyotolewa na M&D Chemical and Surgical Limited haikujumuisha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 63: Ulinganisho wa bei baada ya kujumuisha VAT kwa Bei inayotolewa na msambazaji bila kujumuisha VAT

| Namba | Jina la Mkandarasi | Bei iliyonukuliwa (Tshs) | Bei iliyosahihishwa (Tshs) | Mlinganisho wa Bei |
|---|---|---|---|---|
| **Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa Hospitali 3 za Wilaya Mjini Magharibi (Chumbuni, Magogoni na Mbuzini) - Unguja- Lot 2** | | | | |
| 1 | M&D Chemical & Surgical Ltd | 1,967,409,000 | 2,262,520,350 | 2 |
| 2 | KATMED Group (T) Limited | 2,183,445,000 | 2,183,445,000 | 1 |
| 3 | Comptech-ICS (T) Limited | 4,486,373,156 | 4,486,373,156 | 6 |
| 4 | Lab Equip Ltd | 2,066,346,000 | 2,376,297,900 | 3 |
| 5 | Indepth Scientific Company Limited | 4,513,288,264 | 4,513,288,264 | 7 |
| 6 | Labtech Tanzania Limited | 3,090,734,738 | 3,090,734,738 | 4 |
| 7 | SCIEX | 5,276,729,850 | 5,276,729,850 | 8 |
| 8 | Comfix Engineering | 4,029,383,500 | 4,029,383,500 | 5 |
| **Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa Hospitali za Wilaya 3 za Mkoa wa Kaskazini (Kinyasini, Vitongoji na Micheweni) Pemba - Lot 5** | | | | |
| 1 | M&D Chemical & Surgical Ltd | 1,973,409,000 | 2,269,420,350 | 2 |
| 2 | KATMED Group (T) Limited | 2,183,445,000 | 2,183,445,000 | 1 |
| 3 | Comptech-ICS (T) Limited | 4,486,373,156 | 4,486,373,156 | 5 |
| 4 | Lab Equip Ltd | 2,066,346,000 | 2,376,297,900 | 3 |
| 5 | Indepth Scientific Company Limited | 4,513,288,264 | 4,513,288,264 | 7 |
| 6 | Labtech Tanzania Limited | 3,091,451,018 | 3,091,451,018 | 3 |
| 7 | SCIEX | 5,276,729,850 | 5,276,729,850 | 8 |
| 8 | Comfix Engineering | 3,964,281,000 | 3,964,281,000 | 5 |

*Chanzo: Uchambuzi wa Ripoti ya Tathmini, Taarifa na Mkataba*

Ukaguzi ulibaini kuwa, mzabuni bora aliyetathminiwa kwa loti 2 na 5 alitakiwa M/S KATMED Group (T) Limited badala ya M/S M&D chemical & Surgical Ltd. Matokeo yake, bei za mkataba za loti namba 2&5 ziliongezeka kwa shilingi 165,050,700 (4,531,940,700-4,3060,800) kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

## Jadweli Nambari 64: Ulinganishi wa bei kwa Aliyepewa na mzabuni aliyetathminiwa vyema

| Namba | Jina la Mkandarasi | Bei iliyonukuliwa (Tshs) | Bei iliyosahihishwa (Tshs) | Mlinganisho wa Bei |
|---|---|---|---|---|
| **Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa Hospitali 3 za Wilaya Mjini Magharibi (Chumbuni, Magogoni na Mbuzini) - Unguja- Lot 2** | | | | |
| 1 | M&D Chemical & Surgical Ltd | 1,967,409,000 | 2,262,520,350 | 2 |
| 2 | KATMED Group (T) Limited | 2,183,445,000 | 2,183,445,000 | 1 |
| 3 | Comptech-ICS (T) Limited | 4,486,373,156 | 4,486,373,156 | 6 |
| 4 | Lab Equip Ltd | 2,066,346,000 | 2,376,297,900 | 3 |
| 5 | Indepth Scientific Company Limited | 4,513,288,264 | 4,513,288,264 | 7 |
| 6 | Labtech Tanzania Limited | 3,090,734,738 | 3,090,734,738 | 4 |
| 7 | SCIEX | 5,276,729,850 | 5,276,729,850 | 8 |
| 8 | Comfix Engineering | 4,029,383,500 | 4,029,383,500 | 5 |
| **Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa Hospitali za Wilaya 3 za Mkoa wa Kaskazini (Kinyasini, Vitongoji na Micheweni) Pemba - Lot 5** | | | | |
| 1 | M&D Chemical & Surgical Ltd | 1,973,409,000 | 2,269,420,350 | 2 |
| 2 | KATMED Group (T) Limited | 2,183,445,000 | 2,183,445,000 | 1 |
| 3 | Comptech-ICS (T) Limited | 4,486,373,156 | 4,486,373,156 | 5 |
| 4 | Lab Equip Ltd | 2,066,346,000 | 2,376,297,900 | 3 |
| 5 | Indepth Scientific Company Limited | 4,513,288,264 | 4,513,288,264 | 7 |
| 6 | Labtech Tanzania Limited | 3,091,451,018 | 3,091,451,018 | 3 |
| 7 | SCIEX | 5,276,729,850 | 5,276,729,850 | 8 |
| 8 | Comfix Engineering | 3,964,281,000 | 3,964,281,000 | 5 |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi wa Ripoti ya Tathmini, Taarifa na mkataba wa sehemu ya 2 &5*

Kushindwa kujiridhisha kwa Kamati ya Tathmini juu ya usawa wa bei iliyotolewa na mzabuni na uhakiki usioridhisha kwenye kitengo cha Manunuzi ulipelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama za shilingi 165,050,700 kwa kumchagua mzabuni aliyekosa sifa ya ushindani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unaongeza umakini wakati wa kufanya tathmini ili kuepusha kujitokeza kwa ongezeko la gharama zisizo na tija katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

### 6.7.6.9 Kamati ya Tathmini haikutia saini hati za kiapo

Kanuni ya 118 (6) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inaitaka Kamati ya Tathmini kusaini hati za kiapo kama zilivyoainishwa katika Jadweli la Sita la Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020.

Mapitio ya ripoti za tathmini ya zabuni za usambazaji wa vifaa tiba, gari la kubebea wagonjwa, mtambo wa kuzalishia oksijini, vifaa vya kitengo cha damu salama, na usambazaji wa lori la mizigo kwa Idara ya Bohari ya Dawa Zanzibar, ukaguzi ulibaini kuwa, Kamati ya Tathmini haikutia saini hati za kiapo ambazo zinatoa utambulisho wa mjumbe kutokuwa na mgongano wa kimaslahi wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Kutokusainiwa kwa hati ya kiapo kunaweza kukapelekea kujitokeza kwa viashiria vya kutokuwepo kwa uadilifu au kujitokeza kwa upendeleo katika mchakato wa tathmini kwa baadhi ya wajumbe na hatimae kumzawadia mzabuni asie na sifa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha Mkuu wa kitengo cha Ununuzi na Usambazaji anapitia na kusimamia kamati ili kuhakikisha inazingatia mahitaji ya kisheria wakati wa mchakato wa tathmini.

### 6.7.6.10 Uwepo wa Vifaa Tiba vyenye thamani ya shilingi 107,732,000 ambavyo havifanyi kazi

Kanuni ya 5(2) (d) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 inaeleza kuwa maafisa, wajumbe wa Bodi za Zabuni na Afisa Masuuli kuhakikisha bidhaa zinazonunuliwa ziko katika ubora wa kuridhisha.

Wakati wa ukaguzi na majadiliano na mtumiaji wa vifaa tiba, ukaguzi ulibaini kuwa, Hospitali ya Wilaya ya Kitogani na Hospitali ya Abdullah Mzee Pemba ndio hospitali pekee zilizoanza kutumia Vifaa Tiba. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa, vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi 107,732,000 havitumiki kutokana na ubovu wa vifaa kama inavyoonekana kwenye jadweli hapo chini.

### Jadweli Nambari 65: Thamani ya vifaa vya matibabu ambavyo havitumiki kwa sababu ya kasoro

| Jina la Hospitali | Vifaa | Idadi | Bei (Tsh) | Jumla (Tsh) |
|---|---|---|---|---|
| Kitogani | Mtambo wa kukuza watoto (Neonatal Incubators) | 2 | 5,266,000 | 10,532,000 |
| Abdullah Mzee | Kabati la kuwekea vifaa tiba (Instrument Dry Cabinet) | 1 | 22,000,000 | 22,000,000 |
| | Meza ya Upasuaji (Operating Table) | 2 | 21,000,000 | 42,000,000 |
| | Kifaa cha kupimia mgonjwa cha kuhamishika (Movable patient monitor) | 5 | 1,500,000 | 7,500,000 |
| | Kitanda cha kubebea Wagonjwa (Patient Stretcher) | 1 | 3,700,000 | 3,700,000 |
| | Mtambo wa kupumulia (Anathetic Machine) | 2 | 11,000,000 | 22,000,000 |
| **Jumla** | | | | **107,732,000** |

*Chanzo: Uthibitishaji wa Wakaguzi wakati wa Ziara*

Katika hatua nyengine, vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi 107,732,000 vimegundulika kuwa na hitilafu ndani ya muda mfupi baada ya kununuliwa kutokana na kasoro za kimsingi. Ukosefu wa zana hizi muhimu za tiba huibua ishara juu ya kuhakikisha ubora na uimara wa vifaa, jambo linaloweza kuhatarisha huduma za wagonjwa na shughuli za watoa huduma za afya.

Hata hivyo, kumbukumbu zinaonyesha kuwa katika Hospitali ya Abdullah Mzee, vifaa tiba vililetwa tarehe 1 Mei, 2023 na uhakiki ulifanyika tarehe 26 Mei, 2023 na vifaa vingine visivyotumika kusubiri kukamilika kwa ukarabati. Kuna hatari ya kuwa na vifaa tiba vyenye kasoro kwa sababu vitu vingine havikutumika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafanya uchunguzi wa utendaji kazi kwa bidhaa zote zilizopokelewa katika hospitali zote na zile ambazo hazifanyi kazi ipasavyo zirudishwe.

### Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na Usimamizi wa Mikataba

Usimamizi wa mikataba ulitathminiwa kwa kuzingatia usimamizi wa mradi mkuu kwa kuhusu muda, ubora na gharama. Tathmini hiyo ililenga katika maendeleo ya kazi, udhibiti wa ubora na taratibu za uhakiki, kufuata masharti ya nyaraka za mkataba, na kufuata matakwa ya mahitaji kimkataba. Maelezo ya vipengele hivi vyote yanawasilishwa katika sehemu inayofuata.

#### 6.7.6.11 Kutokukaguliwa kwa Gari zenye thamani ya shilingi 2,328,912,322

Ukaguzi ulibaini kuwa jumla ya gari 17 zenye thamani ya shilingi 2,328,912,322 zilizopokelewa na Wizara ya Afya, kati ya hizo gari 12 zenye thamani ya shilingi 1,974,324,600 kwa ajili ya kubebea wagonjwa na gari 5 za mizigo zenye thamani ya shilingi 354,587,722 zilizopokelewa kutoka kwa wazabuni mbali mbali, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa ushahidi wa kukaguliwa kwa gari hizo na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS).

Kukosekana kwa uthibitisho wa kukaguliwa kwa gari hizo kunaashiria uwezekano wa ukiukwaji wa viwango vya usalama na ubora jambo ambalo linaweza kusababisha hatari mbalimbali kama vile ajali, uchafuzi wa mazingira na miundombinu ya barabara.

Tarehe 12 Juni 2023, Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa (CMS) alitoa barua yenye kumbukumbu namba WA/CMS/125/2022/23 kwenda kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya Zanzibar kueleza juu ya kukabidhiwa kwa lori 5 za mizigo kwa ajili ya Bohari Kuu ya Dawa kutoka EICHER ya nchini India.

Pamoja na barua hiyo ya Mkurugenzi wa Bohari Kuu ya Dawa CMS, aliambatanisha barua kwa Afisa Usafirishaji ya tarehe 29 Februari, 2023 iliyoeleza masuala ya kitaalamu baada ya ukaguzi wa Lori za Mizigo na kubaini kuwepo kwa dosari 2 kwenye Lori za Mizigo kama ifuatavyo: -

- **Ukosefu wa ufungaji wa kipooza joto (AC) katika lori la Mizigo**

Afisa Usafirishaji huyo alieleza kukosekana kwa usalama wa matumizi ya gari hizo hasa nyakati za mvua kwani husababisha kioo cha mbele kufanya ukungu na kusababisha dereva kutoona vizuri mbele.

- **Muundo wa Bodi ya gari ya mzigo umetengenezwa kwa Bati na sio kwa Aluminium**

Muundo wa Bodi ya juu ya Gari ya mzigo imetengenezwa kwa bati ambayo husababisha joto kali wakati wa jua jambo ambalo hupelekea kujitokeza kwa joto kali na kutokuwa salama kwa uhifadhi wa dawa wakati wa safari za usambazaji wa madawa kwenye vituo.

Uwepo kwa hali hii umesababishwa na uongozi wa Wizara ya Afya na msambazaji kutozingatia vigezo vya gari za kusambazia dawa jambo ambalo linaweza kupelekea kujitokeza kwa hasara za uharibifu wa dawa utakaotokana na uwepo wa joto kali wakati wa usambazaji wa dawa vituoni na hatimae kuisababishia hasara Serikali kutokana na uhifadhi usio salama kwenye magari wakati wa usambazaji.

Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa dosari mbali mbali ambazo zinatokana na muundo wa bodi ya gari ya mzigo kutengenezwa kwa bati na sio kwa aluminium. Dosari hizo ni kama zifuatazo: -

- **Uwepo wa kutu (Rust) zilizojitokeza ndani ya bodi ya Gari ya Kusambazia Dawa**

Ukaguzi ulibaini ubora wenye mashaka kwenye gari za mzigo za kubebea dawa yaliyotolewa yalikuwa na kutu ndani ya bodi la kubebea dawa kama ilivyoonekana kwenye Picha nambari 3(a)hapa chini.

### Picha Nambari 5: Hali ya uchakavu wa gari za kubebea dawa



*Picha 3(a): Picha hii inaonyesha Kutu ndani ya Bodi ya kubebea dawa*



*Picha 3(b): Picha hii inaonyesha gari lilobadilishwa*

- **Lori lililobadilishwa Ndani ya Nchi**

Ukaguzi ulibaini kuwa utengenezaji wa gari kwa kebini la chuma hauko katika njia sahihi. Kulikuwa na kipande cha ubao ambacho kilibainika kuwa kiunganishi kama inavyoonekana kwenye Picha 3(b) hapo juu. Hizi pia zinaweza kuathiri urekebishaji wa ufundi wa uhandisi na usalama wa gari.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha gari zote zinawasilishwa Taasisi ya Viwango Zanzibar kwa ajili ya ukaguzi na ushauri wa kiufundi kabla ya kupokelewa ili kuepuka kujitokeza kupokea bidhaa zilizo chini ya kiwango.

### 6.7.6.12 Kutokuwasilishwa kwa Hati ya Dhamana yenye thamani ya shilingi 14,548,067,211

Kwa mujibu wa kifungu cha 9.1 cha Masharti Maalum ya Mkataba kinaeleza kuwa dhamana ya utendaji kazi itakuwa ni asilimia 10 ya thamani ya mkataba na itawasilishwa siku 30 baada ya kupokea taarifa ya tuzo.

Ukaguzi ulipitia ripoti za utendaji zilizowasilishwa kwa ajili ya usambazaji na mikataba ya vifaa tiba na kubaini kuwa wazabuni 2 kati ya 10 walifanikiwa kuwasilisha hati ya dhamana za utendaji kazi Wizarani kama inavyoonekana kwenye jadweli hapo chini.

Kati ya mikataba 10 iliyochambuliwa ni dhamana 2 tu za utendaji kazi zilizowasilishwa na wazabuni kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa kwenye mikataba. Hii inawakilisha kiwango cha kufuata cha asilimia 20 pekee, ikionyesha kiwango cha juu cha kutofuata majukumu ya kimkataba kuhusu uwasilishaji wa hati ya dhamana ya kazi.

**Jadweli Nambari 66: Hali ya uwasilishaji wa dhamana ya kazi**

| Namba | Jina la Mkataba | Mkandarasi | Dhamana ya Utendaji Iliyowasilishwa | Kiasi cha thamani ya mkataba kilichokuwa hakijawasilishwa(Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Usambazaji wa Gari 12 za kubebea Wagonjwa (Ambulance) | Zenj Motors Co LTD | Haijawasilishwa | 1,974,324,600 |
| 2 | Usambazaji wa vifaa tiba | M&D Chemical and surgical LTD | EBL / 3003 / PBG300086122 | 3,940,818,000 |
| 3 | Usambazaji wa bidhaa za afya kwa hospitali za wilaya | LAB Equip LTD | Haijawasilishwa | 1,364,068,000 |
| 4 | Usambazaji wa bidhaa za afya kwa hospitali za wilaya | LAB Equip LTD | Haijawasilishwa | 1,887,645,770 |
| 5 | Ugavi wa vifaa tiba | LAB Equip LTD | Haijawasilishwa | 1,364,068,000 |
| 6 | Ugavi wa vifaa tiba | EDLINK LTD | Haijawasilishwa | 900,715,000 |

| Namba | Jina la Mkataba | Mkandarasi | Dhamana ya Utendaji Iliyowasilishwa | Kiasi cha thamani ya mkataba kilichokuwa hakijawasilishwa(Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 7 | Ugavi wa Jenereta hospitali zote | ALPHA GENERAL TRADERS LTD | Haijawasilishwa | 1,809,548,000 |
| 8 | Usambazaji wa Malori ya kubebea dawa na na vifaa tiba CMS | AFRICARRIERS LTD | Haijawasilishwa | 354,587,722 |
| 9 | Usambazaji na ufungaji na uagizwaji wa mtambo wa oksijeni kwa hospitali mbili za wilaya | HYPERMED HEALTHCARE LTD | Haijawasilishwa | 862,100,000 |
| 10 | Usambazaji wa vifaa vya kuongezewa damu kwa benki ya damu | NEBULA HEALTHCARE LTD | BOAT/60067/ged/2022 | 90,192,119 |
| **Jumla** | | | | **14,548,067211** |

*Chanzo: Hati za Mkataba na Usalama wa Utendaji, 2023*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa mikataba 8 kati ya 10 haikuwasilisha hati ya dhamana ya utendaji wao wa kimkataba na hivyo kufanya jumla ya vifaa vya jumla ya shilingi 14,548,067,211 kutolindwa kimkataba.

Kutowasilishwa kwa hati ya dhamana za utendaji kazi kama inavyotakiwa na mikataba kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma na kuisababishia hasara Serikali pindipo mzabuni atakaposhindwa kufuata masharti ya mkataba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafuata na kutekeleza taratibu za manunuzi kwa mujibu wa sheria ili kuepukana na kujitokeza kwa viashiria vya ukiukwaji wa taratibu.

#### 6.7.6.13 Hati ya dhamana iliyomaliza muda wa matumizi (Unrenewed Performance Security)

Kwa mujibu wa kifungu cha 9.1 cha Masharti ya Jumla ya Mkataba inaeleza kwamba hati ya dhamana ya utendaji kazi itakuwa sawa na asilimia 10 ya thamani ya mkataba na itakuwa halali kwa kipindi chote cha Mkataba.

Ukaguzi ulipitia ripoti za utendaji kazi zilizowasilishwa kwa ajili ya usambazaji wa vifaa tiba na kubaini kuwa hati ya dhamana ya utendaji kazi iliyowasilishwa na wazabuni ilikuwa imemaliza muda wa matumizi na haikufanyiwa mapitio mapya ya uboreshaji. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 67: Hali ya Uwasilishaji wa Hati ya dhamana wa Utendaji**

| Namba | Jina la Mkataba | Mkandarasi | Tarehe ya hati ya Dhamana iliyowasilishwa | Tarehe ya Hati ya Mkataba isiyo na dhamana | Tarehe ya kukamilika kwa mkataba |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Usambazaji vifaa tiba | M&D Chemical and surgical LTD | 22/07/2022 | 22/10/2022 | 16/06/2023 |
| 2 | Usambazaji wa vifaa vya kuongezewa damu kwa kitengo cha damu | NEBULA HEALTHCARE LTD | 21/07/2022 | 21/10/2022 | 17/04/2023 |

*Chanzo:Hati za Mkataba na hati ya dhamana ya Utendaji, 2023*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa wazabuni hawakuwasilisha hati ya dhamana ya utendaji kazi iliofanyiwa maboresho ili kuendana na muda wa mkataba uliowekwa.

Kushindwa kuwasilisha hati ya dhamana inayoendana na muda wa matumizi inaweza kupelekea Wizara kuingia katika migongano ya kimaslahi pale mzabuni atakaposhindwa kutekeleza matakwa ya kisheria ya mkataba.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unakuwa makini wakati wa upokeaji wa hati za dhamana pamoja na kufanya mapitio ya mara kwa mara ili kuwepo kwa maboresho ya hati ambazo zimekaribia kumalizika muda wake wa matumizi kwa lengo la kuepusha kujitokeza kwa viashiria vya ukiukwaji wa taratibu za manunuzi kwa mujibu wa sheria.

### 6.7.6.14 Kukosekana kwa ripoti za uchunguzi wa vifaa tiba kabla ya kupokelewa katika vituo vya Afya

Kwa mujibu wa Masharti Maalum ya Mkataba kifungu cha 10.1 kinasema kuwa msambazaji atafanya ukaguzi kwa gharama zake mwenyewe, ripoti ya ukaguzi na vyeti vitawasilishwa kwa mnunuzi siku ya usambazaji ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinatengenezwa kwa kuzingatia mkataba.

Hata hivyo, Kifungu cha 18 cha Masharti Maalum ya mkataba kinasema kuwa mzabuni atalipwa baada ya kuwasilisha, kufanya majaribio na kukabidhisha kwa vifaa, na kiasi kilichosalia cha asalimia 2 kitalipwa baada kumalizika kwa kipindi cha uangalizi.

Ukaguzi ulipitia nyaraka zilizowasilishwa pamoja na mikataba na kubaini kuwa wazabuni walishindwa kuwasilisha ripoti za Ukaguzi wa Ununuzi bidhaa ili kuweza kujiridhisha na ubora wa bidhaa kutoka kwa mtengenezaji (Manufacturer).

Aidha, Ukaguzi ulitembelea eneo la Hospitali ya Kitogani, Hospitali ya Wilaya ya Micheweni na Hospitali ya Abdullah Mzee na kubaini kuwa vifaa vilivyopokelewa vilitumika kabla ya kufanyiwa vipimo vya utaalamu wa matumizi wa vifaa hivyo jambo ambalo limesababishwa na usimamizi duni wa mikataba ya usambazaji wa vifaa tiba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kunakua na usimamizi mzuri wa mikataba kwa kuhakikisha kwamba bidhaa zinazowasilishwa katika vituo vya Afya vinafanyiwa uchunguzi wa kina kabla ya matumizi ili kuondoa madhara yanayoweza kujitokeza kwa watumiaji.

### 6.7.6.15 Malipo ya ziada ya shilingi 516,802,320 yaliolipwa kinyume na masharti maalum ya Mkataba

Kwa mujibu wa kifungu cha 18.6 cha Masharti Maalum ya Mkataba kinaeleza kuwa malipo ya wazabuni yanatakiwa kulingana na hali ya utoaji huduma.

Ukaguzi ulipitia nyaraka za mkataba kwa ajili ya usambazaji wa vifaa kwa ajili ya kutathmini hali halisi utoaji wa huduma mbalimbali na kubaini uwepo wa malipo ya ziada ya shilingi 516,802,320, yaliotokana na wazabuni 2 kati ya wazabuni 10 kufanyiwa malipo ya ziada kinyume na masharti maalum ya mkataba. Hali halisi ni kama inavyoonekana kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 68: Hali ya Malipo ya Wazabuni kuhusiana na Kazi waliyofanya**

| Jina la Mradi | Asilimia ya malipo Iliolipwa hadi Tarehe ya Utoaji wa Vifaa (%) | Asilimia iliotakiwa kulipwa hadi Tarehe ya Utoaji wa Vifaa (%) | Ziada/ Upungufu (%) | Kiasi cha ziada kilicholipwa (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| Usambazaji wa gari za wagonjwa | 100 | 100 | 0 | - |
| Vifaa vya Hospitali | 89 | 80 | 9 | 354,673,620 |
| Usambazaji wa Bidhaa za Afya kwa Hospitali ya Panga Tupu na Kivunge | 20 | 70 | -50 | - |
| Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa Hospitali Mpya ya Mkoa iliyopo Lumumba | 20 | 0 | 20 | - |
| Usambazaji wa Bidhaa za Afya kwa Hospitali za Mwera Pongwe na Kitogani | 30 | 80 | -50 | - |
| Usambazaji na Ufungaji wa Jenereta kwa Hospitali zote za Wilaya | 40 | 0 | 40 | - |
| Usambazaji wa Vifaa vya kusafishia damu kwa Hospitali | 76 | 80 | -4 | - |
| Vifaa vya Hospitali | 98 | 80 | 18 | 162,128,700 |
| Usambazaji wa Mtambo wa wa kuzalishia Oksijini | 90 | 90 | 0 | - |
| Usambazaji wa gari 5 za mizigo | 69 | 70 | -1 | - |

*Chanzo: Kumbukumbu za malipo ya Mzabuni na Mikataba, 2023*

Hali hii inaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za Serikali kutokana na kushindwa kusimamia ipasavyo vipengele vilivyoainishwa katika masharti maalum ya mkataba.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha kuwa ziada ya fedha iliolipwa inasimamiwa ipasavyo ili kuepusha kujitokeza kwa upotevu wa fedha za Serikali.

### 6.7.6.16 Udhibiti usioridhisha wa nyongeza ya Muda wa Mkataba

Ukaguzi ulipitia uchambuzi wa nyongeza ya muda wa mkataba, na kubaini kuwa uhalali wa nyongeza hizo haukuweza kusimamiwa ipasavyo jambo ambalo lilipelekea jumla ya mikataba 8 kati ya mikataba 11 kuchelewa kuwasilishwa kwa wazabuni kwa wakati, hata hivyo kati ya mikataba 8 mikataba 5 ilipewa nyongeza ya muda kwa wazabuni na mikataba 3 haikuweza kupewa muda wa nyongeza na kupelekea kushindwa kutoa vifaa tiba ndani ya muda uliokusudiwa, hali halisi ni kama inavyooneka katika jedwali hapo chini: -

**Jadweli Nambari 69: Hali ya Kuongeza Muda**

| Namba | Jina la Mradi | Tarehe ya Mwisho ya nyongeza | Tarehe halisi ya Uwasilishaji wa bidhaa | Idadi ya siku zilizoongezeka |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Usambazaji wa gari ya wagonjwa | - | 28/06/2023 | |
| 2 | Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa Hospitali za Wilaya za Chumbuni, Magogoni, Mbuzini, Vitongoji na Micheweni - Pemba | 28/01/2023 | 16/06/2023 | 139 |
| 3 | Usambazaji wa Bidhaa za Afya kwa Hospitali ya Pangatupu na Kivunge | 13/09/2022 | 09/06/2023 | 269 |
| 4 | Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa Hospitali Mpya ya Mkoa iliyopo Lumumba | 30/04/2023 | 09/06/2023 | 40 |
| 5 | Usambazaji wa Bidhaa za Afya kwa Hospitali za Mwera Pongwe na Kitogani | 15/02/2023 | 09/06/2023 | 114 |
| 6 | Usambazaji na Ufungaji wa Jenereta kwa Hospitali zote za Wilaya | 20/05/2023 | 20/05/2023 | 0 |
| 7 | Vifaa vya kusafishia Damu vya Hospitali | - | 10/03/2023 | |
| 8 | Usambazaji wa Vifaa Tiba katika Hospitali ya Abdulla Mzee | 30/04/2023 | 01/05/2023 | 1 |
| 9 | Usambazaji wa Mtambo wa kuzalishia Oksijini | - | 20/01/2023 | |
| 10 | Usambazaji wa gari 5 | - | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa mikataba uliofanywa na Wakaguzi, 2023*

Jadweli hapo juu linaonyesha kuwa jumla ya mikataba 3 imezidi muda kwa zaidi ya tarehe ya nyongeza iliotolewa ambapo ilivuka kwa zaidi ya siku 114 hadi 269 na kupelekea ucheleweshwaji wa mapokezi ya vifaa kwa wakati.

Uchelewaji wa kupokea vifaa kwa wakati licha ya wazabuni kuongezewa muda wa ziada kumechangiwa na usimamizi duni wa watendaji wa Wizara ya Afya kulikosababishwa na kukosekana na Msimamizi wa mradi ambae angekuwa na kazi ya kusimamia na kufuatilia wazabuni katika uwasilishaji wa bidhaa kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuongeza umakini katika kusimamia na kufuatilia hatua zote za utekelezaji wa mradi ili kuepusha kujitokeza kutokupatikanwa kwa huduma zilizokusudiwa kwa wakati.

### 6.7.7 MRADI WA UNUNUZI NA USAMBAZAJI WA GARI 12 ZA KUBEBEA WAGONJWA

Wizara ya Afya ilisaini hati ya mkataba yenye kumbukumbu Na. SMZ/IMF/HO3/G/EP/2021 /2022/04 ya tarehe 23 Juni, 2022 na Mzabuni M/S Zenji Motors kwa thamani ya shilingi 1,974,324,600 pamoja na VAT kwa ajili ya Usambazaji wa gari 12 za kubebea wagonjwa kwa ajili ya vituo mbali mbali Unguja na Pemba

Kazi hiyo ilifanyika kwa njia ya kawaida ya ununuzi ambapo Wizara ya Afya Zanzibar ilitayarisha nyaraka ya zabuni na mahitaji ya bidhaa, kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 70: Taarifa za Mkataba wa ununuzi wa gari za kubebea wagonjwa**

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Nambari ya mkataba | SMZ/IMF/HO3/G/EP/2021/2022/04 |
| Jina la Mzabuni | Zenji Motors |
| Tarehe ya Kusainiwa kwa mkataba | Juni 23, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza kwa mkataba | Juni 23, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Miezi 3 |
| Tarehe ya Kukamilisha | Septemba 23, 2022 |
| Mkataba wa awali pamoja VAT | 1,974,324,600.00 |
| Mkataba wa Urekebishaji pamoja na VAT | - |
| Maendeleo ya Kazi (%) hadi Julai, 2023 | 100% |
| Asilimia ya malipo hadi Julai 2023 wakati wa ukaguzi | 100% |

**Matokeo ya Ukaguzi kuhusiana na usimamizi wa Mkataba**

Ukaguzi ulitathmini kiwango ambacho Wizara ya Afya ilihakikisha usimamizi mzuri wa gharama za mradi ikiwemo usimamizi wa malipo, uidhinishaji wa muda wa nyongeza, uzingatiaji wa marekebisho ya bei yalizangatia masharti ya mkataba, ilitathmini matumizi na uwajibikaji wa malipo juu ya fedha za dharura. Pamoja na tathmini hio iliofanywa, Ukaguzi ulibaini uwepo wa dosari mbalimbali ambazo zinapaswa kuchukuliwa hatua za marekebisho ili zisiweze kujitokeza kwa kipindi kijacho.

### 6.7.7.1 Malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani ya shilingi 252,000,000 yaliozuiwa kinyume na utaratibu

Kwa mujibu wa mkataba wenye nambari SMZ/IMF/HO3/G/EP/2021/2022/04 wa tarehe 23 Juni, 2022 wenye thamani ya shilingi 1,974,324,600 pamoja na VAT ambapo Wizara ya Afya ilifanya ununuzi wa gari 12 za kubebea wagonjwa katika vituo mbalimbali vya Afya kwa mzambuni M/s Zenj Motors.

Ukaguzi ulipitia barua yenye kumbukumbu nambari WN/ORFM/EXEMP/TA/2022/VOL. VI/269 kutoka Afisi ya Rais fedha na Mipango na kwenda Mamlaka ya Mapato Zanzibar na kubaini kuwa Serikali ilitoa msamaha wa VAT kwa Usambazaji wa Magari hayo, hata hivyo Wizara ya Afya ilizuia asilimia 15 ya VAT kwa ajili ya Ununuzi wa gari hizo.

Hali hii inaweza kupelekea upotevu wa fedha za Serikali endapo Msambazaji wa magari atawasilisha madai katika Mamlaka ya Mapato Zanzibar kwa lengo la kupatiwa kiasi cha fedha kilichozuiwa na Wizara ya Afya.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unaongeza umakini katika usimamia miongozo mbalimbali inayotolewa ili kuepusha uwezekano wa kujitokeza upotevu wa fedha za Serikali pamoja na kuhakikisha kwamba fedha iliozuiwa inarudishwa Serikalini kwa ajili ya kupangiwa matumizi mengine.

## 6.7.8 UNUNUZI NA USAMBAZAJI WA GARI 5 ZA KUBEBEA DAWA

Wizara ya Afya ilisaini hati ya mkataba yenye kumbukumbu Na. SMZ/IMF/HO3/G/EP-ICT/2021/2022/03- LOT 3 ya tarehe 29 Juni, 2022 na Mzabuni M/S AFRICARRIES LTD kwa thamani ya shilingi 354,587,722.60 pamoja na VAT kwa ajili ya Usambazaji wa gari 5 za kubebea dawa kwa ajili ya vituo mbali mbali Unguja na Pemba.

Kazi hiyo ilifanyika kwa njia ya kawaida ya ununuzi ambapo Wizara ya Afya Zanzibar ilitayarisha nyaraka ya zabuni na mahitaji ya bidhaa, kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 71: Taarifa ya Mkataba kwa gari 5 za kubebea dawa

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba | SMZ/IMF/HO3/G/EP-ICT/2021/2022/03- LOT 3 |
| Jina la Mkandarasi | AFRICARRIES LTD |
| Tarehe ya Kusaini | Juni 29, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza | Juni 29, 2022 |
| Muda wa Mkataba | Miezi 3 na miezi 12 ya kipindi cha udhamini |
| Tarehe ya Kukamilika | Septemba 29, 2022 |
| Tarehe ya Kukamilisha Iliyorekebishwa | |
| Mkataba wa awali wa VAT | 354,587,722.60 |
| Mkataba wa Urekebishaji wa Jumla na VAT | |
| Maendeleo ya Malipo (%) hadi Januari 2023 wakati Ukaguzi uliofanyika | 69% |

**Dosari zinazohusiana na Ununuzi wa wazabuni**

Katika ukaguzi uliofanyika umepitia mchakato wa ununuzi wa zabuni na kubaini uwepo wa dosari mbalimbali ambazo zimepelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama za mkataba kulikosababishwa na kutokuzingatiwa thamani halisi ya fedha, miongoni mwa dosari hizo ni kama zifuatazo: -

### 6.7.8.1 Ongezeko la Gharama ya Mkataba shilingi 55,000,000

Kwa mujibu wa kifungu cha 37 cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshwaji wa Mali za Umma ya 2016 kinataka manunuzi yote yafanyike kwa kuzingatia uchumi na ufanisi.

Katika Mapitio ya mikataba imebainika mnamo tarehe 29 Disemba, 2021 Wizara ya Afya ilitangaza zabuni ambapo tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni hio ilikua ni tarehe 14 Januari 2022, Ukaguzi umebaini jumla ya wazabuni 2 waliwasilisha hati ya zabuni kwa mujibu wa utaratibu kama inavyobainika katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 72: Wazabuni waliowasilisha hati ya zabuni

| Mzabuni | Kiasi cha Fedha (Tsh) | Kodi ya Ongezeko la Thamani (Tsh) |
|---|---|---|
| Zenji Motors Co. Limited, | 1,010,729,000 | 154,179,000 |
| Comfix & Engineering Small solution | 750,000,000 | 112,500,000 |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi, 2023*

Katika jadweli lililopo hapo juu Ukaguzi ulibaini kamati ya tathmini ilionyesha kuwa mzabuni M/S Comfix & Engineering Small Solution hakuwasilisha leseni ya biashara ya kuuza gari ambapo kipindi cha uhalali wa zabuni ulikuwa siku 90 badala ya siku 120 na fomu ya bei haikuwa kama ilivyoainishwa katika hati ya zabuni.

Aidha, fomu ya bei ya M/S Zenji Motors Co. Limited haikuwa kama ilivyoainishwa katika hati ya zabuni ambapo ilibainika gari inayowasilishwa itatoka nchini Dubai wakati jadweli la bei ilionyesha kuwa kitambulisho cha nchi asilia cha Dubai.

Ukaguzi umebaini kwa mujibu wa kikao cha Kamati ya Tathmini kilipendekeza katika hatua ya awali wazabuni wote kutokukidhi vigezo vilivyowekwa na kushauri kutokutolewa kwa tuzo ya zabuni.

Kutokana na hali hio ukaguzi ulishangazwa juu ya kitendo cha kamati ya tathmini kuamua kuzifuta zabuni hizo kwa kisingizio cha kutokukidhi vigezo jambo ambalo ni kinyume na uhalisia.

Kutokana na kufutwa kwa zabuni hizo mnamo tarehe 9 Machi 2022, zabuni ya usambazaji wa lori 5 za mizigo kwa Hospitali za Zanzibar zilitangazwa tena na tarehe ya mwisho ya kuwasilisha ilikuwa tarehe 23 Machi 2023, ambapo jumla ya wazabuni watatu waliwasilisha upya maombi yao kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 73: Uwasilishwaji wa Zabuni za Ununuzi wa gari 5

| Mzabuni | Kiasi cha Fedha (Tsh) | Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) |
|---|---|---|
| Zenji Motors Co. Limited, | 978,650,000 | 127,650,000 |
| Comfix & Engineering Small solution | 828,000,000 | 124,200,000 |
| Africarriers Limited | 299,587,722 | - |

*Chanzo: Uchambuzi wa Wakaguzi, 2023*

Hata hivyo mnamo tarehe 10 Agosti, 2022 uongozi wa Wizara ya Afya ulifanya kikao cha majadiliano na mzabuni M/S Africarriers kwa ajili ya kupewa mkataba wa usambazaji wa gari 5 za Mizigo kwa Bohari ya Dawa ya Kituo cha Zanzibar kwa shilingi 354,587,722 pamoja na VAT ambapo mzabuni huyo alikubali kupokea barua ya kujuulishwa kuwa mshindi (notification letter) ambapo mnamo tarehe 29 Septemba, 2022 hati ya mkataba ilisainiwa yenye thamani ya shilingi 354,587,722.60 baina ya Wizara na M/S Africarriers Limited. Dosari mbalimbali zilibainika kama ifuatavyo: -

- Kutokutelekezwa kwa maamuzi halali ya kikao cha Kamati ya Tathmini kilichoshauri kufutwa kwa zabuni hiyo kutokana na wazabuni wote kukosa sifa za awali.
- Kujitokeza kwa ongezeko la shilingi 55,000,000 baada ya kikao cha majadiliano kilichofanyika ambapo hadi ukaguzi unakamilika hatukuweza kupatiwa maelezo na vielelezo vilivyopelekea kujitokeza kwa ongezeko la gharama za mkataba wa awali ambapo Mzabuni aliwasilisha hati ya zabuni yenye thamani ya shilingi 299,587,722 na hatimae kuzawadiwa tuzo yenye thamani ya shilingi 354,587,722.60.
- Kujitokeza kwa ukiukwaji wa taratibu, kanuni na sheria zilizompa Mamlaka Mhe. Waziri wa Afya kupata uhalali wa kisheria kuwa Mwenyekiti wa Kikao cha majadiliano (negotiation team) kilichofanyika tarehe 10 Agosti, 2022.

Kutokana na dosari zilizobainika hapo juu ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unatekeleza maamuzi halali ya kikao cha tathmini ili kuepuka kutoa zabuni kwa mzabuni ambae hana sifa na hatimae kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma pindipo mzabuni huyo atakaposhindwa kutekeleza matakwa ya mkataba husika.

### 6.7.9 MRADI WA UNUNUZI NA USAMBAZAJI WA VIFAA VYA KUSAFISHIA DAMU

Wizara ya Afya ilisaini hati ya mkataba yenye kumbukumbu Na. SMZ/IMF/HO3/G/EP-ICT/2021/2022/01- LOT 2 ya tarehe 29 Juni, 2022 na Mzabuni M/S NEBULA HEALTHCARE kwa thamani ya shilingi 90,192,119 pamoja na VAT ununuzi na usambazaji wa vifaa vya kusafishia damu kwa ajili ya vituo mbalimbali Unguja na Pemba.

Kazi hiyo ilifanyika kwa njia ya kawaida ya ununuzi ambapo Wizara ya Afya Zanzibar ilitayarisha nyaraka ya zabuni na mahitaji ya bidhaa, kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 74: Taarifa ya Mkataba wa vifaa vya kusafishia damu**

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Nambari ya Mkataba | SMZ/IMF/HO3/G/EP-ICT/2021/2022/01- LOT 2 |
| Jina la Mkandarasi | NEBULA HEALTHCARE |
| Tarehe ya Mkataba | Juni 29, 2022 |
| Tarehe ya Kuanza | Juni 29, 2022 |

| Kipengele | Taarifa katika Mkataba |
|---|---|
| Muda wa Mkataba | Miezi 3 |
| Tarehe ya Kukamilisha | Septemba 29, 2022 |
| Mkataba wa awali pamoja na VAT | Tsh.90,192,119.00 |
| Mkataba wa Maboresho pamoja na VAT | - |
| Asilimia ya malipo hadi Julai 2023 wakati wa Ukaguzi | 75% |

### Dosari zinazohusiana na Upangaji na Usambazaji wa vifaa vya kusafishia damu

Ukaguzi ulifanya tathmini ya kina inayohusiana na upangaji na usambazaji wa vifaa vya kusafishia damu vilivyowasilishwa na wazabuni kwa kufanya mazingatio ya usimamizi wa malipo, usimamizi wa mchakato wa manunuzi, usambazaji wa vifaa katika vituo mbalimbali Unguja na Pemba pamoja na kuangalia ubora wa vifaa vilivyowasilishwa kabla ya kuanza kutumika. Pamoja na kuzingatia majukumu hayo ukaguzi uliweza kubaini dosari mbalimbali ambazo ziliwasilishwa kwenye Uongozi wa Wizara ya Afya na kuahidi kuchukuliwa hatua za marekebisho ili kunusuru kujitokeza kwa viashiria vya matumizi mabaya ya rasilimali za Umma, hali halisi ya dosari hizo ni kama zinavyoonekana hapo chini: -

#### 6.7.9.1 Utayarishaji duni wa Vigezo vya Kiufundi kwa Usambazaji wa Vifaa vya kuongezewa Damu

Kwa mujibu wa kanuni ya 142(5) ya Kanuni za Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020, Taasisi ya Ununuzi na Uondoaji wa mali haitaandaa zabuni ya ujenzi isipokuwa michoro na vipimo vya kiufundi vimekamilika na makisio thabiti ya gharama yameandaliwa.

Ukaguzi ulipitia maelezo ya mkataba wa usambazaji wa vifaa tiba ili kutathmini kwa kina vipimo vya kiufundi vilivyotayarishwa na kubaini kuwa mchakato wa ununuzi wa vifaa vya kuongezewa damu hauna mpangilio uliofafanua vizuri vigezo vya kiufundi. Mkataba uliotayarishwa haukuwa wazi, haukukamilika na haukushughulikia vya kutosha vipengele muhimu vya uteuzi na ununuzi wa vifaa. Yafuatayo yalibainishwa kama dosari katika hati ya mkataba kama ilivyo kwenye jadweli hapo chini.

### Jadweli Nambari 75: Kutofanyika kwa Maandalizi ya kutosha ya vipimo vya vifaa Tiba

| Mradi | Mapungufu yaliyobainika |
|---|---|
| Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa ajili ya huduma za Kitengo cha Damu salama | Ununuzi wa vichochezi (plates agitator) kwa ajili ya huduma ya kitengo cha Damu Salama Zanzibar |
| | Ununuzi wa Mchanganyiko wa Ukusanyaji wa Damu kwa ajili ya kuongezewa damu Zanzibar |
| | Ununuzi wa kifungashio cha damu kwa ajili ya kuongezewa damu Zanzibar |
| | Ununuzi wa jokofu kwa ajili ya kuongezewa damu Zanzibar |

*Chanzo: Uchambuzi wa Fomu ya Mkataba uliofanywa na wakaguzi, 2023*

Kutoandaliwa kwa vigezo vya kiufundi kunaweza kuathiri upangaji wa mradi na uangalizi na kuweza kusababisha kushindwa kushirikisha wahusika muhimu wa mradi kama vile wataalamu wa tiba, wataalam wa Ununuzi, Bodi ya Zabuni kama sehemu ya mchakato wa ununuzi, watengenezaji wa vifaa na mchakato wa kuandaa vipimo vya kiufundi.

Kutoandaliwa kwa vigezo vya kiufundi vilivyoainishwa kwenye vifaa vya kuongezewa damu kunaweza kuwa na athari mbalimbali kama vile:

**Utendaji Usiotija:** Vifaa vilivyonunuliwa huenda visifikie viwango vinavyohitajika vya utendaji kazi, hivyo kuathiri ubora wa uchangiaji damu kwa mgonjwa.

**Ushauri wa Kiusalama:** Vifaa bila vipimo sahihi vya usalama vinaweza kuleta hatari kwa wagonjwa na watoa huduma za afya.

**Kutoendana:** Kutoendana na miundombinu na mifumo iliyopo kunaweza kusababisha utendajikazi usiofaa na kuongezeka kwa mahitaji ya matengenezo.

**Ugumu wa kupata Vipuri**: Wakati kifaa hakiwezi kutoa huduma hivyo itakuwa vigumu kutafuta sehemu sahihi ya vipuri vinavyohitajika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara kwa kushirikiana na ZBS kuhakikisha unafanya ukaguzi wa ubora wa vifaa tiba vilivyonunuliwa ili viweze kuendana na gharama halisi ya fedha iliyotumika kwa kuzingatia ubora na ufanisi na hatimae kuweza kufanya kazi kwa muda mrefu.

### Dosari zinazohusiana na Usimamizi wa Mkataba


Ukaguzi ulitathmini kiwango ambacho Wizara ya Afya ilihakikisha usimamizi mzuri wa gharama za mradi ikiwemo usimamizi wa malipo, uidhinishaji wa muda wa nyongeza, uzingatiaji wa marekebisho ya bei yalizangatia masharti ya mkataba, ilitathmini matumizi na uwajibikaji wa malipo juu ya fedha za dharura. Pamoja na tathmini hio iliofanywa, Ukaguzi ulibaini uwepo wa dosari mbalimbali ambazo zinapaswa kuchukuliwa hatua za marekebisho ili zisiweze kujitokeza kwa kipindi kijacho.

### 6.7.9.2 Kutokufanyika kwa huduma za maboresho "services and maintanance" kwa mashine zilizosambazwa kwa wakati

Mnamo tarehe 31 Julai, 2023 ukaguzi ulitembelea maeneo mbalimbali ya miradi ya hospitali na kubaini uwepo wa mitambo iliyonunuliwa na kufanya kazi katika maeneo mbali mbali ya Wizara ya Afya bila ya kufanyiwa matengenezo ndani ya kipindi cha uangalizi ambapo kwa mujibu wa muda wa uangalizi mashine hizo zilitakiwa kufanyiwa huduma za maboresho "service and maintanance" tarehe 20 Julai, 2023 ili kuweza kufanya kazi na kutoa huduma zilizobora kwa ufanisi.

Katika utembeleaji wa maeneo ya mradi uliofanyika ukaguzi umebaini hadi tunakamisha ukaguzi uwepo wa baadhi ya mashine kutokufanyiwa matengenezo kwa wakati jambo ambalo huwenda likapelekea kutoa majibu hasi ya vipimo vinavyofanyika kwa mashine hizo na hatimae kupelekea kuitia hasara Serikali kwa kushindwa kuzitunza na kuzitumia mashine hizo kwa uangalifu. Hali halisi ya mashine hizo ni kama inavyoonekana katika Picha hapo chini:-

**Picha Nambari 6: Uchelewaji wa kufanyiwa services kwa mashine hiyo ndani ya kipindi cha uangalizi**




*Chanzo: Matembezi ya maeneo ya miradi yaliyofanywa na wakaguzi, 2023*

Kushindwa kurekebisha mtambo ndani ya kipindi cha ungalizi kunaweza kusababisha kupungua kwa ufanisi wa uzalishaji, kujitokeza kwa matokeo yasiyo sahihi, kuongezeka kwa uchakavu, na ucheleweshwaji wa majibu ya vipimo.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wizara ya Afya kuhakikisha unafanyia huduma za maboresho kwa wakati ndani ya kipindi cha uangalizi ili kupunguza gharama za matengenezo zitakazojitokeza baadae kupitia fedha za Serikali.

# SURA YA SABA



# 7.0 HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Sura hii inatoa hitimisho na mapendekezo juu ya masuala muhimu yaliyojitokeza katika ripoti ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/23. Licha ya matokeo ya kina na mapendekezo ambayo tayari yameshawasilishwa katika ripoti hii, ni muhimu kwa mara nyingine tena kuikumbusha Serikali na Maafisa Masuuli kuhusu masuala muhimu na kupendekeza hatua za jumla za kuchukuliwa kama zilivyobainishwa katika Muhtasari wa Ripoti hii.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 nilifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayodhaminiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Washirika wa Maendeleo kwa kuzingatia mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu za ununuzi, utayarishaji wa taarifa za fedha na nyaraka zilizoambatishwa kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizowekwa pamoja na kuzingatia Viwango kubalifu vya Kitaifa na Kimataifa vya Taasisi za juu za hesabu zinazotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi ambazo zinahusu ukaguzi wa kisekta.

Nimetoa hati za ukaguzi kwa kuzingatia taarifa za fedha nilizozikagua na kuzitolea ripoti ya ukaguzi kwa kila taasisi ambayo niliikagua. Aidha, nilitoa barua ya ukaguzi (Management letter) zinazoonyesha dosari kwa kila Taasisi niliyoikagua na pale ambapo dosari hiyo ilikosa majibu na ushahidi sahihi ilichukuliwa na kubainishwa katika kitabu hichi kuwa ni dosari iliyokosa majibu.

Mwenendo wa hati za ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa miradi Thelathini na mbili (32) ya maendeleo ambayo imetekelezwa katika Taasisi kumi na mbili (12) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar umeimarika kwa kuonyesha kwamba Miradi kumi na saba (17) imepata Hati zinazoridhisha na Hati kumi na tano (15) ni Hati za Kushindwa kutoa maoni ambazo ni sawa na asilimia 46.87 ya Hati zote zilizotolewa.

Ni matumaini yangu kwamba watumiaji wa taarifa hii watanufaika na kujifunza kwa yale yote yaliyotekelezwa ikiwemo ubunifu mkubwa wa uanzishaji wa miradi mipya ya maendeleo pamoja na kufanya maboresho na muendelezo wa miradi iliyopita kwa kuwashirikisha wananchi na kuchukuwa mawazo yao ikiwa ni njia pekee ya kuwashirikisha katika kuibua miradi mipya ambayo itasogeza kwa kiwango kikubwa huduma za kijamii karibu na makaazi ya wananchi hao. Hata hivyo dosari zilizobainishwa kwa baadhi ya miradi zitachukuliwa kama chachu ya kuweza kufanya maboresho kwa ajili ya miradi ijayo.

Katika suala hili nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi au kunipa miongozo ya namna ya kutanua wigo wa kazi zangu katika siku zijazo.

Nichukue fursa hii kwa dhati kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukua katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uibuaji wa miradi mipya ikiwemo miradi ya masoko, miradi ya vituo vya afya, miradi ya uboreshaji ya njia za ndani, pamoja na miradi mengineyo ya kimkakati yenye lengo la kuiunganisha jamii kuwa katika kitu kimoja kwa lengo la kuimarisha maisha ya mwananchi mmoja mmoja na jamii kwa ujumla kwa kusogeza huduma za kijamii karibu na makaazi ya wananchi.

Aidha, shukurani za kipekee zimuendee Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kutuamini na kuijengea heshima kubwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake. Pamoja na shukurani hiyo niwashukuru viongozi mbali mbali wa kitaifa wanaounga mkono jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Aidha, nitakuwa mchache wa shukurani kama sitawashukuru wale wote waliochangia kwa njia moja au nyengine utekelezaji wa kazi hii ikiwemo wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Taasisi na Sekta Binafsi nilizoshirikiana nazo, wanajamii, waandishi wa habari pamoja na familia za watendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ustahamilivu wao na subira kubwa walioionesha kwa wapendwa wao wakati wa utekelezaji wa majukumu waliyokuwa nayo.

Nichukuwe fursa hii kuwaombea kheri na baraka tele zitokazo kwa muumba ziwe pamoja nao ili tuzidishiwe afya njema na uzima katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kitaifa.

Mungu Ibariki Tanzania,

Mungu Ibariki Zanzibar,

Mungu Ibariki Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**Ameen**

# KIAMBATISHO NAMBARI 1

## Kiambatisho 1: Hali ya Utendaji wa Kifedha Malipo

| Mzabuni | Kiasi cha Mkataba (Tsh) | Jumla ya kiasi kilicholipwa (Tsh) | Asilimia ya Malipo (%) |
|---|---|---|---|
| Zenji Motor | 1,974,324,600.00 | 1,974,324,600.00 | 100 |
| M&D Chemical And Surgical Ltd | 3,940,818,000.00 | 1,606,291,193.19 | 41 |
| Lab Equment Ltd | 1,364,068,000.00 | 409,220,400.00 | 30 |
| Lab Equment Ltd | 1,887,645,770.00 | 377,529,154.00 | 20 |
| Lab Equment Ltd | 1,364,068,000.00 | 272,813,600.00 | 20 |
| Alpha General Trader Ltd | 1,809,548,000.00 | 723,819,200.00 | 40 |
| Nebula Healthhcare | 90,192,119.00 | 68,686,085.20 | 76 |
| Aedlink | 900,715,000.00 | 720,572,000.00 | 80 |
| Hypermade | 862,100,000.00 | 776,104,500.00 | 90 |
| Africarries Ltd | 354,587,722.60 | 243,703,934.52 | 69 |

# KIAMBATISHO NAMBARI 2

## Kiambatisho 2: Hali ya kuongeza mkataba wa Mradi

| Jina la Mradi | Nyongeza 1 | | Nyongeza 2 | | Nyongeza 3 | | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Usambazaji wa gari za wagonjwa | Kuanza | Mwisho | Kuanza | Mwisho | Kuanza | Mwisho | Vimewasilishwa |
| Usambazaji wa Vifaa Tiba kwa Hospitali za Wilaya katika Hospitali za Wilaya za Chumbuni, Magogoni, Mbuzini, Vitongoji na Micheweni- Pemba | Januari 28, 2023 | - | - | - | - | - | Unaoendelea |
| Usambazaji wa Bidhaaza Afya Kwa Hospitali ya Pangatupu Na Kivunge | - | - | - | - | - | - | |
| Usambazaji wa Vifaa Tiba Kwa Hospitali Mpya ya Mkoa Lumumba | Januari 29, 2022 | Januari 28, 2023 | Tarehe 20 Januari, 2023 | | Januari 29, 2023<br>30 Aprili, 2023 | - | Unaoendelea |
| Usambazaji wa Bidhaa za Afya Kwa Hospitali za Mwera Pongwe Na Kitogani | Septemba 29, 2022 | 15 ya Februari, 2023. | - | - | - | - | Unaoendelea |
| Usambazaji na Ufungaji wa Jenereta kwa Hospitali zote za Wilaya | Novemba 16, 2022 | Februari 15, 2023 | Machi 30, 2023 | Mei 20, 2023 | | | Vimewalisilishwa |
| Vifaa vya kusafishia damu vya Hospitali | | | | | - | - | |
| Usambazaji wa Vifaa Tiba katika Hospitali ya Abdulla Mzee | Septemba ya 29, 2023 | Tarehe 28 Januari, 2023 | Januari 29, 2023 | Aprili 30, 2023 | - | - | Vimewalisilishwa |
| Usambazaji wa Mtambo wa kuzalishia Oksijini | - | - | - | - | - | - | Unaoendelea |
| Usambazaji wa magari 5 | - | - | - | - | - | - | Mikononi |